Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Nane – Tarehe 17 Aprili, 2008**

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

**D U A**

Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge leo kipindi cha maswali kwa Prime Minister hakipo kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameenda kumwakilisha Mheshimiwa Rais katika sherehe za kuapisha Mawaziri katika Jamhuri ya Kenya. Kwa hiyo kufuatana na kanuni zetu kama Waziri Mkuu hayupo kipindi hicho hakipo, kwa hiyo tunaendelea na utaratibu wa kawaida.

### MASWALI NA MAJIBU

Na. 95

**Fedha za Ujenzi wa Barabara**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa, fedha za ujenzi wa Barabara zimeongezeka katika Bajeti ya mwaka 2007/23008 na imehusisha Mkoa wa Mtwara pia:

(a) Je, ni kiasi gani cha nyongeza kimetengwa kwa ajili ya Wilaya ya Masasi kwa ajili ya kuhudumia Barabara za Vijijini ambazo nyingi hazijawahi kufanyiwa ukarabati kwa muda mrefu?
(b) Je, Barabara za Masasi - Matawala hadi Mpekezo na Machenje na zile za Masasi Magharibi kama Nanyindwa – Mpanyani – Nambawala n.k zitakuwepo kwa ukarabati?

(c) Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha kuwa, Wilaya ya Masasi inawezeshwa kununua vifaa vya ujenzi wa Barabara kama vile *Bulldozer D.6, Scrapers* na kadhalika. Ili iweze kutengeneza Barabara za vijijini badala ya kuwapa Makandarasi ambao hawana vifaa na hivyo kukarabati Barabara kwa viwango vya chini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimwia Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi katika mwaka wa fedha 2007/2008 imetengewa kiasi cha Sh.661,610,000/= kutoka kwenye Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya Barabara zake. Hii inaonyesha ongezeko kubwa la fedha hizo ukilinganisha na fedha zilizotolewa ka mwaka 2006/2007 ambazo ni Sh. 146,600,000/=.

Fedha za mwaka 2007/2008 zimepangwa kufanya matengenezo ya Barabara kama ifuatavyo:-

· Matengenezo ya kawaida kilomita 488 kwa shilingi 327,500,000/=.

· Matengenezo ya sehemu korofi kilomita 14 kwa shilingi 16,100,000/=.

· Matengenezo ya muda maalum kilomita 31 kwa shilingi 228,000,00/= Matengezo ya madaraja na makalvati kwa shilingi 56,000,000/=.

· Fedha kwa ajili ya usimamizi wa matengenezo ya barabara shilingi 34,000,000/=.

· Fedha ya nyongeza iliyotengwa kwa mwaka 2007/2008 (Ukilinganisha na mwaka wa fedha 2006/2007) ni shilingi 515,010,000/= sawa na 77.8%.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika barabara ya Masasi – Matawale – Mpekeso hadi Machenje na zile za Masasi Magharibi kama Nyanyindwa – Mpanyani zipo katika mpango wa kufanyiwa matengenzo ya kawaida na kutengeneza sehemu korofi ili ziweze kuptika vizuri. Kwa barabara ya Masasi – Matawale – Mpekeso hadi Machenje matengenezo hayo yataanza baada ya mvua za masika kupungua na gharama yake ni shilingi 7,045,500/=.

Kwa barabara ya Nyanyindwa – Mpanyani matengenezo yamekwishaanza kwa gharama ya shilingi 13,720,000/=. Barabara ya Mpanyani – Nambawala hadi Lukuledi imewekwa kwenye bajeti ya mwaka 2008/2009. Kilomita 12 zitafanyiwa matengenezo hayo kwa gharama ya shilingi 9,600,000/=.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa nia na makusudi ya Serikali ni kufanya shughuli zake kwa kutumia Sekta Binafsi (*Private Sector*) ili kuzuia matatizo mbalimbali yanayoletea Serikali hasara pindi inapofanya kazi yenyewe. Kazi yote ya matengenzo ya barabara zitafanywa na Wakandarasi wenye uwezo baada ya kazi hizo kutangazwa na kufanyiwa tathmini.

Hata hivyo, halmashauri ya Wilaya ya Masasi ina mitambo miwili ambayo ni *Power Grader* na kijiko (*Wheel Loader)* ambavyo hutumika kwa matengenezo mbalimbali kwenye barabara za vijijini. Katika mpango wao wa maendeleo Halmashauri ya Wilaya ya Masasi haina mpango wa kununua mitambo na badala yake wataendelea kuwatumia wakandarasi kwa shughuli za matengenezo ya barabara.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwanza namshukuru Naibu Waziri kwa kutoa maelezo mazuri ambayo yanaridhisha, lakini pamoja na hayo ningeomba kuuliza vipi fedha hizi pia zimehusisha ujenzi wa barabara katika mji mdogo wa Masasi?

Lakini nimeona barabara hizi zimeanza kutengezwa lakini wakati mvua hizi zilizopita barabara zile tayari zimeshageuka kuwa mfereji sasa mambo haya namna gani. Ni kwamba pamoja na jitihada ya *TANROAD* kukarabati madaraja yale yaliyokuwa yamezolewa na mafuriko inaonekana mpaka hivi sasa kuna matatizo makubwa katika daraja la Nango na daraja la Nanganga, sehemu hizi nazo wakati wa mafuriko maji yamepita juu ya daraja sasa Serikali itafanya nini katika kuhakikisha kwamba maji ndiyo yanayopita chini ya daraja?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za mjini Masasi kwa mwaka huu pia zina fedha kidogo kwa ajili ya matengenezo madogo madogo kwa sehemu zile ambazo zimeathirika sana kwa mvua za masika. Kwa hiyo namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba angalau kuziba viraka fedha kidogo zipo zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa upande wa madaraja ambayo yalizolewa kwa mvua zile za eli nino, madaraja hayo nakumbuka yametengenezwa na wenzetu wa *TANROAD* na tutawasiliana na wenzetu wa miundombinu kuona kwamba je, watasaidaje ili kuimarisha madaraja hayo.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa mimi naulizia barabara ya uhuru katika mkoa wa Dar es Salaam barabara hii ina historia ya kuleta uhuru katika nchi yetu lakini Serikali imeitupa barabara hii. Juzi mimi nimetukanwa, hivi Mbunge anakosa gani jamani kuhusu barabara hii ya uhuru, mimi nalia hapa mbele yako naomba barabara hii muitizame kwa jicho la huruma.

**NAIBU SPIKA:** Hata mimi nimeona kwenye *TV*.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumelipokea ombi lake tutalifanyia kazi ili tuone uwezekano wa kuwasaidia wenzetu.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuwa matatizo yaliyojitokeza wilaya ya Masasi yanafanana sana na yale yanayotokea Tunduru hasa katika barabara itokayo Tunduru kwenda Songea ambayo haipitiki miezi minne kila mwaka Je, Serikali sasa hivi iko tayari kuhakikisha kwamba barabara ile inaanza kuwekewa changarawe badala ya matope?

**NAIBU SPIKA:** Mimi namruhusu ajibu lakini hiyo ni ya *TANROAD* na Wizara ya Miundombinu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyomjibu Mheshimiwa Zungu kwa kuwa barabara hii inashughulikiwa na wenzetu wa miundombinu tutawasiliana ili kuona kwamba tutasaidiana vipi katika kuondoa adha ya barabara hiyo.

Na. 96

**Utengenezaji wa Barabara Misungwi**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya Kabale – Ng'olo hadi Mwamboku iliyokuwa itengenezwe wakati wa ugeni wa mtoto wa Mfalme wa Norway aliyetarajiwa kwenda kuona miradi iliyofadhiliwa na Norway katika shule za msingi za Nyashitanda, Mwamboku, Kisesa ilishindikana kwa sababu ya mvua zilizokuwa zinanyesha:-

(a) Je, Serikali ilifuatilia matengenezo hayo na kwamba je, barabara hiyo sasa inapitika wakati wote wa mwaka?

(b) Kama haijatengenezwa ni kiasi gani cha fedha kitatumika na lini barabara hiyo itatengenezwa?

(c) Je, barabara ya Misungwi - Nguge- Mondo itatengenezwa na Kampuni gani na kwa gharama zipi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ilifuatilia matengenezo ya barabara ya Kabale, Ng'obo hadi Mwamboku na kujenga makalvati mistari minne na kuweka changarawe zile sehemu korofi za Kabale kwa kiasi cha shilingi milioni 20. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti ya matengenezo ya barabara za Halmashauri, barabara hii haikufanyiwa matengenezo zaidi hivyo kufanya upitikaji wake hasa wakati wa mvua kuwa mgumu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Kiasi cha fedha kinachohitajika kwa matengenezo ya barabara ya Kabale – Ng'obo hadi Mwamboku ni shilingi 114 milioni. Halmashauri imekuwa ikipata fedha kutoka kwenye Mfuko wa Matengenezo ya Barabara ya fedha nyingine za miradi kutoka kwenye vyanzo mbalimbali kama "*Local Government Capital Development Grants*. Hivyo ni jukumu la Halmashauri kutumia fursa hizi katika shughuli za maendeleo ikiwamo utengenezaji wa barabara iliyotajwa. Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009 Halmashauri imeomba kutengewa shilingi milioni 10 kutoka kwenye fedha za Mfuko wa Barabara na shilingi milioni 55 kutoka kwenye mradi wa *Local Government Transport Programme (LGTP)* kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo.

(c) Barabara ya Misungwi –Nguge-Mondo yenye urefu wa kilomita 24 inahitaji matengenezo makubwa (ukarabati) kwa gharama ya jumla ya shilingi 288 milioni. Hata hivyo, Halmashauri imeomba kutengewa shilingi milioni 16 kwa mwaka wa fedha 2008/2009 kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kufanya matengenezo ya sehemu korofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya itakayotengeneza barabara ya Misungwi – Nguge – Mondo itafahamika wakati Halmashauri itakapopata fedha za matengenezo ya barabara hiyo na kutangaza zabuni ya kupata Mkandarasi atakayetengeneza barabara hiyo.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza kabla sijauliza nianze tu kwa kuipongeza Serikali hasa kwa matengenezo mazuri yaliyofanyika kwenye barabara inayosimamiwa na *TANROAD* chini ya Eng. Kadashi kazi nzuri sana tunakupongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya barabara ya Nguge, Mwaniko hadi Mondo ni mbaya kweli Waziri amekiri kwamba kunahitajika milioni 288 lakini zilizotengwa kutoka mfuko wa barabara ni milioni 16 ni pesa ndogo sana. Kutokana na majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri nimwombe tu akubaliane na ombi langu yeye mwenyewe atenge muda wake kabla ya mwezi wa Juni atembelee Misungwi aje ajionee matatizo yaliyopo na baadaye tutapata ufumbuzi wa pamoja yeye Halmashauri pamoja na mimi ili tuweze kuwahudumia wananchi wa Nguge. Naomba sana hilo alikubali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa baada ya Bunge nitakuwa na ziara katika Mkoa wa Kigoma, Tabora na Shinyanga basi nitatenga muda ili nipitie katika Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza, kwa kuwa barabara hii iliyotajwa katika swali la msingi lina shule ya sekondari ya kata Shilalo na kuna zahanati inayohudumia wananchi wa maeneo hayo ujio wa mtoto wa mfalme wa Norway wangefaidika sana wananchi wa maeneo je, Serikali sasa haioni muhimu kuweka fungu maalum maana yake wanasema yake wanasema Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi haina uwezo kuweka fungu maalum la kuhakikisha kwamba barabara ile inapitika.

**NAIBU SPIKA:** Atakapofika Waziri ataweka fungu hilo maalum.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hii ina matatizo na haipitiki vizuri na kweli mtoto wa mfalme wakati anataka kwenda katika eneo hilo yalifanyika matengenezo madogo yule mtoto hakufika. Lakini Serikali tunasema kwamba tutatenga fedha kwa awamu ili kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika. Kwa sasa uwezo wa Serikali ni kidogo bajeti ya Misungwi ni shilingi milioni 216. Barabara hiyo inahitaji milioni 288 kwa hiyo unaona kabisa kwamba Serikali itatenga fedha kwa awamu ili barabara hii iweze kupitika kwa mwaka mzima.

Na. 97

**Kufungua Tawi la NMB Kibakwe**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:

Kwa kuwa mji mdogo wa Kibakwe unakua kwa harakasana hivi sasa kutokana na kuwepo kwa umeme, mawasiliano ya simu za mkononi kukua na kuongezeka kwa watumishi wa Idara mbalimbali za Serikali hasa Idara ya Elimu, lakini pia Kibakwe ndicho kituo kikubwa cha kibiashara kinachochukua nusu ya Wilaya ya Mpwapwa.

Je, Serikali itasaidiaje kushawishi Benki ya NMB waweze kufungua Tawi katika mji mdogo wa Kibakwe?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba *NMB* haina tawi katika mji mdogo wa Kibakwe na kwamba huduma za kibenki zinahitajika katika maeneo mengi hapa nchini ikiwa ni pamoja na Kibakwe. Aidha, ufunguaji wa matawi ya benki unahitaji tathmini ya kina, ili kuweza kufahamu kama vigezo muhimu vinatimizwa. Vigezo hivyo ni pamoja na:-

(i) Mzunguko wa fedha katika eneo husika.

(ii) Miundombinu kama ulinzi, barabara, umeme, mawasiliano ya simu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusaidiana na wananchi wa mji mdogo wa Kibakwe, *NMB* itafanya tathmini katika eneo la Kibakwe kulingana na vigezo hivyo, ili kuona uwezekano wa kufungua tawi la benki hiyo hapo. Aidha, NMB pia imeuia kupanua mtandao wake kwa kufungua matawi sehemu ambazo huduma za kibenki zinahitajika kwa kuzingatia vigezo.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kuwa mzunguko una vigezo vyote alivyovisema Naibu Waziri vipo na sasa hivi mzunguko wa fedha ni mkubwa zaidi kutokana na kugundulika kwa madini ya Safaya ambayo yanathamani kubwa kuliko hata Tanzanite na hivyo wageni na watu wengi wafanyabiashara wengi ikiwa pamoja na wachimba madini wameongezeka kwa kiasi kikubwa zaidi ya 5,000 je, anaweza akanihakikishia uharaka ambao ataufanya ili kwenda kuangalia uwezekano wa kusaidia kuanzishwa kwa benki hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana vigezo vipi lakini ipo haja vilevile ya kufanya tathimini namhakikishia kwamba tutafanya haraka ili shughuli hii iweze kufanikiwa kwa ufanisi zaidi.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Ahsante sana pamoja na majibu aliyomjibu Mheshimiwa George Simbachawene nina swali dogo la nyongeza, hali ya Kibakwe inafanana kabisa na hali ya mji mdogo wa Sherui, Sherui kuna wafanyabiashara wengi na hatuna benki tunatumia benki ya NMB Igunga na NMB Kiomboi, kwa hiyo wafanyabiashara wanapata tabu. Je, nauliza ili kuwaokoa labda wafanyabiashara na majambazi na hali ya hatari wako tayari sasa kuishawishi benki ya NMB ikawa na mobile benki japo kwa siku mbili za wiki katika eneo la Sherui?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba Sherui na miji mingine wanahitaji huduma za benki kama nilivyoeleza tutafanya tathimini ikionekana kwamba kuna haja ya kuwa na tawi au kuwa na mobile benki basi tutafanya hivyo, namuomba avute subira ili tuweze kufanya tathimini na katika mji wa sherui.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Nashukuru kwa kuwa mji wa Kibakwe unafafana na mji wa Mwandoya wilayani Meatu, je, Serikali itakubaliana na ushauri wangu kuwa wakati tathimini ya haraka inafanyika katika mji mdogo wa Kibakwe itaenda sambamba na ule wa mji mdogo wa Mwandoya?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba kila mmoja anapenda katika eneo lake tufungue benki lakini shughuli za benki lazima ifahamike kwamba ni shughuli za kibiashara, hatutaweza kila mahali kufungua benki mpaka tufanye tathmini nawaomba Waheshimiwa Wabunge wavute subira tuweze kufanya tathimini katika maeneo mbalimbali ikidhihirika kwamba kuna haja ya kufanya hivyo basi tutafanya hivyo ikiwa na pamoja na ule mji ambao Mheshimiwa Mpina ameutaja.

Na. 98

**Vifaa vya Kisasa vya Kuvulia Samaki kwa Wavuvi Mtwara**

**MHE. MOHAMMED S. SINANI** Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imepata fedha nyingi kutoka katika vyombo vya fedha vya kimataifa na ikaanzisha mpango wa hifadhi ya mazingira ya bahari na viumbe wake *(MACEMP)* miaka miwili iliyopita:-

(a) Je, ni lini wavuvi waliopo kando ya bahari ya Hindi, hususan Mkoa wa Mtwara ambao hali zao za maisha ni duni watapatiwa vifaa vya kisasa vya kuvulia samaki kama nyavy, boti na kadhalika?

(b) Je, ni manufaa gani wamepata wananchi hao walio kandokando ya bahari hususani wa mkoa wa Mtwara tangu mradi huo uanzishwe miaka miwili iliyopita?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Said Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipata fedha za mkopo nafuu dola za kimarekani milioni 51 kutoka benki ya Dunia pamoja na dola za Kimarekani milioni 10 kama msaada kutoka Shirika la Mazingira la Kimataifa (*Global Environmental Facility – GEF*) ambazo zinatumiwa kutekeleza mradi wa usimamizi wa mazingira ya bahari na ukanda wa pwani ujulikanao kama *Marine and Coastal Environmental Management Project* ama kwa kifupi *MACEMP*. Gharama za mradi huu jumla ya dola za Kimarekani milioni 61 na mgawanyo wa fedha hizi ni asilimia 60 kwa Tanzania Bara na asilimia 40 kwa Zanzibar. Mradi huu umeanza kutekelezwa kuanzia mwezi Desemba, 2005 na utakamilika mwaka 2011. Shabaha kubwa ya mradi huu ni kuimarisha mfumo wa usimamizi wa rasilimali zilizoko baharini

na pwani, kuboresha maisha ya jamii zinazoishi ukanda wa pwani na kupunguza athari kwa mazingira.Baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika mwaka wa fedha 2008/2009, wavuvi waliopo katika Bahari ya Hindi katika Wilaya za Kilwa, Rufiji, Mafia Bagamoyo, Mkuranga, Temeke, Kinondoni, Ilala Lindi Vijijini, Mtwara Vijijini, Mkinga, Muheza, Pangani, na Jiji la Tanga watanufaika na utekelezaji wa mradi huu kupitia mfuko wa vijiji vya Pwani (*Coastal Village Fund*). Mradi utawapatia wavuvi mafunzo kuhusu uvuvi endelevu na fedha za kuendesha miradi watakayoibua kulinganana vipaumbele vyao. Chini ya utaratibu huu, mfuko umetenga kiasi cha dola za Kimarekani zipatazo 2,880,000 kwa ajili ya kugharamia miradi itakayoibuliwa na wanavijiji wenyewe.

(b) Kwa pande wa Mkoa wa Mtwara mradi umeanza kutelekelezwa katika hifadhi ya Ghuba ya Mnazi na maingilio ya mto Ruvuma (Mnazi Bay na Ruvuma *Estuary Marine Park*) ambayo ni Hifadhi ya Bahari na eneo Tengefu, kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa mazingira ya bahari na ya Pwani. Katika mwaka huu wa fedha, Hifadhi hiyo imetengewa dola za Kimarekani 267,000 kwa jili ya kuendesha doria, kutoa elimu kwa wananchi, kufanya usimamizi wa pamoja wa maliasili za uvuvi, pamoja na kuwapa wananchi zana mbadala bora na endelevu za uvuvi ili kupunguza uharibifu wa mazingira.Katika mwaka 2008/2009 wananchi wa Halmashauri ya Mtwara vijijini na Halmashauri nyingine nilizozitaja wataanza mchakato wa kuibua miradi katika maeneo yao na hivyo kujiunga na wenazao wa Wilaya za Rufiji, Kilwa na Mafia ambao tayari wameanza kutekeleza mradi huo.

**MHE. ABDULKARIM E. HASSAN SHAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mradi huu wa MACEMP ulianza utekelezaji wake toka mwaka Disemba mwaka 2005 mpaka sasa hivi inaelekea ni miaka miwili tayari Mafia, Kilwa na Rufiji wameanza kunufaika baadhi kwa mambo fulani fulani ya kuondoa maskini na utunzaji wa mazingira. Je, Serikali inaweza ikatutayarishia takwimu ya pesa ilizozitoa kwa wilaya ya Mafia, Rufiji na Kilwa katika kipindi cha miaka miwili iliyopita na ikatufahamisha ilitenga kiasi na zilizotumika kuwapata wananchi wenyewe wale wahusika ni kiasi gani na ili tuweze kufahamu matumizi mazuri ya pesa zilizokuwa katika mradi huu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka miwili ya mwanzo ya 2005/2007 kwa wilaya ya Kilwa, Mafia na Rufiji zimepatiwa fedha kupitia TASAF kwa ajili ya kugharamia miradi midogo midogo iliyoibuliwa na wananchi wa wilaya hizo kama ifuatavyo:-

Kilwa miradi 15 yenye thamani ya shilingi 130,828,635;
Mafia miradi 22 yenye thamani ya shilingi 331,105,125; na
Rufiji miradi 30 yenye thamani ya shilingi 328,885,425.

Miradi hii inahusika Miradi iliyotekelezwa ilihusu uvuvi endelevu ufugaji wa nyuki, unenepaji wa kaa, ufugaji wa samaki, ukusanyaji, ukaangaji na uuzaji wa samaki.

Vilevile Halmashauri hizo ambazo ni za Kilwa za Mafia na Rufiji, Kilwa ilipewa 198,880,400, Mafia shilingi 201,717,408, Rufiji shilingi 240,528,252.

**NAIBU SPIKA:** Waziri alishajiandaa hamna matatizo.

Na. 99

**Maonyesho ya Utalii – Berlin**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika maonyesha ya Utalii yaliyofanyika Berlin kuanzia tarehe 5 Machi, 2008 hadi tarehe 9 Machi, 2008 Tanzania ilijitangaza kwenye banda lake kama nchi kwa maana ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, lakini jambo la kushangaza ni kwamba, Tanzania Zanzibar ilikuwa na banda lake yenyewe la kujitangaza kama Tanzania Zanzibar ambalo lilifunguliwa rasmi tarehe 6 Machi, 2008 na Mheshimiwa Mama Shadia Karume; na kwa kuwa, utalii si jambo la Muungano, hatua ya kuwa na mabanda mawili iliwachanganya wateja kwa kufikiria kuwa Tanzania ni tofauti na Zanzibar.

Je, Serikali ina msimamo gani katika kutangaza utalii wetu nchi za nje ili kuzuia mkanganyiko kama huu uliotokea huko Berlin?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba suala la utalii sio suala la Muungano, hata hivyo kwa kutambua umuhimu wasekta hii kwa uchumi wan chi yetu, Wizara yangu imekuwa na ushirikiano wa karibu na Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu utangazaji na ukuzaji utalii Bara na Zanzibar.

Aidha, Wizara yangu kwa kupitia Bodi ya Utalii Tanzania imekuwa na ushirikiano wa karibu na Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuhusu utangazaji wa vivutio vya utalii vivyoko pande zote mbili za Muungano. Toka mwaka 1994, kutokana na ushirikiano huu, vivutio vyetu vilikuwa vinaendelea kutangazwa kwa pamoja kwa kutumia mikakati mbalimbali chini ya kaulimbiu moja ijulikanayo kama Tanzania Nchi ya Kilimanjaro na Zanzibar yaani (*Tanzania, The Land of Kilimanjaro and Zanzibar*)

Mkakati mwingine umekuwa ni ule wa kushiriki kwenye Banda moja la Tanzania kwenye maonesho ya utalii yanayofanyika nchini na nje ya nchi. Utaratibu huu unahusisha pia wadau binafsi wa Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ni kweli kulikuwa na mabanda mawili katika maonyesho ya utalii yaliyofanyikka Berlin Ujerumani hivi karibuni. Banda moja ilikuwa ni lile linalosimamishwa na Bodi ya Utalii Tanzania kila mwaka na ambalo washiriki wake wanatoka pande zote mbili za Muungano.

Katika maonyesho hayo pia ilikuwepo eneo maalum kwa ajili ya nchi visiwa kwenye bhari ya Hindi au nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Rim*). Hivyo baada ya nafasi ya pili kuwa ipo kwa Tanzania, ilionekana kuwa ni vizuri kwa Tanzania Zanzibar kutumia fursa hiyo kwa ajili ya kuongeza msukumo katika kutangaza vivutio vya utalii hasa vya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa masuala yote yanayofanyika nje ya mipaka yetu huchukua sura ya muungano. Wizara yangu kupitia bodi ya utalii Tanzania itaendelea kushirikiana na Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu kuendeleza na kutangaza utalii kwa pamoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ku-declare kwamba mimi nilikuwa katika yale maonyesho na kulikuwa na *confusion* kubwa sana pamoja na Tanzania kuwa ni member wa Indian Ocean. Kulikuwa hakuna sababu yoyote kwa Zanzibar kuwa na banda lake la tofauti.

Je, kwa sababu kuna huu mchanganyiko wa ku-confuse wageni wanapokuja kwenye banda letu la Tanzania. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kufanya suala la utalii kuwa la muungano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ajibu Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu, kuna mmoja aliniuliza kwamba Waziri Mkuu hayupo nani anakaimu, ndiyo huyu. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) – KAIMU WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Utalii napenda kumjibu swali lake la nyongeza Mama Owenya kama ifuatavyo:

Kwanza Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Muungano kuhusu *issue* hii tulishirikiana kwa karibu zaidi na Ofisi yangu ndiyo ilikuwa mratibu mkubwa wa shughuli hii tukijua kwamba kutakuwa na mabanda haya mawili kule Ujerumani. Kwa hiyo, Serikali ya Zanzibar haikuvunja Katiba kwa kuweka banda lake katika maonyesho hayo. Jambo la msingi ni kwamba kuelewa kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano ina vianzio vingi vya kupata mapato yake katika Serikali yake tokea dhahabu, samaki na kadhalika. Lakini kwa Serikali ya Zanzibar vyanzo vikubwa ni utalii peke yake. Kwa

hiyo, kama Serikali ya Zanzibar imepata nafasi ya kuwa autonomy yake lazima isaidiwe katika kuboresha fedha zake ili iweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania haina mpango wa kufanya Wizara hii ya Utalii kuwa Wizara ya Muungano.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jina la Tanzania ni suala la Muungano na tunapozungumzia jina la Tanzania nje ya nchi hakuna nchi inayojulikana kama Zanzibar. Ni kwa sababu gani kusiwe na banda moja lenye vyumba viwili vinayoonyesha Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kuliko mabanda mawili yanayotenganishwa kuonyesha nchi mbili tofauti?

**MHE. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ni kwamba katika maonyesho ya Berlin hakukuwa na mabanda mawili kama jinsi anavyoelezea, ni kwamba banda la Tanzania linalowakilisha lilikuwa moja na ndiyo sababu Mheshimiwa Mama Shadia Karume alikuwa mgeni rasmi na alifungua banda hilo kwa niaba ya Tanzania nzima, na pia itakumbukwa kwamba katika banda lile lingine kama tulivyosema ni kwamba ilikuwa tu kwamba tulipata nafasi ya kuweza pia kujitangaza zaidi na ni nafasi ambayo ni ya pekee kwa ajili ya visiwa vilivyoko Indian ocean na tuliona kwamba nafasi hiyo tusiipoteze pia.

Lakini hata hivyo napenda kuongezea kwamba hakuna *confusion* yoyote katika Wizara hizi mbili kwa sababu Wizara hizi mbili zote zimetungwa na Sheria mbalimbali kwa upande wa visiwani Sheria ya kuanzisha hiyo Wizara imetungwa na Baraza la Mapinduzi na Sheria ya Bara imetungwa na Bunge letu hili sisi wenyewe. Kwa hiyo, hakuna *confusion* katika hizi mbili.

Na. 100

**Ufugaji wa Wanyamapori - Siha**

**MHE. NURU A. BAFADHILI** aliuliza:-

Kwa kuwa wakazi wa Ngara Nairobi Wilayani Siha wanatakiwa wahamishwe kwa ajili ya ufugaji wa wanyamapori (wawekezaji):-

(a) Je, zoezi hilo litafanyika lini?

(b) Je, wananchi watafidiwa?

(c) Je, Serikali haioni kuwa kwa kuwahamisha wananchi ni kurudisha nyuma maendeleo yao kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja na kwa kifupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ngara – Nairobi ni kijiji kinachopakana na mashamba matano yaliyotaifishwa na kumilikishwa kwa Shirika la Taifa la Kilimo na Chakula *(NAFCO).* Mashama hayo yalikabidhiwa kwa iliyokuwa Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)* kwa ajili ya kuyabinafsishwa. Shamba la Matadi pekee ndilo lililopata mwekezaji.

Aidha, mwekezaji mmoja aliwasilisha mpango wa kuendeleza uhifadhi wa wanyamapori na utalii katika mashamba hayo. Hata hivyo ombi lake halikufikiriwa kwa kuwa halikuwa katika vigezo vilivyokuwa vimetolewa na *PSRC.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mchakato wa ubinafsishaji wa mashamba hayo bado unaendelea na mpaka sasa haujakamilika na wala matumizi ya mashamba hayo baada ya kubinafsishwa hayajajulikana, Wizara yangu kwa sasa haiwezi kusema zoezi hilo litafanyika lini kwani mwekezaji hajapatikana. Aidha, masuala ya fidia na maamuzi kuhusu hatma ya wananchi jirani na mashamba hayo yatafanyika muda utakapofika.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, hawa wananchi wanahamishwa ili kuboresha mandhari ya misitu inayozunguka Mlima Kilimanjaro na kwa kuwa Mlima Kilimanjaro unaingiza pesa nyingi kwa njia ya utalii na kwa kuwa mlima Kilimanjaro unazungukwa na Halmashauri tano ambazo ni Longido, Siha, Moshi Vijijini, Rombo na Hai.

Je, Serikali itaanza lini mkakati wa kutoa 25% ya mapato ya Mlima Kilimanjaro kwa Halmashauri zinazozunguka mlima huo kama inavyotoa kwa Halmashauri zinazozunguka Game Reserves?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aloyce Kimaro kama ifuatavyo:

Ni kweli kwamba kuna baadhi ya Halmashauri zinazozunguka sehemu zetu za utalii na sehemu mbalimbali za wanyama pori wanapata percent kama hiyo na pia napenda kumwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hilo tutaliangalia na pia tutaona

uwezekano uliopo na tutakaa nao wenyewe ili tuweze kuzungumza masuala haya. (*Makofi*)

Na. 101

**Matukio ya Ujangili kwa Maeneo Yanayopakana na Nchi Jirani Zenye Vita**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa matukio ya ujangili yameshamiri kwenye maeneo yanayopakana na nchi jirani zenye vita vya wenyewe kwa wenyewe na kwa kuwa askari wetu wa maeneo hayo wanafanya kazi katika wakati mgumu kutokana na wimbi la uingizaji wa silaha za kivita kama SMG, AK 47 na kadhalika hususan kwenye Wilaya ya Mpanda ambako mbali ya kuwa na mapori makubwa pia huwahifadhi wakimbizi kutoka Burundi ambao baadhi yao ni majangiri kama ambavyo wamewahi kukamatwa na silaha husika na kufunguliwa kesi na kwa kuwa askari wanyamapori wa Halmashauri hiyo hutumia silaha duni na za zamani zisizohimili zile walizonazo majangili na pia Halmashauri hiyo haina gari kwa ajili ya doria:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia Halmashauri hiyo gari pamoja na silaha za kisasa ili kukabiliana na changamoto zilizopo na kuimarisha uhifadhi kwenye maeneo hayo ambayo ni muhimu katika uchumi wa nchi yetu?

(b) Kama mpango huo upo. Je, ni lin utakuwa tayari kwani kuendelea kuchelewa ni sawa na kuruhusu uharibifu huo uendelee?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Lupembe, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa matukio ya ujangili yameshamiri katika mapori yaliyo kwenye ukanda wa Magharibi kuaizna Mpanda, Ngara na Karagwe. Pia ni kweli kuwa Askari wetu katika ukanda huo wanafanya kazi katika wkati mgumu kutokana na wimbi la uingizaji wa silaha za kivita katika maeneo hayo na wakimbizi toka nchi jirani.

Kwa kutambua hali hiyo, Wizara yangu imekuwa ikielekeza vitendea kazi hususani magari ya doria na silaha katika ukanda huo katika Kikosi Dhidi ya Ujangili (KDU) Kanda ya Magharibi – Tabora, Pori la Akiba Rukwa/Lukwati, Hifadhi ya Taifa Katavi, Pori la Akiba Moyowosi/Kigosi, Burigi/Biharamuro, Kimisi na Ibanda/Rumanyika.

Kwa mfano, mwaka 2007, Wizara yangu ilinunua silaha za kisasa 500 na tayari zimekwisha gawiwa katika vituo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kikosi Dhidi ya Ujangili Tabora, Pori la Akiba Rukwa/Lukwati na Hifadhi ya Taifa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Wizara yangu imepeleka jumla ya magari matano (5) katika kituo cha Kikosi Dhidi ya Ujangili Tabora, magari manne (4) katika Pori la Akiba Rukwa /Lukwati na magari matano (5) katika Pori la Akiba Ugalla. Aidha, juhudi za Wizara katika kutoa vitendea kazi zimeelekezwa katika ngazi ya Kanda na baadaye ngazi ya Wilaya, Kata hadi Vijiji kadri uwezo utakavyoruhusu. Sambamba na hatua ya Wizara yangu, Serikail kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikifanya operesheni za kusaka wahalifu wahamiaji haramu pamoja na silaha harama katika ukanda huo.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imekuwa ikiimarisha doria pamoja na vitendea kazi kwa askari wanyamapori, na itaendelea kufanya hivyo. Pia itaendelea kuongeza na kuboresha vitendea kazi ikiwemo magari na silaha kadri bajeti itakavyoruhusu.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Vilevile naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa kujibu swali langu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali halisi ya Wilaya ya Mpanda jiografia ikiwa mbaya vilevile pale Wilayani Ofisi ya Utalii hakuna gari hata moja ambalo linaweza kusaidia kusaka majangili na ukitegemea Wilaya ya Mpanda kuna majangili wengi na mapori mengi. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuleta silaha katika Wilaya ya Mpanda na lini Serikali italeta gari kwa ajili ya doria katika Wilaya ya Mpanda.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anna Lupembe kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, tungependa sana kuhakikisha kwamba kila sehemu yenye matatizo kuwe na silaha za kutosha lakini kwa sababu ya ufinyu wa bajeti ndiyo sababu inabidi tuende hatua kwa hatua.

Hata hivyo napenda kumueleza Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa upande wa mkoa wa Rukwa hadi sasa silaha tulizotoa ni nyingi na kwa hali hiyo na ni silaha ambazo ni nzito na ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu mambo ya silaha ni mambo ya siri nisingependa kuyatoa hadharani lakini namuomba aje nimuelekeze ajue ni silaha gani na ziko wapi. Lakini silaha ni nyingi za kutosha kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ila pia naomba niongee kitu kimoja ya kwamba katika bajeti yetu ya safari hii tunawaomba Waheshimiwa Wabunge mtusaidie ili tuhakikishe kwamba tupate hela ya kutosha ili kuongeza vifaa kama hivyo kwani wote tunafahamu

kwamba jambo la ujangili na wenzetu waliopo huko hiyo ni kama vita na kama ni vita hapo inatishia maisha ya wananchi. Tunaomba mtusaidie katika bajeti ili tuweze kuongeza vifaa na silaha. (*Makofi*)

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. nina swali moja la nyongeza. Kwa sababu kikosi cha kuzuia ujingili kilichopo Tabora Kanda ya Magharibi kina eneo kubwa la kufanya kazi.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuanzisha kikosi kingine ambacho kitaangalia maeneo ya Magharibi kabisa mwa nchi yetu kwa maana ya mapori yaliyopo Magharibi mwa Wilaya ya Mpanda kuelekea Kigoma na kuongeza idadi ya Askari ambao hawatoshelezi?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Arfi, kama ifuatavyo:-

Katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu vizuri sana na ameeleza wazi Kanda ya Magharibu ni sehemu gani mpaka sasa hivi tumegawa na tumepeleka silaha na ninapenda kusema kwamba kwa kufuatana na ufinyu wa bajeti narudia tena ndiyo sababu tunashindwa kuongeza vikosi. Kwa hali hiyo, napenda nimuahidi kwamba pindi jinsi tutakavyopata pesa ndivyo tutakavyoongeza.

Kwa hivi sasa, sehemu ambazo tulizonazo na zina silaha mbalimbali na vifaa mbalimbali ni kwa upande wa Magharibi nzima tukiondoa Tabora kuna Moyoyosi, *Kigoma Game Reserve* kuna kikosi na silaha, Burigi kule ambako kuna matatizo makubwa ya wakimbizi mpaka Biharamulo na Kimisi pia huko tunazo, Rukwa mpaka Lukwati pia huko tumeweka. Tukija Rungwa, Kigosi kote huko tumeweka na pia na nyingine ni kwenye Kanda ya Tabora hadi kuna Manyoni kuja Iringa kote huko tumeweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii kinachotushinda ni ufinyu wa bajeti lakini hata hivyo tunaahidi tutazidi kuongeza.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza nimpongeze kwa mipango mizuri wanayoifanya kuweza kulinda wanyama ambao wanaleta manufaa. Lakini Geita tuna misitu ambayo iko chini ya Maliasili ambayo inatuletea matatizo. Majangili ya wanyama hawapo lakini kuna majambazi yanayoshambulia watu kwa kutumia au kwa kijificha ndani ya misitu hiyo. Na Wizara husika inayoangalia Askari Polisi uwezo inaonekana imezidiwa. Je, Wizara yako inaweza kuisaidia Wizara ya Mambo ya Ndani ili kuweza kuwapa vifaa kwa ajili ya kutusaidia kupambana na wale majambazi wanaojificha kwenye misitu hiyo kwa sababu inatuweka katika hali mbaya?

**NAIBU WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rwilomba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Tatizo la ujambazi ni kweli lipo kwenye huo ukanda nafikiri na nilikuwa namuomba Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Wizara tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya ndani lakini ningependa kuwaomba Makamanda wa Polisi wa Mikoa hasa Mkoa wa Mwanza waige mfano wa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kagera yaani Kamanda Tosi, tumekuwa tukijua shughuli nyingine ambazo amekuwa akizifanya na tatizo limeshuka. Kwa hiyo naomba Polisi wafanye operesheni maalum kwenye maeneo hayo na imewezekana kama ilivyowezekana Kagera sisi kama Wizara ya Maliasili na Utaliii tutatoa ushirikiano pale ambalo inahitajika kushirikiana.

Lakini ushauri na wito ni Kamanda wa Polisi na vikosi vya Polisi kwenye eneo hilo kufanya operesheni kwenye hayo maeneo ambayo ni maficho ya majambazi.

**MHE. JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niulize swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja. Kwa kuwa matatizo ya ujangili yaliyopo Mikoa ya Tabora, Mpanda na Rukwa ni sawa na Kigoma. Je, Serikali ipo tayari kushawishi makampuni kuweka mitambo ya mawasiliano au *Radio Call* ili Askari waweze kuwasiliana wanapokuwa na matatizo?

**MHE. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niamba ya Mheshimiwa wa Maliasili na Utalii ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Genzabuke kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninapenda kusema kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani iko imara na tunayo nguvu ya kulinda maeneo yetu mengi hapa ndani ya nchi. *Radio Call* tunazo na zinafanya kazi na mara kwa mara tunafanya operesheni katika mengi ya nchi hii ambapo ujangili unapatikana. Ninapenda sana kuwapongeza Makamanda wa *Force* ya Polisi wakiwemo Makamanda kama Kamanda Tosi ambaye ametajwa lakini wapo wengi wengine ambao wanao uwezo wa kufanya kazi. Ninapenda kuwahakikishia Watanzania kwamba pale ambapo pana matatizo tutaingia katika operational maalum kuhakikisha kwamba hawa majambazi tunawasaka.

**MHE. PROF. RAPHAEL BENEDICT MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naomba niulize swali fupi la nyongeza.

Kwa vile Mheshimiwa Waziri kazungumzia kwamba katika utendaji kazi na kutoa vitendea kazi wanatilia mkazo kwanza kwenye maeneo ya Kanda je, Waziri anatambua kwamba huo ni utaratibu wa kujenga himaya na kurundika vifaa kama magari kwenye zone na kuacha maeneo yaliyo kwenye vituo wanakochapa kazi bila vitendea kazi kwa kweli ukienda kule unawaonea huruma hawana vitendea kazi lakini magari yako kwenye kanda yamerundikwa hayafanyi kazi. Je huu ni utaratibu wa kufanya kazi?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII :** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba nakubaliana naye kama ikiwa ni vifaa vinagaiwa na wahusika katika sehemu hiyo wanavirundika badala ya kuvigawa vifanye kazi. Madhumuni ya sisi kuweka kwenye Kanda ni kama kituo ambacho ndiyo kitatumiwa katika kusambaza huduma katika sehemu mbalimbali. Napenda kutoa wito na kwa zaidi kwa upande wa Maliasili kwa kufuatana na silaha na magari mbalimbali ambayo tumeyagawa ni kwamba magari hayo yatumike ipasavyo kupelekwa kwenye sehemu ambazo yatakuwa yanafanya kazi na siyo binafsi mtu aweze kuyaweka yeye awe ndio mmoja anatawala hayo magari.

Na. 102

**Mawasiliano ya Simu za Mkononi**

**MHE. BUJIKU P. SAKILA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imefanya vizuri kuruhusu kampuni nyingi sana za simu za mkononi kuwekeza hapa nchini na kurahisisha mawasiliano ndani na nje ya nchi, na kwa kuwa teknolojia hiyo haijatimiza hata miaka ishirini (20) kuweza kuwafikia watu wengi hapa nchini:-

(a) Je, ni mionzi mawimbi ya aina gani yanayopokelewa na simu hizo kutoka kwenye minara ya mitandao ya simu hizo zinapotumika?

(b) Ili kujua kama mionzi /mawimbi hayo yana madhara ya muda mfupi, kati na mrefu suala kwa watumiaji. Je, utafiti huo ulifanywa wapi? Lini na kwa watu gani?

(c) Katika mikataba ya Serikal na kampuni hizo. Je, vimo vipengele vinavyovitaka kampuni hizo kulazimika kulipa fidia kwa watakaothibitika kuathirika kutokana na matumizi ya teknolojia hizo; hasa kwa kuzingatia ukweli kuwa hakuna mipango ya mafunzo inayopangwa na Serikali au kampuni hizo kwa watumiaji,na wale walioko karibu na minara ya mitandao ya teknolojia ya simu hizo kabla ya wakati wa matumizi yake?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mbunge wa Kwimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali imewapa nafasi kampuni nyingi za simu za mkononi kuwekeza hapa nchini kwetu. Hili si

jambo baya hasa ukizingatia kuwa sera zilizopo  zinaainisha umuhimu wa mawasiliano kwa wananchi kwa ajili ya maendeleo yao.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano ya simu za mkononi hutumia mawimbi ya radio ambayo huanzia masafa ya *30MHz – 300GHz.* Lakini  ndani ya masafa haya kuna teknolojia za aina mbalimbali  zinazotumika kwa ajili ya matumizi ya simu za mkononi ambapo kila teknolojia hutumia mawimbi tofauti. Teknolojia inayotumika sehemu nyingi ulimwenguni ni ile inayofahamika kama GSMm, hii hutumia  mawimbi ya 900 na 1800MHz, lakini pia kuna teknolojia inayofahamika kwa jina la SDMA ambayo hutumia mawimbi ya 450-470MHz na 824-894MHz. Mawimbi yote haya yaliyotajwa hapo awali yametengwa na Umoja wa Mawasiliano ya kimatifa (ITU) ili yaweze kufanikisha mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kama nchi nyingine zinazoendelea hutegemea viwango na miongozo ya udhibiti  wa mionzi inayotolewa na Tume ya Kimatifa ya Udhibiti wa Mionzi ijulikanayo kama *International  Commission on Non –Ionizing Pprotection (ICNIRP)* . Tume hii ilianzishwa na Umoja wa Mawasiliano ya Kimataifa (ITU) ili kutafiti juu ya madhara yatokanayo na mionzi inayotokana na vifaa vya radio hususani simu za mkononi.

Kulingana na tafiti za Tume (ICNIRP), ilibaini kwamba tofauti  na mionzi mengine kama vile *X-rays na Gama Rayas* ambayo naweza kuharibu chembechembe za mwili (Body Cells) na kupelekea madhara kama saratani na  kadhalika. Athari zinazoweza kusababishwa na mionzi /masafa ya radio ni ongezeko la joto mwilini pale mtu au mnyama anapokaribia chombo kinachorusha masafa – (*antenna*).

Kwa vile nguvu iliyomo katika masafa/mionzi inayosarishwa hupungua kwa kiwango kikibwa sana kutoka antenna (mara elfu moja katika umbali wa mita moja kutoka antenna), na kwa vile antenna hufungwa mita kadhaa juu ya minara, nguvu ya mionzi hiyo huwa ni ndogo sana ifikapo chini ya minara.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika utafiti huu umekuwa ukifanyika tangu mwaka 1988 ambapo mwaka 1988 Tume (ICNIRP) ilitoa miongozi ya udhibiti  wa mionzi hiyo. Hata hivyo, Mamlaka na watoaji wa huduma za simu za mkononi huchukua hatua za kutosha za kiusalama  na hivyo kupunguza  joto. Hii ni kwa kuhakikisha kila mnara unapowekwa antenna zinawekwa juu kiasi kwamba haziwezi kufikiwa na mwananchi.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo katika mikataba ya Serikali na makampuni ya simu kwa maana ya leseni za utoaji huduma hizo za Mawasiliano, kuna vipengele vinavyosisitiza uzingatiaji wa usalama kati ya watumiaji na watoa huduma. Hivyo, endapo kutathibitika kutokea athari yoyot e  kwa mtumiaji kampuni husika itapaswa kuwajibika kikamilifu.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA**: Mheshimwia Naibu Spika ahsante sana. kwanza nampongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Lakini nina maswali ya nyongeza mawili.

Kwanza, aulizaye anataka kujua, lisemwalo lipo na kama halipo laja lakini vilevile Serikali ina wajibu wa kulinda usalama wa raia wake. Je, Serikali itakuwa tayari kufanya utafiti wake yenyewe ili kujiridhisha kwamba kweli maelezo hayo ni ya kweli?

Pili, kama Serikali haitakuwa tayari kufanya utafiti huo itakuwa tayari kubeba mzigo wa kutoa fidia kwa wale watakaoathirika itakapothibitika kwamba kuna athari zake?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mbunge wa Kwimba, kama ifuatavyo:

Nakubaliana naye kwamba anayeuliza anataka kujua na lisemwalo lipo na kama halipo laja. Sasa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia kwa kupitia Tume yake ya Udhibiti wa Mawasiliano inashirikiana na Tume ya Mionzi ambayo iko Arusha kufanya masuala ya utafiti na kama nilivyosema kuna sheria, Kanuni na taratibu ambazo zimewekwa kwa wale wote wanaoingia vifaa hivi kwamba viwe ni vifaa approved na salama kwa matumizi ya watu.

Lakini nataka nitoe wito vilevile kwamba wanaojenga minara wahakikishe minara inayojengwa iwe ni mirefu na inawekwa juu ili kila ikienda juu zaidi na ile mionzi inapungua.

Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba anayehusika na kuleta athari kwa wananchi ndiye atakayewajibika kulipa fidia. (*Makofi*)

Kwamba viwe ni vifaa *approved* na salama kwa matumizi ya watu, lakini nataka nitoe wito vilevile kwamba wanaojenga minara wahakikishe minara inayojengwa iwe ni mirefu na inawekwa juu ili kila ikienda juu zaidi na ile mionzi inapungua, lakini napenda nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge anayehusika na kuleta athari kwa wananchi ndiye atakayewajibika kulipa fidia.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri aina ya mawimbi *electrical magnetic waves or sound waves*. Je, ina *effects* gani katika *nerve* namba saba yaani *facial nerve*? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi siwezi kubishana kwenye masuala ya *electrical magnetic* au nini, kuna *ionizing* and *non-ionizing.* Sasa ziinazoharibu ni *ionizing, non-ionizing* hazina madhara. Mheshimiwa namjua kwamba yeye yupo katika fani ya *radiation* kwenye mambo ya *X-ray*, ile *X-ray* inaleta athari, lakini tumepewa *prevention* tukizitumia simu lazima uweke kile kidude cha kwenye kisikio ili usipate madhara kwenye hizo *nerves* anazoziongelea Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

**MHE. ELIATA N. SWITI:** Ahsante. Kwa kuwa wakati mwingine minara hiyo hupoteza mwelekeo wa kusambaza hiyo mionzi na kuelekea kwa wananchi. Je, Serikali inaandaa nini ili mionzi hiyo isiwe wakati mwingine inapoteza mwelekeo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Nimkumbushe Mheshimiwa Switi kwamba vibali vya ujenzi wa minara katika maeneo mbalimbali vinatolewa na Halmashauri zetu na husimamiwa vizuri na wenyewe wanaojenga. Kama kutakuwa na mwelekeo mzuri ambao mimi sijui ni mwelekeo gani labda kama ni kupinda au ni vipi, basi ni vizuri tu tujulishane ili wanaohusika (*regulators*) waweze kufanya kazi yao ipasavyo.

**MHE. JANETH B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa minara hii mingi sana siku hizi inazidi kujengwa katika maeneo ya makazi ya watu, ndani ya makazi ya watu au karibu na makazi ya watu likiwemo Jiji hili la Dodoma, kwani kwanza sura ya Jiji haipendezi lakini pia hiyo minara ipo karibu na wananchi, hata ukiwa mrefu kiasi gani bado watu watadhurika hapa chini. Je, Serikali imetunga sheria zipi za kukataza ujenzi wa minara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba kuna baadhi ya maeneo minara imekuwa mingi ndani ya miji yetu, lakini nataka nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari tumewaambia Tume ya Mawasiliano wafanye marekebisho ya kanuni zao ili kuwepo na uwezekano wa ku-*share* minara katika baadhi ya kampuni na baadhi ya kampuni hivi sasa wana *share* minara ili kutunza *environment*. Naomba pia nitoe wito kwa Halmashauri zote, ambazo wao ndiyo wanaotoa vibali kwa ajili ya ujenzi wa minara hii, waweke maslahi ya wananchi kwanza na si maslahi ya mtu binafsi ambaye analipwa kama dola mia tatu kwa mwezi kwa ajili ya kuweka mnara katika nyumba yake. (*Makofi*)

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa kuna wafanyabiashara ambao wameshamiri kuuza vyombo vidogo au *devices* ambazo wao wanasema kwamba ukizibandika kwenye simu basi simu hiyo haiwezi kukusababishia matatizo hasa saratani na kutobandika *devices* hizo kunaweza kusababisha saratani baada ya matumizi ya muda mrefu wa hizi simu za mkononi.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anawaeleza nini wananchi, kila mmoja anunue na kuvibandika hivi ili kujikinga na hilo ambalo linaweza kutokeza au ni biashara tu watu wanajitafutia riziki?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikiri kwamba hizo *devices* mimi sijaziona labda nichukue kutoka kwako ili nifanyie kazi ili na Bunge liweze kujua na kama zitakuwa na faida kwa wananchi sioni sababu kwa nini wananchi wasiweze kununua kuji-*protect*.

Ninachoweza kusema ni kwamba, kwanza tusipende kutumia simu ya mkononi kwa muda mrefu. Pili, tusipende kukandamiza karibu na sikio na tatu tutumie *aid* ile ya sikio ambayo inafanya simu iwe mbali na wewe. Ni vizuri basi *protections* kama hizo tukazifanya ili kuwa salama wakati wote.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu. Swali langu kwa Waziri ningependa kujua kama taarifa kwamba hii teknolojia ya milingoti mirefu na minara imeshapitwa na wakati. Sasa hivi inatumika *fibre optics* katika nchi zingine za Ulaya, yaani hii imeshapitwa na wakati. Je, ana taarifa hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Na kama ana taarifa afanyeje sasa? Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, najua yapo matumizi ya *fibre optics* kwa ajili ya mawasiliano lakini kwamba imekuwa *condemned* hii, mimi nahudhuria mikutano yote ya *ITU* haijasema hata siku moja kwamba, teknolojia hii iko *condemned* na inayotakiwa ni ya *fibre*. *Fibre* inatumika na hii inatumika na sisi tunasoma *research* kila siku, leo asubuhi nilikuwa katika internet sijaona kitu kama hicho.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa swali mama linaulizia simu za mkononi na kwa kuwa siku hizi kumezuka mtindo unapompigia simu mtu yeyote yule, namba ambayo umesevu katika simu yako, unajibiwa kwamba umekosea, hakikisha nambari uliyopiga. La pili, wakati mwingine.....(*Kicheko*)

Bado sijauliza. Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine unaambiwa mtumiaji wa simu hii kwa sasa hapatikani wakati simu ipo wazi. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba tatizo hili litasababisha talaka zitoke nyingi? (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haroub pamoja na kwamba nimekupa nafasi lakini swali lilikuwa la mionzi siyo la msemo. Mheshimiwa Kumchaya.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja tu la nyongeza. Katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri amesisitiza kujenga minara mirefu zaidi ili iweze kupunguza nguvu ya mionzi. Pale Lupaso kuna mnara mfupi sana wa *Celtel.*

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuwaeleza wanaohusika ili waweze kufanya marekebisho ili mnara ule usiendelee kuleta madhara?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba pale Lupaso kuna mnara ambao kidogo ni mfupi ukilinganisha na mingine, lakini kama nilivyosema katika jibu la msingi

jamani, minara hii mara nyingi inawekwa sehemu za juu na mahali penye mwinuko na kama ipo chini inakuwa ni mirefu zaidi.

Sasa labda niwaombe *Celtel* wakaangalie hali halisi ilivyo pale Lupaso, lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tahadhari zote zinazohusika zinachukuliwa na Tume ya Mawasiliano inafuatilia kwa karibu sana juu ya *research* mbalimbali zinazofanywa kama kutakuwa na athari yoyote haitasita kuchukua hatua zinazofaa.

Na. 103

**Shirika la Posta Kuongezewa Fedha**

**MHE. GRACE S. KIWELU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italiongezea fedha Shirika la Posta ili liweze kufanya kazi kwa ufanisi na kukidhi mahitaji ya wateja wake?.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Bunge namba 19 ya mwaka 1993 ambayo inaliunda Shirika la Posta Tanzania imeelekeza kwamba Shirika la Posta linatakiwa lijiendeshe kibiashara na maendeleo. Aidha, Sheria hiyo pia imeelekeza ni namna gani Shirika litapata mtaji wa kuendeshea shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba Shirika la Posta linakuwa katika mazingira mazuri ya kuliwezesha kupata mtaji kwa njia ya mkopo kutoka taasisi za fedha, Serikali imechukua madeni yote ya Shirika hilo na kusafisha mizania ili liweze kukopesheka. Aidha, Serikali imeshaanza kufanya tathmini ya mahitaji ya mtaji kwa ajili ya maendeleo muhimu ya kibiashara na maendeleo kwenye shirika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hili ambalo linatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2008/2009, litaweza kubainisha vyanzo mbalimbali vya mtaji kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya muda mrefu na muda mfupi kama ilivyobainishwa kwenye mpango mahsusi wa kibiashara na maendeleo ya Shirika la Posta.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa imekuwa ni kero na usumbufu hasa kwa wateja wa shirika hilo ambao Ofisi zao zipo katika Manispaa ya Moshi Mjini hasa wale wanaotumiwa fedha wanapokwenda kuchukua fedha zao hukuta fedha hizo zimetumka aidha kulipa wateja wengine au kwa kazi zingine. Je, huo ndiyo utaratibu na kama siyo utaratibu Waziri anatwambia nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna utaratibu wa kutumia fedha za mteja, *money fax* ukituma ni lazima upate pesa zako, kama kutakuwa na hitilafu yoyote Mheshimiwa Kiwelu naomba tuwasiliane ili tuweze kuondoa dosari hizo. (*Makofi*)

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kutokana na kubadilika sana kwa teknolojia ya mawasiliano ambayo inafanya baadhi ya kazi zilizokuwa zinafanywa na Shirika la Posta zisiwe na maana sasa hivi, je, ni ubunifu gani unaofanywa na Wizara na Shirika hili kuhakikisha kwamba linajiendesha kibiashara na kwa faida? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli teknolojia ya Posta sasa inahitaji mabadiliko makubwa sana kwa sababu teknolojia tuliyo nayo sasa hivi ya *internet* inachukua nafasi kubwa sana kwa kazi ambazo Posta inafanya. Tayari tumeshawapa changamoto wenzetu ya kuona wanaweza kufanya nini ili kuendana na wakati huu.

Zamani watu walikuwa wanatuma vifurushi na barua kwa kutumia Posta, sasa hata kadi za mwaliko zinatumwa kwa kutumia *internet*. Kwa maana hiyo, wanachofanya sasa watu wa Posta ni kuhakikisha kwamba wanakuwa na mitandao ya mawasiliano nchi nzima kwa kutumia *computer*, zile huduma ambazo zinaweza kutolewa za *ICT* kama huduma za *Internet Café* sasa zipatikane katika sehemu zote za Posta, tunaanza na Mkoa, tutakuja Wilaya, halafu tutakuja na sehemu nyingine zilizobakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza mapato wanataka kufanya utafiti wa soko ili kujua mahitaji, lazima kama mfanyabiashara ujue mteja wako anataka nini, mionjo gani iliyoko hivi sasa, huwezi kumwambia mtu sasa hivi anataka kunywa soda wakati kuna baridi, hatotaka soda na haitauzika.

Kwa hiyo, na wao wamo katika shughuli hizi za kujiendesha kibiashara, lakini pia kuwa mawakala wa taasisi na mashirika mbalimbali kwa mfano, kama kunatakiwa kulipiwa *bill* za umeme au za maji, wao wawe mawakala wa kuzipeleka, halafu wao wanapata chochote. Hizi ni mbinu za kibiashara ambazo ziko nyingi, lakini zinahitaji fedha na fedha hizo tutazipitisha katika Bunge hili. Kwa hiyo, nitawaomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono katika hili ili Posta nayo sasa iweze kusimama kwa miguu yake. (*Makofi*)

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa Mji wa Iringa umepanuka na kuwa na wakazi wengi na wananchi wengi wanategemea Posta Kuu iliyopo katikati ya Manispaa kwa ajili ya huduma za Posta na matawi madogo madogo. Je, Serikali itakuwa tayari kujenga tawi la Posta eneo la Ipogoro ili kufanya wananchi wapate huduma kule chini badala ya kupanda mlima ili kuweza kupata huduma za Posta?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi tulifikiria na wenyewe katika *business plan* yao watu wa Posta wana nia ya kujenga Posta za kisasa arobaini na saba, hizi zitagharimu kama Sh. 5bn/=. Sasa kama tutapata fedha hizo tunaweza kufanya shughuli hiyo. Lakini tulichokifanya kikubwa hivi sasa kwa Serikali ni nini? Ni kuchukua madeni yao mengi tu waliyonayo, kuweka mizania ya mahesabu yao vizuri ili waweze kukopesheka, hiyo ndiyo kazi ambayo Serikali inafanya, hata madeni ya wale wastaafu wa *East African Post Communication*, Serikali italipa deni lile la Sh. 8.2bn/=. Hayo yote ni juhudi za Serikali kuona Posta inaweza kusimama yenyewe na ikiweza kusimama yenyewe ikaweza kupata hati safi wanaweza kupata nafasi ya kukopesheka kwenye mabenki mbalimbali na kufanya biashara, lakini zaidi ni vizuri tuka-*restructure*, tukawa na *management* nzuri, maana yake unaweza kuwapa watu fedha lakini bila kuwa na *management* nzuri wasiweze kutoa huduma inayopasa. Mashirika yote yanayo-*survive* ni yale ambayo yanajali *management* na yanajali wateja wake. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge sasa nakubaliana na ule usemi kwamba, mzigo mzito mpe Mnyamwezi. Kwa hiyo, Mnyamwezi wetu leo ni Naibu Waziri Mheshimiwa Maua Daftari, tunakushukuru sana. (*Makofi*)

Kwa sababu Naibu Spika alizidiwa hapa, idadi ya maswali yaliyowekwa leo yalikuwa yanafikiria Waziri Mkuu atakuwa na kiti moto. Kwa hiyo, yalikuwa machache, kwa hiyo tumemwuliza Mnyamwezi huyu maswali kumi na tano. Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa uhodari wako na umahiri wako wa kujua sekta za kazi unazofanyia tunakutakia kheri nyingi sana.

Waheshimiwa Wabunge naona mnastuka kwamba leo ipo *gender* tu humu ndani ya Bunge, tunajaribu kufanya mazoezi tutakapokuwa *fifty fifty* inakuwaje. Kwa hiyo, hayo msiyashangae ni ya kawaida baadaye. Kuhusu wageni wetu leo. Kwanza kabisa tuna wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Mabalozi kutoka Jumuiya ya Ulaya. Yupo Balozi Kiongozi wa *Delegation* hiyo, *can you please rise up your hand*. Tuna Balozi Carley Van Casten, Balozi wa Netherland; halafu tuna Balozi Stafen Heristom, Balozi wa Sweden; tuna Mr. Josephine Kitama, yeye ni Afisa kutoka Ubalozi wa Netherlands aliyeongozana nao. (*Kicheko/Makofi*)

*Your excellences we invite you to our Parliament and I understand that in this afternoon we shall have some discussions with the Deputy Speaker, welcome to our House*. Pia tuna wageni wengine, tuna wageni wa Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Ndugu Mshamu Mussa Nayopa, Katibu wa Siasa na Uenezi, Mtwara. Kuna wageni wa Mheshimiwa Janeth Kahama, yuko Mama Getrude Luangisa, mke wa muasisi wa CCM Kagera na alikuwa Mbunge humu ndani, yeye amefuatana na binti zake. Tuna mgeni wa Mheshimiwa Mohammed Missanga, Ndugu Samuel Joseph Mushi kutoka *Vodacom,* nafikiri alikuwa anaelewa haya tuliyokuwa tunazungumza hapa. Tuna wanafunzi wetu thelathini na tano kutoka Chuo Kikuu cha Tumaini Iringa, ni wageni wa Wabunge wa Mkoa wa Iringa, wote wasimame. Vilevile, tunao wanafunzi sabini kutoka Chuo Kikuu

cha Mtakatifu John Dodoma.  Naona leo hawajaja lakini walikuja jana.  Kuna wanafunzi arobaini kutoka shule za msingi Mnadani Dodoma, naomba wasimame na walimu wao. Pia wageni wengine wote mliopo Bungeni mnakaribishwa, hili ni Bunge lenu na tunafurahi kwamba wageni mnakuja kuona mambo yanavyoendeshwa ndani ya Bunge lenu, kwa hiyo wote mnakaribishwa.  (*Makofi*)

Kuhusu shughuli za kazi.  Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Hassan Khatib anawaomba wajumbe wa Kamati yake leo tarehe 17, saa tano asubuhi hii, wakutane katika chumba Na. 231. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa William Shellukindo, anawaomba wajumbe wa Kamati yake wakutane leo hii saa tano katika chumba Na. 227.  Anasema kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika saa tano asubuhi katika ukumbi Na. 227, ghorofa ya pili na kikao cha wajumbe wote kitafanyika saa saba mchana katika ukumbi huo huo.  Sijui kuna aina mbili za Wabunge hapa, nadhani wao wanaelewa.Mheshimiwa Raphael Chegeni, Mwenyekiti wa *CPA*, Kanda ya Tanzania anawatangazia wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji ya *CPA* kuwa kutakuwa na kikao leo saa tano asubuhi kwenye ukumbi Na. 432, ghorofa ya nne, mnaombwa kuhudhuria.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge leo nilitaka kusema tathmini ya ujibuji wa maswali, ukiacha yale ya mwisho.  Lakini Waheshimiwa Mawaziri na wauliza maswali swali lililozidi sana ni dakika tisa, swali namba 95 ni dakika nane, 96 dakika tano, 97 dakika tano, 98 dakika tisa  na 100 dakika nne.  Baada ya hapo niliacha kufanya tathmini kwa sababu tumemgandamiza  mtu mmoja.  Kwa hiyo, naomba niwapongeze Wabunge wote na Mawaziri kwa kujibu vizuri maswali na kuuliza vizuri.  Sasa tunaendelea,  Katibu endelea  na *Order  Paper.* (*Makofi*)

## MISWADA  YA  SERIKALI

### Muswada wa Sheria wa Kurekebisha Sheria Mbalimbali za  Ukusanyaji wa Mapato ya Mwaka 2008 (*The Financial Laws Miscellaneous (Amendments) Bill,* 2008)

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mtoa hoja tutatoa *Supplementary Order Paper* baadaye kwa sababu kuna maazimio mengi yamekamilika. Kwa hiyo,  sasa namwita mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge Muswada wa Sheria ujulikanao kama *The Financial Laws Miscellaneous (Amendment) Act*, 2008 wenye lengo la kufanyia marekebisho sheria mbalimbali za fedha na kodi ili kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya kodi za majengo kwa niaba ya Serikali za Mitaa.Awali ya yote, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni kwa kujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako kwamba Serikali imezingatia kwa dhati michango ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ambayo imesaidia sana katika kuboresha Muswada huu. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipotembelea Mamlaka ya Mapato Tanzania tarehe 30 Januari, 2006, aliiagiza Mamlaka pamoja na mambo mengine kuzisaidia Halmashauri za Serikali za Mitaa ili nazo ziweze kuboresha makusanyo ya mapato yake.

**NAIBU SPIKA:** Wanaotoka watoke kimya.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na agizo hilo chimbuko la Muswada huu lilitokana pia na agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akifanya majumuisho ya hotuba ya bajeti ya Ofisi yake kwa mwaka 2007/2008, alifahamisha Bunge mikakati iliyochukuliwa na Serikali katika kuboresha mapato ya Halmashauri zetu. Mojawapo ya mikakati hiyo ilikuwa ni uamuzi wa Serikali wa kuitaka Mamlaka kukusanya kodi ya majengo *(property tax)* kwa niaba ya Serikali za Mitaa kuanzia mwaka 2007/2008. Hata hivyo, uamuzi huo haukuweza kutekelezwa mara moja kwa kuwa ilibidi kutoa nafasi kwa vyombo vinavyohusika kufanya maandalizi ya kutosha ikiwa ni pamoja na kupendekeza marekebisho ya sheria zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kutekeleza maamuzi ya Serikali ya kuitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya kodi ya majengo kwa niaba ya Serikali za Mitaa. Ili kufanikisha utekelezaji wa maamuzi haya inapendekezwa kuzifanyia marekebisho sheria tatu zinazohusu fedha za kodi kwa lengo la kuipa nguvu za kisheria Mamlaka ya Mapato Tanzania katika suala zima la kukusanya kodi ya majengo kwa niaba ya Serikali za Mitaa kuanzia mwaka wa fedha 2008/2009. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali za Mitaa yanayotokana na kodi za majengo ambayo kwa sasa hukusanywa kwa kiwango kisichoridhisha kutokana na Halmashauri nyingi kutokuwa na uwezo wa kitaalam wa kukusanya kodi hii. Pamoja na Halmashauri zetu kuwa na uwezo wa kisheria wa kuteua wakala wa kukusanya mapato yake kama ilivyoanishwa katika Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura Na. 290, Halmashauri hizo haziwezi kuiteua Mamlaka ya Mapato kuwa wakala wake bila sheria hii kuhuishwa kwenye sheria ya Mamlaka ya Mapato kutokana na kuwa Mamlaka ni wakala wa Serikali Kuu na imeundwa hivyo kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ya kukadiria, kukusanya na kuhasibu kodi mbalimbali za Serikali ni kwa mujibu wa Sheria.

Hivyo, mamlaka isingeweza kufanya kazi ya Uwakala wa Serikali za Mitaa bila Sheria husika kurekebishwa na kuhuishwa katika Jedwali la Orodha ya Sheria zinazosimamiwa na Mamlaka ambazo idadi yake ni 25. Hivyo basi, ni lazima ukusanyaji wa Kodi ya Majengo kwa niaba ya Halmashauri za Serikali Mitaa uwekwe kwenye Orodha hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutimiza malengo yaliyobainishwa hapo juu Muswada unapendekeza kufanyia marekebisho Sheria tatu zifuatazo:-

Kwanza, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura Namba 290;

Pili, Sheria ya Mamlaka ya Mapato ya Tanzania Sura Namba 399; na

Tatu, Sheria ya Mamlaka ya Mji Sura Namba 289.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kushirikiana na Halmashauri za Serikali za Mitaa kuwa Wakala wa kukusanya Kodi ya Majengo;

Pili, Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kushirikiana na Halmashauri za Serikali za Mitaa kuwa mamlaka ya kuthamini majengo kwa kuzingatia taratibu zilizoainishwa chini ya Sheria ya Kodi; Mamlaka ya Miji na kuhasibu kodi itakavyokusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Nne. Sehemu ya Kwanza, yenye kifungu cha kwanza na pili, inahusu masuala ya utangulizi, kama vile jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Muswada wenyewe ambapo Sheria hii itaanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai, 2008.

Sehemu ya pili, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura Namba 290 kama ifuatavyo:-

(a) Kurekebisha kifungu cha nne kinachohusu tafsiri ya maneno mbalimbali ili kuhuisha tafsiri ya maneno Mamlaka ya Mapato Tanzania ndani ya Sheria hii.(b)Kurekebisha Kifungu cha 31 kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuingiza Kifungu kipya cha 31(a) ili kuanza kutoa nguvu za Kisheria kwa TRA kwa kushirikiana na Halmashauri za Mitaa kuwa Wakala wa Serikali za Mitaa katika kukusanya Kodi za Majengo.

(ii) Kumpa mamlaka Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kutangaza kupitia Gazeti la Serikali maeneo ya Halmashauri ya Mji au maeneo mengine ambayo *TRA* itakusanya kodi kadri itakavyohitajika.

(iii) Kubainisha kwamba TRA watafaidiwa na Halmashauri madhara na hasara endapo zitatokea wakati wa kutekeleza majukumu yao. Aidha, Halmashauri hazitahusika

na madhara au hasara zitakazosababishwa na Mamlaka ya Mapato katika utekelezaji wa shughuli zake.

(iv) Kubainisha kwamba taratibu za ukusanyaji kodi zinazotumiwa na *TRA* katika Sheria ya Kodi ya Mapato na zinazotumika katika Sheria ya Kodi Mamlaka ya Mji zitatumika kwa pamoja katika kukusanya Kodi ya Majengo.

Kwanza, kuingiza Kifungu kipya cha 31(b) ili kubainisha kwanza *TRA* itafanya tathmini ya majengo kwa kushirikiana na Halmashauri za Serikali za Mitaa kwenye maeneo ya Mamlaka ya Mji au maeneo mengine ya Halmashauri ambayo watakuwa ni Wakala wa Halmashauri katika kukusanya Kodi za Majengo.

Aidha, *TRA* itaandaa orodha ya walipa kodi na kiasi cha kodi kinachopaswa kutozwa kwa kila mlipa kodi kwa kuzingatia taratibu zilizoainishwa katika Sheria ya Kodi ya Mamlaka ya Miji.

Pili, migogoro itakayohusu tathmini ya majengo na ulipaji wa kodi kwa maeneo ambayo TRA ni Wakala itashughulikiwa kwa kuzingatia taratibu zilizopo chini ya Sheria ya Bodi na Baraza ya Rufaa za Kodi Sura Namba 408.

Tatu, kuweka muda wa Mamlaka kutekeleza shughuli zake katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania Sura Namba 399 kama ifuatavyo:-

Kwanza, kurekebisha Kifungu cha tatu kwa kuhuisha neno *'rates'* kwenye tafsiri ya neno *'revenue'* ili kubainisha kwamba Kodi ya Majengo ni mojawapo ya mapato yatokanayo na kodi zitakazokusanywa na *TRA.*

Pili, kurekebisha Kifungu cha 5(2) kwa kuongeza Kifungu kidogo kipya cha (e) ili kubainisha kwamba *TRA* na Halmashauri husika watafanya mashauriano na kukubaliana kiasi cha kodi kitakachopaswa kukusanywa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha husika.

Tatu, kurekebisha Kifungu cha 14 kwa kuongeza Kifungu kidogo kipya cha 8 ili kubainisha kwamba *TRA* itatoa misamaha ya Kodi ya Majengo baada ya kushauriana na Halmashauri husika.

Nne, kurekebisha jedwali la kwanza kwa kuongeza katika Orodha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura Namba 290 na Sheria ya Kodi ya Mamlaka ya Miji Sura Namba 289 kuwa ni miongoni mwa Sheria zitakazosimamiwa na *TRA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mamlaka ya Miji Sura Namba 289 kama ifuatavyo:-

Kwanza, kurekebisha Kifungu cha 4 ili kutoa uwezo kwa *TRA* wa kushauriana na Halmashauri za Serikali za Mitaa kuchagua Mtathmini wa Majengo kwa ajili ya kutathmini majengo yaliyopo kwenye maeneo ambayo TRA ni Wakala wa Serikali za Mitaa katika kukusanya Kodi za Majengo.

Pili, kurekebisha Kifungu cha 23 kinachohusu Misamaha ya Kodi ya Majengo kwa kuongeza Kifungu kidogo kipya cha 6 ili kubainisha kwamba misamaha ya kodi inayotolewa chini ya Kifungu cha 23 haitahusu maeneo ambayo TRA ni Wakala wa Serikali za Mitaa katika kukusanya Kodi ya Majengo.

Tatu, kurekebisha Kifungu 49 kinachohusu kosa kwa mpangaji wa jengo au nyumba atakayekataa kubainisha jina la mmiliki au mpokeaji wa kodi ya pango ya jengo au nyumba husika, inapendekezwa kuongeza faini kwa kosa hilo kutoka kiasi kisichozidi shilingi 100 na nyongeza ya kiasi kisichozidi shilingi 10 iliyopo hivi sasa kwa kila siku ambapo faini hiyo itakuwa haijalipwa na kuwa asilimia 20 ya kodi ambayo itakuwa haijalipwa.

Endapo mpangaji wa jengo au nyumba ataendelea kukataa kubainisha jina la mmiliki au mpokeaji wa kodi ya pango ya nyumba au jengo husika mwezi mmoja baadaye pamoja na miezi inayofuata atatozwa zaidi ya asilimia 5 ya kodi hiyo kwa kila mwezi. Aidha, faini yote kwa ujumla hatozidi kiwango cha kodi kinachodaiwa katika jengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii ina lengo la kuongeza mapato ambayo hivi sasa hukusanywa kwa kiwango kisichoridhisha na Halmashauri hizi, na pia kuwajengea uwezo wa utaalam watumishi wa Halmashauri katika ukusanyaji kodi katika kutekeleza dhamira ya kupeleka Madaraka kwa Wananchi *D by D.* Sambamba na hatua hii TRA itakuwa inazijengea uwezo Halmashauri hizi ili baadaye ziweze kukusanya zenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba mjadili Muswada ulio mbele yenu kwa lengo la kuuboresha na hatimaye kuiwezesha Serikali kuukamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Msemaji wa Kamati iliyo chambua Muswada huu. Mheshimiwa Mwenyekiti mwenyewe Dr. Abdallah Omar Kigoda.

**MHE. DR. ABDALLAH OMAR KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** nakushukuru kwa kunipa fursa ya kutoa maoni ya Kamati yangu juu ya Muswada wa Marekebisho ya

Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2008 kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (1) ya Bunge Toleo la mwaka 2007 uliipatia Kamati yangu jukumu la kuupitia na kuuchambua Muswada huu wa marekebisho ya sheria na hatimaye kutoa maoni na mapendekezo kwa Serikali juu ya Muswada huu. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati imetekeleza jukumu hilo na hatimaye Muswada huu kuletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** katika hatua za kuchambua na kuupitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha, Kamati ilishirikiana vyema na Wizara ya Fedha, Wizara ya Mambo ya ndani ya Nchi, wataalam toka Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wataalam toka Mamlaka ya Mapato Tanzania, Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Wadau wengine wa fedha. Wote kwa pamoja walitusaidia sana katika kupata uelewa, ufafanuzi na majibu ya hoja mbalimbali za Wabunge katika kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuliongezea Taifa mapato bila kutegemea sana vyanzo vya nje, hatuna budi kuvitumia kwa ukamilifu na ufanisi vyanzo vya ndani ambavyo vingine bado havijatumiwa kikamilifu. Na katika dhana ya kutekeleza azma ya kusogeza madaraka kwa wananchi yaani kwa mantiki ya *D by D (Decentralisation by Devolution*) ni vyema mamlaka za wananchi hawa zikawa na uwezo wa kipato ili kuweza kujiendesha. Muswada huu unalenga kufanya marekebisho ya Sheria tatu zinazohusu fedha na kodi ili kuweza kuongeza mapato ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** mara baada ya kutambua uwezo, ujuzi na ufanisi wa *TRA* katika kukusanya kodi, Kamati yangu imekubali kimsingi TRA wafanye kazi ya kukusanya Kodi ya Majengo katika Halmshauri zetu. Kisheria *TRA* inaruhusiwa kukusanya aina 23 za kodi na hivyo basi, kama itapaswa kukusanya aina nyingine ya kodi , kwa utawala bora, lazima Sheria iliyopo ifanyiwe marekebisho. Hii ndiyo mantiki ya kufanya marekebisho ya Sheria iliyopo mbele yetu ili *TRA* iweze kukusanya Kodi ya Majengo katika Halmshauri za Wilaya. Aidha, Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1983 vilevile itatumika na Serikali za Mitaa kufanya kazi kwa kushirikiana na *TRA* katika kukusanya mapato ya Kodi za Majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza lengo la kuongeza makusanyo ya Serikali za Mitaa, marekebisho ya Sheria husika yaliyowasilishwa yataipa uwezo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kukusanya Kodi ya Majengo (*Property Tax*) ambayo mapato yake yamekuwa yakilegalega kutokana na uwezo mdogo wa Halmashauri katika kukusanya kodi hizi. Mathalani takwimu zinaonyesha jumla ya majengo 279,243 yaliyofanyiwa uthamini katika Jiji la Dar es salaam katika kipindi cha miaka miwili iliyopita ambapo kati ya majengo hayo 74,000 yapo Wilaya ya Ilala, 118,037 yapo Kinondoni na majengo 87,206 yapo Temeke.

Mwaka 2005/2006 malengo ya mapato ya kodi ya majengo yalikuwa shilingi bilioni 6.2 na makusanyo halisi yalifikia shilingi bilioni 4.8 ikiwa ni asilimia 71.1. Mwaka 2006/7 malengo ya kodi hii yalikuwa shilingi bilioni 5.0 na makusanyo halisi

yalifikia shilingi bilioni 3.5 ikiwa ni asilimia 70. Kwa mwaka huu wa fedha malengo ni kukusanya shilingi bilioni 5.8 kutokana na kodi ya majengo na inaelekea Halmashauri hizi hazitafikia lengo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia nyingine, marekebisho ya Sheria hii yanalenga kuanzisha utaratibu wa Halmashauri zetu kutumia (*outsourcing*) utaalamu wa *TRA* wa kukusanya kodi kwa mantiki ya kuongeza mapato ya Halmashauri zetu kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uwezo, uzoefu, nyenzo na utaalamu walio nao TRA Kamati inaendelea kushawishika kuwa Sheria hii pia itaboresha makusanyo ya kodi hii ya majengo ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wa kitaalamu maafisa wa Halmashauri ili nao waweze kukusanya kodi hizi kwa ufanisi hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia marekebisho haya yataanza kutekelezwa katika Halmashauri za Wilaya tatu za Mkoa wa Dar es salaam, yaani Ilala, Kinondoni na Temeke kama Halmashauri za majaribio ya mpango huu mpya. Kwa kuzingatia idadi ya majengo yaliyofanyiwa uthamini katika Wilaya zote hizi tatu, ni wazi kuwa kodi ya majengo ni chanzo kikubwa cha mapato kwa Halmashauri husika. Sheria imetenga miaka mitano kwa majaribio haya ingawa pia imeacha mwanya kwa Halmashauri zingine kutekeleza mpango huu hata kabla ya kumalizika kwa muda huu pale Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa atakapoona inafaa kwa Halmashauri husika kuanza kutekeleza mpango huu.

Halmashauri za Wilaya katika Mikoa ya Tanga, Arusha, Mwanza, Mbeya, Iringa na Dodoma na kadhalika ni maeneo yanayoweza kufaidika na utaratibu huu wa kwa nia ya kuongeza kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii pia inaipa mamlaka *TRA* kwa kushirikiana na Halmashauri kuthamini majengo (*valuation*) kwa kuzingatia taratibu zilizoainishwa chini ya Sheria ya Kodi ya Mamlaka ya Miji na kuhasibu kodi itakayokusanywa. Hii itawezesha kukusanya mapato yanayoendana na thamani halisi ya majengo yaliyopo katika eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** ili kuweza kutenga maeneo ya Halmashauri ambayo yatahudumiwa na *TRA* Sheria pia inampa mamlaka Waziri wa Nchi – TAMISEMI ya kuchagua maeneo maalum ya Halmashauri ambayo makusanyo yake ya kodi hizi za majengo yatafanywa na *TRA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na marekebisho yatakayowezesha Waziri mhusika na Serikali za Mitaa na Waziri wa Fedha kuunda Kamati Maalum ya kuthibitisha uwezo wa Halmashauri husika, kujitegemea yenyewe katika kukusanya kodi ya majengo kwa ufanisi na tija. Aidha, Kamati hii inaweza kuongeza muda pale ambapo Halmashauri husika bado haijajitegemea kiuwezo katika ukusanyaji wa kodi husika, hata baada ya kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona haja ya kusaidia katika kuongeza mapato ya Serikali za Mitaa. Ni ukweli usiofichika kuwa baada ya kuondolewa kwa kodi kadhaa ambazo zilikuwa kero kwa wananchi Halmashauri nyingi zimejikuta zikipata makusanyo kidogo kutokana na kutokuwa na uwezo mkubwa wa kukusanya kutoka katika vyanzo vilivyobaki ikiwemo kodi za majengo.

Aidha, Kamati pia inaipongeza Mamlaka ya Mapato nchini kwa kuwa tayari kutoa mafunzo kwa maafisa wa Halmashauri katika kuboresha ukuzaji wa kodi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliweza kuchambua Muswada huu wa marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha na kutoa maoni na ushauri mbali mbali kwa Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Mapato yanayokusanywa na *TRA* katika Halmashauri hizi ni mali ya Halmashauri. Hivyo, Kamati inashauri mapato hayo yapelekwe moja kwa moja kwa Halmashauri husika baada ya makusanyo ili kuweza kutumika kwa shughuli za maendeleo katika sehemu husika na kulingana na mipango ya Halmshauri hiyo.

(ii) Utaratibu huu wa kutumia *TRA* katika makusanyo ya kodi za Halmashauri zilenge kuwajengea uwezo maafisa wa Halmashauri kuweza kufanya makusanyo haya. Kamati inashauri programu ya mafunzo ya ukusanyaji kodi yawe endelevu ili ushirikiano huu kati ya Mamlaka na Halmashauri uwe na uwiano mzuri wa kiutaalamu. *(Makofi)*

(iii) Kwa kuwa Sheria hii mpya itaipa *TRA* uwezo wa kusamehe kodi ya majengo kwa kushirikiana na Halmashauri, na kwa kuwa sasa misamaha ya kodi imefikia kiasi cha takribani asilimia 30 hadi 35 ya mapato ya Taifa, Kamati inashauri Serikali kutoa kwa tahadhari misamaha katika kodi hii ya majengo. Maeneo yanayoweza kupata msamaha huu yawe ni nyumba rasmi za ibada, hospitali za Serikali, mashule, zahanati na majengo mengine ambayo Waziri ataona yanafaa na ikiwa kuna sababu ya kufanya hivyo.

(iv) Sheria ndogondogo *(bylaws*) zitakazoonekana zinakinzana na zoezi hili la upatikanaji wa mapato kwa nia ya kuziboresha ili kujiongezea mapato. Katika kujadili Muswada huu, Kamati yangu iliona kwamba marekebisho ya Sheria ya Leseni ya usafirihsaji kwa lengo la kuwezesha pikipiki kutumika kama chombo cha usafiri wa abiria kwa malipo bado yalikuwa hayajakamilika kutokana na mazingira halisi ya usafirishaji na vyombo vyetu vinavyotumika katika usafiri nchini kwetu. Hii imetokana na sababu zifuatazo:-

(i)Vipo vyombo vya usafiri ambavyo vinatumika kwa kiwango kikubwa nchini kwetu hasa baiskeli katika Mikoa mingi hasa ile ya Kanda ya Ziwa Viktoria. Marekebisho yanayopendekezwa yamekuwa kimya katika eneo hili. Marekebisho yaliyopendekezwa hayakutoa maelezo yanayotoa mwanya (*flexibility*) wa matumizi ya vyombo vyote vya usafirishaji. Kamati yangu inaona marekebisho haya yawe *flexible* zaidi ili yaweze kutumika kwa vyombo vyote vya usafiri.

(ii) Kamati yangu ilipata tatizo la wigo wa utendaji kazi wa vyombo hivi vyote vya usafiri hasa katika Miji mikubwa. Aidha, Kamati ilipata tabu kuelewa kama ni lazima udhibiti wa vyombo hivi vya usafiri utungiwe sheria inayotaka Serikali Kuu ifuatilie au utaratibu huu uachwe kwa Halmashauri za Miji na Wilaya zinazojua mazingira ya maeneo husika ( *Geographical zones*)

(iii) Kamati inapenda kuona kuwa marekebisho haya ya Sheria yanaainisha yatakapotumika ikizingatiwa kwamba hivi sasa katika Miji yetu mikubwa mbalimbali linajitokeza tatizo la msongamano wa magari unaosababishwa na sababu mbalimbali hasa Jiji la Dar es salaam. Ni vyema ukaangaliwa utaratibu wa barabara vipi zitumike hususan katika viunganishi au yale maeneo ambapo magari makubwa hayapiti au hayafiki. Hadi Januari 2008 idadi ya magari nchini ilifikia 392,039 tu.

(iv) Kamati inaishauri Serikali iangalie jinsi ya kuiweka vyema Sheria inayorekebishwa hasa ikizingatiwa kuwa marekebisho haya ya Sheria yameletwa kwa mfumo wa leseni na sio mfumo wa usafirishaji (yaani *road traffic* )

(v)Kamati vilevile imeishauri Serikali kuweka vyema na kuainisha nani atatengeneza Kanuni za kiutekelezaji (*implementing regulations*) ili kuzuia migongano kati ya Idara ya Usalama Barabarani, Wizara ya Miundombinu na kadhalika.

(vi) Marekebisho ya Sheria hii yazingatie zaidi suala la usalama wa watu na mali zao katika kuruhusu vyombo vingine vya usafiri katika usafirishaji.

(vii) Vyombo hivi vitengenezwe kwa ubora unaokidhi viwango kwa kuzingatia ukubwa wa injini. Aidha, SUMATRA iwe makini kufuatilia ubora wa vyombo hivi.

(viii) Suala la usimamizi wa vyombo hivi litekelezwe na Halmashauri za Miji badala ya Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hii Kamati yangu haikujadili kabisa kipengele hiki kinachozungumzia Masuala ya Usafirishaji wa Leseni yanayohusiana na pikipiki, na hivyo, tungependa pia hili lingeonyeshwa kwenye *Schedule of Amendment* kwa sababu Serikali iliomba muda kulifanyia kazi eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, Kamati inapenda kumshukuru sana Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkullo, Manaibu wake Mheshimiwa Jeremiah Solomo Sumari na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, pamoja na wataalamu wao. Aidha, Kamati inawashukuru pia wataalamu wote toka Mamlaka ya Mapato (TRA), Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwezesha Muswada huu kueleweka kwa wajumbe wa Kamati na hatimaye kutuwezesha kuujadili na kuutolea maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ambao wameweza kutoa maoni na michango ya mawazo yao mbali mbali katika kuboresha Muswada huu ili hatimaye uletwe mbele ya Bunge hili Tukufu. Naomba nitumie nafasi hii kuwatambua wajumbe wote kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Fatma Fereji, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa. Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Hamad R. Mohammed, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa. Monica N. Mbega, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Mossy S. Mussa, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Dr. Omari M. Nibuka, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Sulemain Saddiq, Mheshimiwa Elizabeth Batenga na Mheshimiwa Mzee Zubeir. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Kaimu Katibu wa Bunge Dr. Thomas D. Kashillilah, pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha napenda kuwashukuru Ndugu Anselm Mrema na Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati hii, kwani sote kwa pamoja tumeweza kukamilisha maandalizi ya Muswada huu wa marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa mwaka 2008 (*Financial Laws (Miscellaneous amendment)* act, 2008).

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi ahsante sana, lakini sasa nitamwita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Anna Komu.

**MHE. ANNA M. KOMU (K.n.y. MHE. HAMAD R. MOHAMED-MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kumshukru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nguvu za kutuwezesha kuendelea kuwatumikia wananchi. Aidha, natoa shukrani zangu kwako kwa kushirikiana na Kambi ya Upinzani Bungeni katika kutimiza majukumu yetu kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Toleo la 2007, kanuni ya 53(6)(c) na 86(6) naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali za Fedha wa mwaka 2008 [*The Financial Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2008.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 5 cha Muswada kinachoongeza kifungu cha 31(a) kwenye marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290. Kwa

ujumla dhana yenyewe ni nzuri kwani inajaribu kupanua wigo na kuboresha ukusanyaji wa mapato kwa uliokuwa ukifanywa na Serikali za Mitaa za Mkoa wa Dar es salaam.

Ni matumaini ya Kambi ya Upinzani kwamba mpango huu pia hatimaye, baada ya uzoefu wa Mkoa wa Dar es salaam utaenezwa Mikoa mingine kama vile Arusha, Mbeya, Mwanza, Kilimanjaro na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji wa mapato yatokanayo na mali isiyohamishika umeanza muda mrefu kidogo lakini, ufanisi wake haukuwa nzuri, kutokana na kukosa utaalamu wa ukadiriaji, ufuatiliaji, uwekaji wa kumbukumbu na pengine ubaridhifu.

Hatua ya Serikali kuikabidhi uwakala Mamlaka ya Mapato jukumu hili ni kilio cha siku nyingi cha Kambi ya Upinzani na hasa Kamati ya Hesabu za Serikli za Mitaa, hivyo, baada ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri, Kambi ya Upinzani haina pingamizi na Muswada huu ila itapenda kutoa angalizo kwa baadhi ya maeneo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa tathmini ya Halmashauri tatu, jumla ya majengo yaliyokusudiwa kutozwa kodi ni 279,243 kwa hesabu za mwaka 2005/2006 na kukusanya wastani wa Tshs.59,000/ kwa kila jengo, kutokana na ukadiriaji uliofanywa wakati huo. Katika Muswada huu inapendekezwa kuwa ukadiriaji ufanywe kwa kuangalia thamani ya soko ya majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ina wasiwasi na ukadiriaji huu wa kuangalia soko. Kutokanana na hali halisi ya mfumko wa bei kwamba walipaji wanaweza kushindwa kwani gharama nyengine zinazomkabili mlipaji ni nyingi. Ni vyema ukadiriaji kwa kutumia tathimini ya Kiserikali itasaidia sana watu wetu kuweza kulipa kadi zao bila ya usumbufu kwani chururu si ndondondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa jengo kama lilivyo gari thamani yake hupungua kadri muda na matumizi yanavyoongezeka. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani ingependa kupata ufafanuzi juu ya muda wa kufanywa tathmini mali isiyo ondosheka kama ni kila mwaka au vipi, maana Sheria ya *The Urban Authority (Rating) Act,* sehemu ya II iko kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka miongozo iliyo wazi ili kuondokana na usumbufu usio wa lazima ambao utaweza kujitokeza.

Angalizo hili tunalitoa kwa kuelewa kuwa siku zote wananchi si kwamba hawapendi kulipa kodi ila matumizi ya kodi zao na usumbufu unaowakuta wale wenye nia ya kulipa kodi ni mkubwa mno. Kwa mfano, misururu mirefu wakati wa kupata huduma na baadhi ya watendaji wasiojali watu, ni miongoni mwa sababu zinazosababisha walipa kodi kukwepa kodi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa kodi ni mapato kwa Serikali, na madhumuni yake ni kutumika kwa huduma wanazohitaji walipa kodi. Fedha hizo zinatakiwa zitumike kwa kuboresha miundombinu, huduma za jamii na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza ni kila uchao hali ya miundombinu na huduma za jamii zinazidi kuwa mbaya hadi kufikia kila wakati kuomba wahisani waziboreshe, na Serikali husema kuwa haina fedha hata ya kuziba mashimo madogo madogo. Lakini akitokea mgeni fedha hizo hupatikana haraka, kama vile ilivyoparwa barabara ya uhuru hadi Amana Hospital wakati wa ziara ya Rais Bush. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndio mambo yanayowakatisha tamaa walipa kodi. Ni matumainio ya Kambi ya Upinzani kwamba Muswada huu pamoja na mambo mengine utaongeza ufanisi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kwa msingi huohuo wa kuona vyanzo vya mapato ambavyo havikusanywi na Halmashauri na Manispaa za miji ifanye kazi ya kukusanya mapato kwa mfano, kwenye Stendi za Mabasi makubwa na madogo katika Mikoa yote, kwenye Vivuko, Maegesho ya magari hasa katika Jiji la Dar es Salaam na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kuwa mapato yanayopatikana katika Kivuko cha Kingamboni kwamba hayatoshi kukiendeshea na kununulia vivuko vipya hadi fedha itoke Serikali Kuu, aibu kubwa.

Kwa njia hii ya Serikali kuingilia kati pale inapoona Halmashauri zinashindwa kukusanya mapato halali kwa mujibu wa sheria, utegemezi uliokithiri wa Halmashauri zetu utapungua kama si kwisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ina wasiwasi na njia za udhibiti wa wizi kwa fedha hizo zitakazokuwa zinakusanywa. Hivyo basi njia pekee ya kuhakikisha fedha hizo zinakusanywa na kufika salama zinapotakiwa kufika na kufanya kazi iliyokusudiwa ni vitambulisho vya uraia**.**

Sheria ya kila Mtanzania kuwa na kitambulisho cha uraia kitakachoainisha kumbukumbu zote muhimu ikiwemo zile za kodi, itasaidia sana kupunguza usumbufu na wizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itakuwa ni rahisi kwa mwenye nyumba kwenda Benki na kulipa kodi zote stahiki bila ya usumbufu wowote na wao wapeleke stakabadhi za malipo Halmashauri tu. Kazi ya Halmashauri ni kufanya *Bank reconciliation* kwa wakati unaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa hii ndio njia mojawapo ya kudhibiti wizi na uzembe unaofanywa na watendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante kwa maneno uliyosema. Sasa sijui ni kwa nini wachangiaji wapo watatu tu.

Kwa hiyo, wa kwanza ni Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, atafuatiwa na Mheshimiwa Chacha Wangwe na Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Ndiyo hao watatu na kama wapo wanaotaka kuchangia pia nafasi bado ipo. Mheshimiwa William Shellukindo.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango kidogo kwenye Muswada wa Kurekebisha Sheria Mbalimbali za Ukusanyaji wa Mapato wa Mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na mapendekezo ya Serikali kwamba eneo hili ni eneo gumu sana. Kwa hiyo, ni vizuri likapata msaada …..!

**NAIBU SPIKA:** Eneo lipi? Eneo gani hilo?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasema eneo hili la kukusanya kodi za majengo, ni eneo gumu sana. Hasa ugumu mkubwa uko katika utaalamu wa ukadiriaji. Mimi nadhani tusiishie hapa tu kwenye *TRA* kuchukua jukumu hili kwa niaba ya Halmashauri kwa muda. Mimi nadhani zoezi la kufanya hivyo lingekwenda sambamba na hatua za kufanya mafunzo kufundisha wakadiriaji. Kwa sababu tatizo halipo katika kukusanya, tatizo lipo katika kukadiria, ukishajua ni kiasi gani basi ukusanyaji unakuwa mwepesi. Kwa hiyo, nadhani *TRA* wasishikilie kwenye kukusanya zaidi, wajenge uwezo na pengine wangefanya hiyo kazi pamoja na hao watu ambao baadaye wanaweza kuifanya Halmashauri, wasiifanye wenyewe tu halafu baadaye unasema sasa ingieni mwendelee. Lakini kwa sababu Serikali ni moja, Serikali Kuu na Halmashauri za Miji ambazo pengine tutaanzia basi huo utaratibu wa kufanya kazi hiyo pamoja ili hao wajifunze wapate uzoefu wa *TRA*, halafu *TRA* inasogea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kodi kuna mambo mawili makuu katika dola. La kwanza kabisa mamlaka ya dola inaathihirika kwenye kukusanya kodi halafu na ulinzi wa nchi, hayo mambo mawili hayo. Kwa hiyo, kama tutabaki nalo hili tutaliondoa kwenye Halmashauri, Halmashauri hizi kidola zinapungua nguvu kwa sababu kazi kubwa moja ni hii kwamba Serikali lazima ijiendeshe kwa kodi. Halafu ihakikishe kwamba nchi ipo katika usalama inalinda wananchi na mali zao. Kwa hiyo, huku tulichukua isije ikachukua muda mrefu na kama nilivyosema mimi tatizo ni kwamba hakuna wataalamu. Tungejenga huo uwezo isiwe kusisitiza kwenye kukusanya tu lakini kujenga uwezo wa kusaidia hizi Halmashauri ili ziweze kufanya kazi hiyo yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika sana na hayo mageuzi yanayokuja katika kufanya kazi za Serikali. Nimefarijika sana na hili pendekezo la kutumia faini kwa

kutumia asilimia, linasaidia sana hili kupunguza migogoro.  Kwa mfano, hivi nilivyosema kama mtu hajalipa kodi yake ya jengo na amepitisha muda ule unaotakiwa na unazungumza asilimia 20 basi hakuna kubishana, hapo ni asilimia 20.  Kwa hiyo, napendekeza kwamba hata kodi nyingine au faini nyingine toeni kwenye utaratibu wa thamani wa kile kitu basi kwa asilimia, hapo hakuna kuzungumza maana iko wazi kabisa itapunguza hata masuala ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kimoja hapa ambacho nadhani kimeahirishwa lakini nadhani kisiahirishwe kwa muda mrefu sana.  Nimesikiliza hapa kwa muda mrefu sana wenzetu wa mikoa ya Ziwa Victoria kule usafiri wa baiskeli, pikipiki ni muhimu sana na umepigiwa kelele.  Nakumbuka kulikuwa na ahadi kwamba suala hili linangojea sheria itungwe sasa hapa imekuja tu kwa njia ya leseni.  Lakini kubwa zaidi ni kwamba sheria hiyo itungwe kuhalalisha matumizi ya baiskeli za miguu mitatu, halafu na pikipiki za miguu mitatu.  Kwa kuwa halikuzungumzwa nadhani tutoe maelekezo kwamba hili lifanyiwe kazi wale wenzetu ambao wanategemea sana pikipiki hizi ziwe ni wazi kabisa na ziwe ni pikipiki za miguu mitatu.  Hapa katika lugha nimeiona amezungumza *tricycle,* ni baiskeli ya miguu mitatu, labda tutafute jina kwa hiyo pikipiki inaitwa nini labda *tri-motorcycle* .  Ukiacha tu *tricycle* ni baiskeli, kimataifa nje wanatumia sana hiyo ni jina lake hilo.

Sasa ukiacha katika sheria hiyo kwanza *tricycle* ni kwamba ni baiskeli ya miguu. Lakini kwenye madhumuni na sababu ametumia vizuri sana ni *motorcycle* na *tricycle*. *Motorcycle* za magurudumu matatu na baiskeli za magurudumu matatu.  Hivyo vitu ni viwili tofauti.  Maana kile kimoja cha baiskeli hakina nguvu ya mashine lakini pikipiki ina nguvu ya mashine.  Kwa hiyo, naomba sana hili litiliwe mkazo lisikae muda mrefu. Nakumbuka kuna wakati lilikuja hapa ilikuwa kwenye maswali ya Bunge, nakumbuka kabisa wenzetu wa Mkoa wa Mwanza walizungumza kwa nguvu sana kwamba ni usafiri unaotegemewa.

Kwa hiyo, ni vizuri tutatue tatizo hilo.   Niseme nina machache tu ya kuzungumza, naunga mkono mabadiliko haya yanayotakiwa kufanywa, lakini nasisitiza kwamba la msingi zaidi ni kujenga uwezo (*capacity building)* kwa zile Halmashauri ili zifanye kazi hiyo.  Kwa hiyo, huu muda wa *TRA* kukasimiwa hiyo kazi iende sambamba pamoja na kujenga hiyo *capacity*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:**  Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, ningependa kuchangia kama ifuatavyo.  Huu Muswada wa "*The Financial Laws"* ni Muswada muhimu sana na umekuja ukiwa umechelewa.  Kwa sababu kikatiba na hii inahusu nchi zote na Serikali zote, wajibu wa mwananchi ni kulipa kodi.  Kwa hiyo, kila nchi ni lazima mwananchi alipe kodi, huo ndio wajibu wake wa Kikatiba. Wajibu wa Serikali wa Kikatiba ni kukusanya kodi.  Kwa hiyo, Serikali yoyote ambayo ina uzembe wa kukusanya kodi inajiondoa katika orodha ya Serikali zinazofaa kutawala.

Ningependa kumkumbusha kwamba hili suala la kukusanya kodi katika nchi yetu limekuwa likizembewa sana. Kwamba tangu uhuru kodi zimekuwa zikikusanywa lakini sio kwa kiwango kinachotakiwa. Lakini hata zile zilizokusanywa hazijulikani wazi wazi kwamba zilifanya nini ndiyo maana wananchi wanakuwa wanavunjwa moyo katika kulipa kodi. Kwa sababu haiwezekani wananchi wawe wanalipa kodi halafu hawaoni ile kodi inafanya nini. Sasa mkataba uliopo tukiacha mambo ya Ilani za vyama, mkataba uliopo ni kwamba mwananchi lazima alipe kodi na Serikali lazima ikusanye kodi. Halafu itumie ile kodi kutoa huduma muhimu za kijamii kwa wananchi. Ndiyo maana katika nchi zote wajibu wa kujenga barabara, madaraja, shule, hospitali na kadhalika ni wajibu wa Serikali.

Watu kama wa nchi za Ulaya wanalipa kodi kubwa sana na kila mtu anajua anawajibika kulipa kodi, ndiyo maana lazima unapokuwa na kitambulisho chako kionyeshe vilevile kama unalipa kodi. Lakini sasa unapokuwa unalipa kodi halafu huoni ile kodi inakusaidiaje, hii ndiyo inayovunja moyo wananchi kwa sababu sasa hivi nchi yetu haina barabara, shule, hospitali, maji mijini na vijijini. Lakini kwa sababu elimu ya uraia haijaenea vizuri wananchi wanashindwa kuibana Serikali kwa kufahamu kwamba Serikali inatoa misaada. Kwa hiyo, Serikali yetu imejikita katika sera ya kuonyesha kwamba kila kitu wanachopelekewa wananchi ni misaada.

Kwa hiyo, hata Mawaziri wanaposimama kuzungumza wanasema: "Serikali imesaidia kujenga barabara sehemu fulani, itasaidia kujenga zahanati, itasaidia kupeleka visima. Sasa ni lazima tufike mahali tuseme kwamba msaada na wajibu yaani haki ya mwananchi inaanzia wapi na inaishia wapi? Kwa sababu sasa kila mtu anayesimama hata Mbunge hapa anasema naomba Serikali badala ya kuja na mahesabu ya kuonyesha kwamba katika jimbo lake wananchi wamelipa kodi kiasi gani na madai yao kwa Serikali kama wajibu wake kutokana na huduma wanazohitaji ni kiasi gain. Sasa wote tunakuja kuomba hapa. Tunakuja kuomba barabara, hospitali hapa, na Serikali yetu ikiondoka huku ikienda Ulaya inakwenda kuomba. Sasa tumejenga utamaduni wa ombaomba ambao hatujui utaisha lini. Lakini ningeomba sasa Katiba yetu tuifuate na irekebishwe vilevile.

**NAIBU SPIKA:** Wanasema wewe mwenyewe mbona hutuambii mfano?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mfano ambao naweza kuutoa ni wa jimbo langu, linatoa fedha nyingi sana Serikalini. Lakini ugomvi ulioko pale ni kwamba hatujui hizo fedha zinatusaidiaje? Jimbo langu linatoa zaidi ya shilingi bilioni 300 kila mwaka. Kwa mfano, sasa hivi Serikali imepeleka Polisi wengi pale kupiga watu 92, wako ndani kwa sababu wanaokota mawe ya dhahabu. Yale mawe wanayaokota ile nchi yetu imejaa dhahabu ni haki yetu sisi kupata dhahabu. Lakini tunaambiwa yale mawe ni ya mzungu, wakati yule mzungu mwenyewe halipi kodi kwenye Halmashauri yetu. Anatoa shilingi milioni 250 kwamba ndiyo kodi kwenye Halmashauri. Lakini katika *principles* zote za *land laws* sijui Serikali inaweza kutuambia waliweza kufikiaje *figure* kwamba kwa dhahabu anayochimba ya tani 12 kila mwaka anastahili kulipa shilingi milioni 250 kila mwaka kwenye Halmashauri. Alitumia *base* gani kufikia hilo. Kwa hiyo, maana ya kwamba dhahabu yetu inachukuliwa bure na

tunapoanza kuokota mawe ambayo tunayaona pale karibu tayari tunaletewa Polisi kwamba hiyo nchi hatujamwuzia….!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wangwe, ujielekeze kwenye Muswada!

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ndiyo Mheshimiwa Naibu Spika, narudi hapa. Nilikuwa na-*make a long points.*

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae kidogo. Huu Muswada hakuna mahali unazungumzia madini. Kama ni kodi inayozungumziwa ni ile ya majengo ambayo kawaida ilikuwa inatakiwa ikusanywe na Halmashauri lakini kutokana na Halmashauri zenyewe sasa Serikali Kuu kwa kupitia *TRA* ndiyo itakayokusanya, hiyo ndiyo *discussion*. Ukienda kwenye madini sio Muswada huu.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante mimi nilitaka kuonyesha kwamba huu Muswada una mapungufu kwa sababu katika elimu ya *economics* unapokuwa unazungumzia *land rent* ni pamoja na majengo. Hiyo kodi inayokwenda kukusanywa ni kodi inayotokana na majengo na majengo yako katika eneo linaloitwa *land rent*. Lazima tulizungumzie kwa ujumla kwamba kama Serikali imekuwa haikusanyi siku za nyuma na sasa imeamua kwamba inataka kukusanya hiyo kodi basi ikusanye vilevile na ile inayohusiana na hata maeneo ambayo yana migodi, hiyo ndiyo pointi ambayo nilikuwa nataka kuitoa.

Basi nitarudi kusema kwamba katika kukusanya hii kodi kwa mfano, kwa Dar es Salaam imeonekana wanatarajia kukusanya shilingi bilioni 6.2 kutokana na majengo 279 na 243 ambayo yamethaminiwa. Lakini Dar es Salaam yenyewe asilimia 75 ya ardhi na makazi ya nyumba za watu ni zile ambazo hazijathaminiwa na hazitambuliki kwamba ni ardhi au majengo ambayo yako pale kihalali. Ni kwamba ni asilimia 25 tu ya ardhi ambayo imethaminiwa. Kwa hiyo, hayo ndiyo majengo ambayo ni halali ya yale yanakuja kuvunjiwa yale majengo. Hivyo, inavyoonekana tunataka kuanza kuchukua kodi katika majengo ambayo hayahesabiki kwamba yako pale kihalali na wale wananchi hawajui.

Kwa hiyo, ni katika kutoa elimu ya kiraia kwamba kuna juhudi kubwa ambayo inahitajika katika kuhakikisha kwamba hii kodi inakusanywa lakini pia inawasaidia wale wananchi. Kwa sababu wale wananchi lazima waelewe hii kodi wanayolipa itarudi kwao vipi? Sio kwamba wananchi wanakusanya kodi kwenda Serikalini halafu hiyo kodi haiwezi kuelezeka kwamba inawasaidia kwa namna gani. Ndiyo maana suala ambalo linahusiana na kodi ni muhimu kwamba hicho kipengele pia kiangaliwe vizuri kwenye Katiba yetu kwamba ni kipengele gani ambacho kinaweza kuibana Serikali pale ambapo itakuwa imeshindwa kupeleka huduma za wananchi kutokana na kodi inayokusanywa. Kwa sababu katika Katiba yetu, katika wajibu muhimu Serikali hakuna namna ambayo tunaweza tukaibana pale ambapo itakuwa imeshindwa kutumia ile kodi vizuri. Ndiyo maana hata hili suala la *BoT* ndiyo sasa wananchi wanaanza kuelewa kumbe Serikali inakusanya fedha nyingi sana lakini hizo fedha haziwarudii kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili suala la kodi lina utata mkubwa sana katika nchi yetu na ningependa wananchi waanze sasa kuibana Serikali itoe hesabu kamili ya kodi inazokusanya kila mwaka na kila mkoa ili wale wananchi waweze kudai zile fedha kwa sababu kodi haiwezi ikalipwa bila sababu, kodi inalipwa kwa ajili ya kurudisha maendeleo kwa wananchi. Lakini kodi imekuwa ikilipwa lakini kodi hiyo imekuwa haiwasaidii wananchi kwa njia inayofaaa.

Kuhusu suala la usafiri hasa katika kanda ya Ziwa, sisi tunapakana na Kenya na Uganda kwa hiyo, wakati mwingine wananchi wakaweza kuona tofauti. Usafiri unaotumika zaidi ni usafiri wa pikipiki. Kwa sababu usafiri ule ni nafuu na pikipiki ina uwezo wa kwenda hata njia za vijijini za miguu. Lakini kukamata pikipiki za wananchi hakuleti maendeleo yoyote. Kwa mfano, mji wa Bukoba, Mwanza, Musoma Polisi wanashinda wakikamata pikipiki za watu na kwenda kuzirundika kule kwa ajili ya kuwapiga faini. Lakini hili ni kupoteza kodi, badala yake ni bora watozwe kodi kiasi fulani halafu zile pikipiki ziweze kusaidia wananchi kwa sababu wao ndio wanaozihitaji. Kwa hiyo, ningependa Serikali iangalie namna ya kurekebisha hilo suala ili huu usumbufu uweze kwisha.

Mwisho, ningependa kuishauri Serikali yetu iangalie kwamba katika kukusanya kodi inabandika matangazo na *TRA* iweze kutueleza kikamilifu kwamba kodi inazokusanya ni kiasi gani na halafu hayo matangazo yaeleze kwamba hizo kodi zimetoka wapi, eneo gani na zinatakiwa kufanya nini kwa sababu kuna giza kubwa sana katika eneo la kodi. Kwamba kodi inakusanywa lakini haina manufaa yoyote kwa wananchi wa Tanzania na tunaishia kuwa ombaomba kuomba misaada pamoja na Wabunge kukosa namna ya kusaidia majumbani. Sina zaidi, ya kwangu ni hayo tu, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Muswada huu ambao umeletwa mbele yetu.

Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wote wa jimbo langu na Wilaya yangu ya Siha kutoa pole sana kwa ndugu zetu wa Mererani ambao wamepata matatizo ambayo sisi wote tunayafahamu. Wako wengine ambao wametoka katika Wilaya ya Siha, ninachoweza kusema kwa niaba ya wananchi wa Siha ni kwamba tunawaweka hawa wote mikononi mwa Mungu na aziweke roho zao mahali pema peponi. *Amin!*

Najua kwamba ndugu zetu wa Kyela wamepata matatizo ya mafuriko, kwa hiyo, naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Siha kusema pole sana kwa ndugu zetu wa Kyela, tumemwona Mbunge wao akihangaika kwa sababu ya mafuriko na matatizo waliyoyapata na wananchi wa Siha wanapenda kusema pole sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuzungumza hapa naomba nitangaze maslahi yangu (*declare interests).* Mimi ninayezungumza hapa ukiacha kwamba ni Mbunge pia ni mwakilishi wa Mkoa wa Kilimanjaro katika *ALAT*. Lakini wakati huo

huo ni mwakilishi ambaye nilipata fursa kuingia katika Kamati ya Utendaji ya *ALAT* (*The Association of Local Authorities of Tanzania*). Kwa hiyo, Muswada unaokuja hapa unaozungumzia habari ya kuingiza *TRA* isaidie kukusanya mapato ya Halmashauri nimeshiriki toka mwanzo. Nimetumwa hapa niseme yale ambayo nitayasema, tumeelewana, tumezungumza bahati mbaya Waziri anazungumza hapa sikuwepo nilikuwa na tatizo la mguu nimepita hospitali, lakini tumefahamiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu katika eneo hili la kukusanya kodi sisi sasa baada ya mapendekezo ya *ALAT* kukubalika hatuna tatizo la Muswada huu, tunaunga mkono. Hata mkininukuu mnaweza, mtu akiniuliza naweza nikamwambia ni msimamo na masuala haya ya kuendesha nchi ni masuala ya msimamo. Kama huna msimamo unapata matatizo sana wakati unapofikia katika maamuzi. Ndiyo *Politics is all about position* yako na msimamo wako, hiyo ndiyo maana yake. Sasa kinachosumbua na ambacho kilikuwa kinatusumbua sana ili tuweze kushiriki wote na tuweze kupata mjadala mpana zaidi ni nini? Ni kwamba unazungumza kwamba unatoa *power* kwa wananchi kwa maana *decentralisation* na nashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hayumo humu ndani. Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni Serikali kama Serikali nyingine yoyote na tunapozungumza na Serikali Kuu tunaketi, wanazungumza na sisi tunazungumza, tunafika mahali tunakubaliana.

Kwa hiyo, tukaja tukafika mahali tukasema *decentralisation* ilimaanisha *giving more power to the people*. Baadaye tukaenda mbele zaidi tukasema *decentralisation* haiwezi kuishia kwenye kutoa madaraka kwa wananchi tu. Lazima ufike mahali useme kwamba unatoa pia na *resources*. Ndiyo maana tumeingia kwenye kitu kinachoitwa *D and D*. Sasa unapokuja hapa unapozungumza kwamba umetoa madaraka kwa maana ya Halmashauri na wakati huo huo umewapa uwezo na ndiyo bajeti zinaonekana kama zimeelekezwa kwenda kule. Ukizungumza habari ya *TRA* kwamba unakwenda kukusanya kodi kule *it is a contradiction.* Lazima ielezwe vizuri ieleweke kwamba ni kwa nini unafikia hatua hiyo. *Otherwise* kama watu hawataelewa watakwambia wewe unataka kujenga uwezo wa Halmashauri halafu wakati huo huo unaingiza chombo kinaitwa *TRA* mle ndani kinakwenda kukusanya kodi na *TRA* ni chombo ambacho mnacho pale kwa ajili ya kupeleka fedha Hazina. Fedha za nchi hii zote zinakusanywa zinapelekwa Hazina, nataka ni-*privatise* kwanza, tukafanya utafiti tukaangalia kwanza uwezo wa Halmashauri zetu ukoje.

Tulipoangalia Halmashauri zetu tukaona kwamba *collection* sawa katika eneo hili la majengo haizidi asilimia 60, asilimia 60 ni chache sana. Kwa hiyo, uwezo wa Halmashauri wa kukusanya hii kodi ya majengo inayozungumzwa hapa umeonekana kwamba ni mdogo sana. Sasa katika hali hiyo unafanya nini? Unang’ang’ana humu tu unasema sisi katika Halmashauri tuna nguvu, huna kitu. Mimi ninayezungumza hapa Mchaga, kama huna pesa maana yake *you are not powerful,* mimi nina mamlaka lakini huna uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukafika mahali tukakaa tukaulizana vizuri. Lakini huyu anayekwenda kutukusanyia kodi hii ya majengo hivi kweli pale tunachofanya ni hicho tu, tatizo liko wapi? Uwezo wetu kwanza ni mdogo sana, pili

utaalamu wetu wa kukusanya ni mdogo sana, mbinu zetu za kukusanya ni ndogo sana. Ndiyo maana humu ndani kuna mambo ambayo nitawaeleza hapa Mheshimiwa Waziri ataangalia, kwa kweli nia ya Muswada huu unaoletwa hapa si tu kuifanya *TRA* iwe wakala halafu niishie hapo, ni kuzijengea Halmashauri zetu uwezo, uzoefu na kuziwezesha ili hatimaye baada ya miaka mitano ambayo nazungumza ndani ya huu Muswada ziweze kukamilika.

Tukasema tuweke *conditions,* tukasema fedha hizi zitakwenda wapi. Fedha zikitoka hapa zikiingia Hazina pale, halafu ukasema hizi ni za Maswa hazitoki mle. Serikali inafanya kazi kama baba kule nyumbani. Fedha zikishaingia kwa baba zimeingia kwa baba, yeye ataamua hii ni *school fees,* hii ni kwa ajili ya kwenda kulima shamba, hii ni kwa ajili ya maziwa. Tukasema hatuwezi kukubali jambo hili mpaka muwaambie mtaziwekawekaje. Ndani ya Muswada huu tukakubaliana kwamba kutakuwa na akaunti maalumu ambayo itakwenda moja kwa moja kwenye Halmashauri zinazohusika. Sasa mimi siwezi kusimama hapa nikasema jambo hilo nalipinga kwa sababu hiyo *condition* imekubalika. Serikali Kuu ikienda kule mbele ikageuka ikasema aah, tena watu tumeshapitisha, ikarudi humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa mimi mtoto mdogo darasa la 7 niliambiwa kwamba kazi ya Mbunge ni kutunga sheria. Tutarudi humu ndani tutawaambia nyinyi mmetuambia kwamba tutakusanya kwa niaba yetu mmefika mle mmekusanya watu kule fedha imekwenda moja kwa moja. Jambo hili linawahusu zaidi watu walioko katika miji mikubwa. Watu walioko Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, jambo hili linawahusu kwa sababu hii ndiyo *source of income* kubwa kule kwao na *Regional Commissioner* wa Mwanza ananiangalia. Kule kwako *TRA* akakukusanyie, akipeleka Hazina huzipati hizi fedha hazitarudi kwa ajili ya kwenda kujenga uwezo wa Halmashauri. Tukakubaliana kwamba tutakuwa na akaunti maalumu na fedha zile zitakuwepo. Tunazungumza habari ya *Commission*, *TRA* inaweza ikazipeleka kule lakini ikakwambia hizi zote ni *overhead expenditure* utafanyeje? Tumekubaliana na tumeambiwa na Mheshimiwa Waziri jana na *TRA* wako hapo kwamba kwa kuanzia hakutakuwa na *commission* yoyote, itafanyika kazi ya Serikali kuziwezesha Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa sababu kwa nini nakubaliana na Muswada huu. Mimi siwezi kusema tu nimekubali lazima niseme *why*? Ndiyo lazima nieleze kwa nini nimekubali tu hivi hivi. Mimi niliona kipengele kile wamesema tunakubali zitakusanywa na nyinyi na hakutakuwa na *commission* isipokuwa pale ambapo itatokea Halmashauri yenyewe imetoa taarifa ambapo zinaisababishia *TRA* hasara ndipo watafanya *penalty* kwa maana kwamba wanawatoza, ndizo gharama zitakazoingia pale, *otherwise* hakutakuwa na tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukaenda mbele tukasema hicho kipindi kitakuwa ni kirefu kiasi gani. Tukasema hii ni kama *pilot study,* inafanyika tu kwa kipindi maalumu, wakishajengewa uwezo kuweka *clause* mle ndani ambaye inampa *mandate* Siha kusema mimi sasa nimejenga uwezo hivyo nitakusanya fedha zangu mimi mwenyewe. Sababu nyingine ya kukubali jambo hili, Waheshimiwa Wabunge nimekubali jambo hili mimi

nazungumza hapa si tu kama Mbunge wa Siha, nazungumza kama Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya *ALAT*. Tukasema hivyo iwekwe *clause* kama mnafika mahali. Mwanza wanasema *look here forget about TRA* tutakusanya sisi wenyewe, ni kwa *clause* pale itamke iseme kwamba basi hawa wanaweza kufanya hivyo. Lakini vyotevyote vile itakavyokuwa tukaweka *limit* tukasema kati ya miaka 3 na 5. Miaka 5 wakifika mahali na Waziri mwenye dhamana na Waziri mwenzako wa Fedha wakiona kwamba bado uwezo huo wa fedha haujapatikana watazungumza, watajadiliana na baadaye wanaweza wakaendelea hata *beyond 5 years*. Sisi hatuna mgogoro. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wenzangu utakapofikia wakati wa kukubali jambo hili naomba mpitishe. Msikatae, *both opposition* wamekubali na Wabunge mpitishe jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa nataka kusema jambo moja hapa kile kichwa cha habari kinasema: *"An Act to amend certain written laws for enabling Tanzania Revenue Authority to collect property tax on behalf of Local Government Authorities"*. Halafu mimi nasema *"in order to enhance councils revenue, building capacities and experience and collection of property tax"*.

Mimi maneno haya niliposikiliza kule *ALAT* na tulipozungumza kwenye Kamati tulisema maneno haya yaingie na tutaomba Mheshimiwa Naibu Waziri atakapokuwa ana *wind-up* mtuambie kama hiki kipengele kinaingia au inakuwaje. Lakini tulipendekeza kwamba Mheshimiwa Naibu Spika naona unaniangalia labda nirudie, naona unasikiliza nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *to provide for licensing* halafu kule mbele inaweza ikaendelea vyovyote kwa sababu huu mjadala wa *motor cycles* na magari na nini kama alivyosema Mwenyekiti wangu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi sitaki tena nianze ku-*contradict.* Ni kweli kwamba sisi hatukuijadili, kwa hiyo, msimamo ni ule alioutoa Mheshimiwa Abdallah Kigoda, ndiyo msimamo wetu na nilikwishasema kule mwanzoni kwamba masuala ya siasa haya ni masuala ya msimamo. Kwa hiyo, mimi siwezi kugeukageuka hapa nianze kusema mbona kule ulikwenda kusema tofauti, mimi nilikuwa ni sehemu ya mazungumzo. Kwa hiyo, naomba nizungumze hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kuhusu hawa wanaoomba misamaha. *TRA* ikija pale haiwezi kukaa ikaji- *super re-impose* halafu ikasema fulani tumemsamehe. Tulizungumza hilo na nimemsikia Mheshimiwa Shellukindo akilizungumza hapa. Uwezo wa kujua nani mwenye uwezo wa kulipia *how much* au hana uwezo na kumsamehe uko ndani ya Halmashauri yenyewe na hii Mheshimiwa Sumari naona unaniangalia haya ni masuala ya msimamo. *TRA* ilichoambiwa baada ya sisi Halmashauri ya Wilaya ya Siha kukaa chini na kuangalia tukaona hawa ndiyo wanastahili kulipa na hawa wanastahili kusamehewa. Sisi ndiyo tukasema kwamba tumewasamehe lakini barua ya kuandika kwamba umesamehewa itatolewa na *TRA* sababu nyingine ya kuunga mkono mswaada huu unaokuja hapa.

Halikuachwa tu hivi hivi, kwa hiyo, tulipokaa pale tumekunywa soda na sambusa lakini tulijua kwamba tuna wajibu na kubeba wajibu wa watu wetu kwamba hapa lazima

tuwe waangalifu. Ni kwa msingi huo, sisi tulipoangalia tuliona kwamba huu mpango ambao unaletwa na Serikali una nia njema na Halmashauri zetu. Kama wengine wanajisikia kwamba tumenyang'anywa uwezo pale hatukunyang'anywa uwezo. Matumaini yetu pale baada ya miaka mitano tunategemea kwamba Halmashauri hizi zita-*take off* zitakuwa zinafanya zenyewe bila kutegemea tena *TRA*. Kwa hiyo, kwa msingi huo tunaona kwamba hili ni jambo jema. Najua lina mawazo mengine, watu walioko nje, wanaotoa misaada nyinyi mbona mnawanyima Halmashauri uwezo lakini Halmashauri hizi zimefika mahali kama nilivyoeleza uwezo wake wa kuokota kodi umeonekana ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha naomba kurudia tena kusema kwamba nauunga mkono Muswada huu. (*Makofi*)

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali inayohusu masuala ya majengo na masuala ya usafiri. Awali ya yote kwanza ningependa kutoa pole kwa waathirika wa Tabata *dampo* wa Wilaya ya Ilala waliovunjiwa nyumba zao bila kufuatwa Sheria za nchi zinavyotaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Muswada huu umekuja wakati muafaka sana na maamuzi yaliyowekwa katika kuangalia upya masuala mazima ya majengo katika nchi hii ni muhimu na utasaidia kuongeza mapato ya kusaidia maendeleo ya wananchi. Wananchi wanapotoa kodi katika nchi yao wanategemea maendeleo mbalimbali na maendeleo hayo hayapatikani mpaka kodi zikusanywe ipasavyo.

Kwa maana hiyo ukiangalia majengo hasa ya Mkoa wa Dar es Salaam, Mkoa huu una majengo mengi sana makubwa sasa hivi katika Tanzania na ukiangalia majengo kwa mfano katika Wilaya ya Ilala, majengo ambayo sasa hivi yamejengwa Kariakoo ni makubwa sana na kwa muda mrefu majengo haya yalikuwa yanalipa kodi ambayo haistahili. Kwa mfano, nyumba ndogo ya Kariakoo ilikuwa inalipa shilingi 11,000/= mpaka 35,000/- kwa mwezi na kwa sasa majumba yote yamevunjwa na yamejengwa majumba ya kisasa ya ghorofa hadi tisa, nane, tano au sita, bado kodi zinazolipwa ni zile zile za kiwango kile kilichotathminiwa miaka ya nyuma. Kwa hiyo, katika maamuzi haya kuipa *TRA* uwezo wa kutathmini upya majengo na kuanza kupanga upya kodi nafikiri ni sahihi na yatalipelekea taifa hili kupata kodi za kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zetu bila kuficha ukweli uwezo wa kukusanya kodi ni mdogo na si kama hawapendi kukusanya kodi, kodi wanapenda kukusanya lakini ile tabia ambayo imejengwa kwa mwananchi kwamba anapelekewa *notice* ya kulipa kodi, anapelekewa nyumbani kwake na ikishafika pale wale wahusika hawahakikishi kama ile taarifa imemfikia mhusika. Na kama unavyojua hali ya sasa hivi ni ngumu sana, kwa hiyo, mtu anaona si lazima kwenda kuzipeleka pesa kule, anasema kwanza huduma muhimu sizioni. Wananchi wanasema hawapati huduma za afya za kutosha, barabara hakuna, mfano barabara ya Uhuru kutoka Buguruni kuja Kariakoo na imetengenezwa kwa sababu kaja Rais Bush. Sasa hii si sahihi inaleta taswira mbaya kwa

wale watu ambao wanalipa kodi kwamba hapa hakitengenezwi kitu cha maendeleo mpaka aje kiongozi fulani ili nchi ionekane eneo hili analopita ni zuri.

Hata hivyo, bila ya kuona aibu barabara ile ilijengwa nusu tu na nusu ikaachwa barabara ambayo haifiki kilomita tatu. Kwa hiyo, haya yote yanachangia kuwafanya wananchi wasipende kulipa kodi na kuchangia taifa lao. Hivyo pamoja na Sheria hizi ambazo tunataka kuzipitia leo hii lakini vilevile tusiwasahau kuwaangaliza vizuri sana hawa watoa kodi na tusisahau kuwapa elimu ya kutosha. Lazima watendaji wa Halmashauri wapewe elimu ya kutosha na lazima vilevile wananchi wanyewe wapewe elimu ya kutosha ya kuchangia kodi. Kwa nini wanachangia kodi, ni mambo gani muhimu wanastahili kupata wanapolipa kodi zao. Haya ni mambo ambayo yatasaidia taifa letu kupata mapato ya kutosha baada ya wananchi kupata huduma ambazo zinastahili. Lakini tumesema kwamba asilimia 75 ya majengo katika jiji la Dar es Salaam yamejengwa kiholela. Sasa hivi ndiyo wameanza utaratibu wa kuwapa vyeti wamiliki wa maeneo yale ambayo ni machache tu. Sasa naomba wananchi wote ambao wamejenga katika maeneo hayo hasa katika jiji la Dar es Salaam ili kupata uhalali walipe kodi na kuchangia maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano kwa sasa hivi eneo la Jangwani kuna nyumba ziko katika maji lakini watu wanaishi kwa sababu ndiyo maeneo ambayo wameyapata. Sasa wale nao wapewe elimu angalau kidogo kidogo isiwe sawa mtu anayekaa Jangwani au katika nyumba ambazo hazina utaratibu iwe sawa na mtu kulipa kodi mtu ambaye amejenga nyumba kubwa. Hizi kodi zitenganishwe lakini tuhakikishe Watanzania wote wenye nyumba wanalipa angalau kwa asilimia kidogo na wale wanaostahili asilimia kubwa wataendelea kulipa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* ni vizuri sasa kama walivyotangulia kusema wenzangu hapa kwamba kwa kuwa itakuwa kuna muda fulani wa ukusanyaji wao basi ni vizuri Halmashauri wachukuliwe watu wakati wanafanya zoezi la kutathmini majumba haya. Na wakati wanafanya zoezi la kutathmini thamani ya majengo watu wa Halmashauri washirikishwe katika zoezi hilo ili baadae wakija kukabidhiwa wajue kwamba nini wanawajibika kufanya badala ya kuwa *TRA* ndiyo itatathmini yenyewe na itapanga bei yenyewe na itakusanya tu kodi kwa kupitia hii akaunti ya kujitegemea. Hii itakuwa si sahihi na hatukuwafanyia haki watu wa Halmshauri katika kujua mchakato mzima wa kazi ambayo wanatakiwa waifanye katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa niingie kwenye suala la usafiri ingawa suala hili Mwenyekiti alilizungumzia kwamba bado halijajitosheleza sawasawa na kulichangia ipasavyo. Lakini ukweli usiofichika Watanzania wengi sasa hivi wanategemea usafiri kama huo wa baiskeli tatu na miguu mitatu na baiskeli ya miguu miwili na pikipiki. Sasa tusicheleweshe kwa sababu tunawapa tabu wananchi huko. Huko katika Wilaya, Mikoa na Halmashauri wananchi wanapata taabu sana na vyombo ambavyo vinasimamia vitu hivi ni usumbufu mkubwa. Kwa hiyo, ni vizuri sasa tukahakikisha tukija hapa kwenye Bajeti ikaja kikamilifu suala hili tukalipitia na kulifanyia kazi na kulipa baraka za Bunge ili wananchi wetu nao wawe katika kujikwamua kiuchumi wakiwa salama kwa mujibu wa Sheria za nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. FATMA A. MIKIDADI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2008. Pili na mimi napenda kutoa pole kwa maafa yaliyotokea Kyela pamoja na Mererani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichangie hoja chache kuhusu muswada huu. Kwanza kabisa ni kwamba hoja hii naiunga mkono asilimia mia kwa mia kabla sijasahau. Hoja hii kwa kweli ni nzuri kwa sababu ukiiangalia jinsi alivyosoma Mwenyekiti na jinsi walivyochangia wengine wote walivyoanza kuuzungumzia Muswada huu inaonyesha moja kwa moja na inaonyesha wazi muswada huu utaleta mafanikio kwa wananchi kama ifuatavyo. Kwanza itawapunguzia mzigo mzito Halmashauri zetu. Kwa sababu Halmashauri zetu hapa nchini zina uwezo tofauti tofauti, kuna Halmashauri zingine zina uwezo mkubwa na zingine zina uwezo mdogo. Sasa zile ambazo zina uwezo mdogo kazi hii ikifanywa na mtu mwingine kama *TRA* kwa kweli watapunguziwa mzigo mkubwa sana. Kwa hiyo, mzigo huu utakuwa umepunguzwa kwa Halmashauri zetu na *TRA* watakuwa wanaifanya hiyo kazi, hivyo moja kwa moja inaonyesha hapo jinsi gani tutanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo litasaidia kwa Halmashauri zetu tunajua kwamba Halmashauri zetu zinakuwa zikikusanya pesa katika maeneo mbalimbali ya uchumi. Lakini wakati mwingine unapokusanya pesa za kodi inawezekana mtu kwa bahati mbaya tu akakusanya pesa akaweka mfukoni kwa bahati mbaya tu bila kudhamiria akasema kwamba hii kodi nitaiwasilisha baadaye, baadaye ikawa basi tena kutokana na hilo inakuwa ni kashfa. Sasa kama *TRA* itakabidhiwa mzigo huu hii kashfa kwake itakuwa imeondoka kwa watu wa Halmashauri. Sasa *TRA* ikipewa mzigo huu wa kukusanya fedha za uchumi wa aina hii wa majengo, kwa hiyo, moja kwa moja Halmashauri itaweza kumwondoa kashfa hii kwake kwa maana Halmashauri itakuwa imesamilika katika masuala ya kashfa, masuala ya rushwa, wizi na itapata heshima kwa sababu kazi zake zitakuwa zinafanywa na *TRA*. Kwa hiyo, pointi hizi zote zinanifanya nikubali kwamba *TRA* kwa kweli hizi pesa za majengo hawana budi wakabidhiwe *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ambalo nataka nilizungumzie kuhusu ukusanywaji wa kodi hizi ni suala la uelimishaji wa wananchi katika matumizi ya kodi hizi. Kwa sababu wananchi wanapoona kodi hizi zinakusanywa hawajui matumizi yake, wenzangu waliotangulia wamezungumza kwamba zinatumika vipi. Kwa hiyo, ningeishauri Wizara kwa makusudi kabisa waandae semina kwa wananchi kuwaelimisha jinsi ya matumizi ya fedha hizi za makusanyo ya kodi ili nao waelewe. Kwa sababu watu wengi wanaona uvivu kutoa kodi ya majengo, wengi tu, ni kwa sababu hawajui matumizi ya fedha hizi. Kwa hiyo, na mimi naunga mkono kuwepo kwa elimu kwa ajili ya matumizi ya fedha hizi, vilevile elimu kwa Halmashauri kwamba kwa nini kazi hii tunawakabidhi *TRA* waweze kukusanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ambalo napenda kuzungumzia ni kwamba Serikali imeacha mwanya kwa Halmashauri zingine kutekeleza suala hili kabla ya miaka mitano. Yaani wakitaka wanaweza wao kuwapa *TRA* wakusanje kabla ya miaka mitano ile ambayo imeiachia Serikali. Lakini tuangalie wasije wakalipuka tu wakafanya bila ya kuangalia Sheria na Kanuni na bila kuangalia mbinu za kutumia mpango huu mpya wakaja tu wakalipuka wakafanya. Waangalie wenzao wanafanyaje, wenzao wamefaidika vipi, wenzao wamepata madhara gani na wenzao wamekuwa na matumizi yepi na matumizi yepi wameweza kufanikisha ndipo waweze kuutumia mpango huu, wasije tu wakalipuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naunga mkono hoja hii, nawatakia kila la kheri Wanakamati na lile suala la usafiri kweli ni zuri lakini tulifanyie kazi haraka iwezekanavyo ili wanaotumia usafiri wa baiskeli nao waweze kutumia kwa sababu ni wengi wanaotumia baiskeli sasa hivi. Ukiangalia huko mitaani kuna baiskeli zimekuja zile ambazo katikati hapana mti ule, zimejaa mjini pote na kila mahali. Kwa hiyo, watu wanashindwa kuzitumia kwa sababu maelekezo hakuna, sasa tunaomba Serikali iliangalie suala hili la matumizi ya baiskeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kupata nafasi ya kuchangia muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2008. Nianze kwanza kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioanza kuchangia. Kwa kweli yaliyo mengi wamekwishayazungumza na mimi kama nikizungumza nitakuwa kama narudia lakini kwa sababu ni wajibu wangu natakiwa nizungumze. Kwa hiyo, lazima na mimi nizungumze kwa yale ambayo natakiwa niyazungumze. Cha kwanza nimpongeze sana Naibu Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha muswada huu na niipongeze sana Kamati iliyohusika kutengeneza huu Muswada. Kwa kweli imetupa *guideline* nzuri na sisi kama Wabunge naona wamefanya kazi nzuri chini ya Mwenyekiti wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kabla sijaanza kuchangia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Njombe Magharibi napenda nitoe pole kwa sababu tulikuwa tuna tatizo kidogo kule Wanike tuliunguliwa na shule. Nawapa pole sana Wananchi wa Njombe Magharibi hasa kata ya Mdandu kwa kuunguliwa na shule ya sekondari, nawapa pole sana na mimi Mbunge wao nipo pamoja nao, tutashirikiana nao vizuri kutatua hili tatizo ambalo wanafunzi wanapata shida mahali pa kuishi. Lakini mbali ya hizi pole nichukue nafasi ya kipekee kukupongeza wewe kwa jinsi unavyoendesha vikao, kwa kweli umekuwa mama jasiri, tunakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kabla sijaendelea lazima nitangaze maslahi niliyonayo *(declare interest)* kwamba kabla sijawa Mbunge nilikuwa ni mkusanyaji kodi ya Serikali kupitia kampuni ya *Yono Auction Mart,* kwa hiyo, unapozungumza kuhusu kodi kwa kweli inanigusa sana. Suala la kodi ni suala muhimu na uwezo wa *TRA* kwa kweli tunaufahamu, wenzetu ni wazoefu wana utaalamu, hata nyenzo wanazo

ukilinganisha na wenzetu wa Halmashauri. Hata nilipokuwa nafuatilia hizi data ukiangalia malengo waliyojiwekea ya upande wa Halmashauri, jiji la Dar es Salaam kwa mwaka 2005/2006 walijiwekea malengo wakusanye shilingi bilioni 6.2 lakini wakakusanya shilingi bilioni 4.8 ambayo ni asilimia 71.1. Kwa mwaka uliofuata 2006/2007 wao walijipangia shilingi bilioni 5 wakakusanya shilingi bilioni 3.5 ambayo ni asilimia 70. Mwaka 2008/2009 malengo yao ni kukusanya shilingi bilioni 5.8 lakini inavyoonekana hawatafikia malengo. Kama wakifikia malengo basi ni chini ya asilimia hizo.

Kutokana na takwimu zilizopo hapo inaonyesha wazi kwamba uwezo wa Halmashauri unazidi kudorora. Kwa hiyo, ni vizuri hizi kazi za *property tax* zingekabidhiwa *TRA*. *TRA* ni wazoefu kama tulivyozungumza mwanzo, wana utalaamu na ningependekeza kwamba pamoja na kwamba tunawaongezea mzigo wa kukusanya na kodi za Halmashauri ni vizuri vilevile tuwaongezee hata marupurupu na motisha zaidi. Kwa sababu unapomwongezea majukumu mtumishi au hawa maofisa maana yake ni vizuri tuangalie na wao kwamba ni binadamu wana uwezo fulani. Kwa hiyo, ni vizuri kama wanaonyesha wanafanya kazi vizuri ni vema tuwaongezee marupurupu na motisha zaidi ili waweze kufanya kazi vizuri pamoja na kwamba wenzangu wanaanza kuguna lakini ukweli ndiyo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine ni suala la mapato mengine ambayo hatujayazungumzia hapa. Hizi *Bajaj* pikipiki ndogo zinazobeba abiria ziko pale Dar es Salaam nyingi tu. Zinasanya abiria lakini wanalipa kidogo sana au hawalipi kabisa. Kwa hiyo, na hili kwa Halmashauri ingeliangalia kwamba zile *Bajaj* zisajiliwe, zihalalishwe na zikatiwe Bima kusudi wananchi waweze kuzitumia katika Jiji la Dar es Salaam na sehemu nyingine ambazo zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala jingine ni suala la mabango, haya matangazo ya biashara. Kwa nchi ya Tanzania ninavyofahamu ni kwamba haya matangazo ya biashara kwa kweli tunapata hela kidogo sana ukilinganisha na nchi nyingine, hata Kenya wanakusanya vizuri sana kwenye matangazo ya biashara. Hata nchi nilizozitembelea kama Japani, Ujerumani, Uswisi kule kwa kweli makusanyo ya biashara ni mazuri sana. Sasa sielewi huku kwetu kwa nini matangazo ya biashara hatukusanyi kodi kama inavyotakikana. Kwa sababu tunavyokusanya haizidi asilimia 40, karibu asilimia 60 zote tunaacha. Kwa hiyo, nashauri kwamba ni vizuri tuangalie matangazo haya ya biashara mfano mabango yaanze kukusanywa na Halmashauri kupitia *TRA*. (*Makofi*)

Kwa mfano, utaona kwenye nyumba ya mtu binafsi au kwenye kuta mbalimbali wanaweka yale matangazo makubwa tu, unaweza ukaona jengo zima limeandikwa *VODACOM* au *TIGO* au sehemu mbalimbali kuta nzima zimeandikwa *TIGO* au *CELTEL*. Sasa ukiuliza yale maandishi, yale matangazo wanalipa wapi? Kwa hiyo, nafikiri kwamba haya matangazo yakibandikwa tu Halmashauri kupitia *TRA* wakusanye yale mapato. Hata kwa wenzetu wamiliki wa vyombo vya habari kwa mfano Televisheni, Redio na Magazeti yale matangazo ya biashara inafaa watozwe kodi tena ni kwa asilimia mbili, sehemu nyingine na hizi asilimia mbili zingeweza kuboresha mapato ya Halmashauri kuliko ilivyo sasa hivi yale matangazo hayatozwi kodi kabisa. Yale

matangazo tungekuwa tunapata fedha nyingi zaidi kuliko hata kwenye magari lakini kwa sababu hivyo vyanzo watu wanavi-*ignore* kwa kweli tunapata hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiria kwa *TRA* au kwa Halmashauri zinazohusika waangalie yale matangazo, tungeweza kupata kodi vizuri sana kuliko kuhangaishana na mwananchi mnyonge kumbana alipe kodi kwenye majengo, mimi naona kwa kweli siyo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kuchangia kingine kwamba haya majengo, tuwe tunaangalia majengo na majengo. Sasa mtu hujampa hata hati ya nyumba, unasema alipe *property tax*, sawa ni vizuri, lakini naona hapa ni kumwonea kwa sababu suala la hati ni suala muhimu na ni suala la Serikali. Kwa hiyo, ni vizuri kama unataka kufanya tathmini, tuhangaike tuwape na zile hati za nyumba. Tunawapa hati za nyumba, *at the same time* wale watu wanaweza wakapata hata mikopo sehemu mbali mbali. Mnakusanya kodi, lakini wanakuwa na hati za nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizo *property tax*, tusiwe tunawafuatilia hata watu ambao wana vijumba vibovu vibovu. Kwa mfano, kule kwangu Ilembula, unahangaika na nyumba ya nyasi au nyumba ipo imejengwa ya bati wala haina hati. Mimi ningeshauri kwa kweli mjaribu kutafuta hati. Hati nazo tuziwekee mkazo pamoja na kwamba tutakusanya hizo kodi. Hati ni jukumu la Serikali lisiwe jukumu la mwananchi, anahangaika foleni mpaka anahangaishwa sana miaka na miaka hapati hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mfano hai kwamba kupata hati unaweza kuchukua muda mrefu sana zaidi hata ya miaka miwili, nina uhakika kabisa. Wakati ile hati ingeweza kutengenezwa hata mwezi mmoja, watu wanapata shida sana huko vijijini, wana nyumba nzuri lakini wanashindwa kupata mikopo. Kwa hiyo, pamoja na kwamba tutakusanya hizi kodi lakini ni vizuri tuangalie na wananchi wa kawaida wapewe hizo hati na gharama za kupata hati zisiwe kubwa kama ilivyo sasa wananchi wanapata shida sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine niseme kwamba pamoja na kwamba tunachangia Muswada wa *TRA* wakusanye *Property Tax* kwa sababu wana uzoefu kuliko Halmashauri. Vilevile tuangalie wenzangu wamezungumza kuhusu suala la hizi kodi zinatumikaje. Mtu akusanye kodi, aelewe kwamba anafanyiwa kitu gani. Lakini siyo anakusanya kodi halafu barabara bado zinakuwa mbovu, zile huduma za jamii zinakuwa mbovu. Kwa kweli wananchi wataanza kukata tama. Kwa hiyo, nafikiria kwamba kodi hizi watu wanapenda sana kukusanya lakini tuangalie na Serikali iwajibike vizuri. Nitatoa mfano kama hii barabara ya Makete – Njombe. Juzi juzi nimezungumza, inatia aibu sana, haipitiki kabisa kuna mashimo marefu na mkandarasi akiwepo….!Sijui kama nimemaliza muda?

**NAIBU SPIKA:** Bado moja!

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *Okay*! Kwa hiyo, niseme kwamba kwa kweli inasikitisha sana kwamba mtu analipa kodi, halafu barabara zinakuwa mbovu, hazipitiki na wenzetu wa *TANROADS* wanajua kabisa ile barabara ni

muhimu kwa wenzetu kwa kusafirisha mazao yao, kwa mfano, viazi mviringo kule, mbao, kusafirisha wagonjwa kupeleka Makete kule. Sasa hivi kila kitu kimefungwa, watu wanashindwa kupita, wanashindwa kabisa kabisa. Bahati nzuri nilifanikiwa kuongea hata na Meneja wa *TANROADS*, akasema Bwana, nitaenda kutengeneza, lakini mpaka sasa hivi anasema anangojea mvua. Sasa mvua! Watu wanashindwa kupita! Sasa mvua kwa nini usiweke *temporary measures* kuliko kungojea mvua iishe. Kwa kweli hali ni mbaya kule, watu wanakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwamba kwa kweli pamoja na kwamba tunajadili huu Muswada, haya mapato yanayopatikana yatumike kutengeneza miundombinu zikiwemo barabara tuziimarishe tena katika kiwango cha lami. Kwa mfano, Makete na Njombe ukitengeneza barabara ya lami kupitia kule Igosi na Kipengele, kwani kunakuwa na matatizo gani! Wananchi watazidi kutoa kodi zaidi kwa sababu wanaelewa mnawajali. Na viazi vitaweza kupelekwa sehemu mbalimbali, Kenya na nchi zingine za mbali. Kwa hiyo, nashauri kwamba pamoja na kwamba tunaujadili Muswada huu, kwa kweli kodi itumike vizuri, iboreshe miundombinu. Halafu na wenzetu wa *TRA* pamoja na kwamba tumewasifia kwamba wanafanya kazi vizuri, wajitahidi sana kuwa waaminifu kwamba wamedhaminiwa na umma, wajitahidi kufanya kazi kwa uaminifu. Wale wachache wanaopokea rushwa, wadhibitiwe au watimuliwe kazi. Lakini wale ambao wanafanya kazi vizuri tuwape zawadi za kutosha. Kwa mfano, Kamishna Mkuu na Makamishna wengine na watumishi ambao wanafanya kazi kwa malengo, wanafikia malengo, tuwape vyeti vizuri vilivyotukuka. Hata ikiwezekana tuwape motisha, tunaweza tukaamua kuwajengea majengo mazuri mazuri kwa ajili ya kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilichokuwa nafikiria hapa, kwa kweli ni vizuri watu wanapofanya kazi vizuri, tuwazawadie, tuwapongeze. Serikali ielewe kwamba wanajituma sana. Kama nilivyokuwa nazungumza mara ya kwanza, kwa vile Wabunge wenzangu wamekwishazungumza yaliyo mazuri, na mimi naona kwa kweli nisiwe mzungumzaji zaidi, niwaachie wenzangu wachangie. Kwa kweli Muswada huu umecheleweshwa, ungekuja mapema wenzetu wa *TRA* wangeweza kutusaidia mambo mengi mazuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana!

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu ambao uko mbele yetu unaohusiana na kodi ya majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naungana na wenzangu kukubaliana kwamba ni vizuri kodi hii ya *Property Tax* ikakusanywa na ndugu zetu wa *TRA*. Ni imani yangu kwamba ndugu zetu wa *TRA* watakapokusanya kodi hii, wataikusanya kwa ukamilifu na Halmashauri zetu zitapa fedha za kutosha. Ni imani yangu kwamba wataweza kukusanya kwa sababu wanao uwezo ambao wanaweza kukusanya fedha hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa kutoa angalizo kwamba ni vyema tukafahamu kwamba Serikali Kuu ni Serikali na Serikali za Mitaa nazo ni Serikali. Lakini wakati Serikali za Mitaa zinaanzishwa lengo la Serikali Kuu lilikuwa ni kuzijengea uwezo Serikali za Mitaa ili zifike mahala ziweze kujiendesha zenyewe. Na namna pekee ya Serikali za Mitaa kujiendesha zenyewe ni pale zinapoweza kukusanya mapato yake zenyewe. Lakini saa hizi ni ukweli usiofichika kwamba zaidi ya asilimia 80 ya mapato yote yanayoingia katika Serikali za Mitaa ni mapato yanayotokana na Serikali Kuu. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba huko tunakokwenda badala ya kusema kwamba tunazijengea uwezo basi zinafika mahala mwisho tutaziita tu labda ni mawakala wa kutoa huduma baada ya kuwa wamepewa fedha na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ninachokielewa kwamba hata Halmashauri zetu bado zingeweza kukusanya fedha hizi na zingeweza kukusanya fedha nyingi pasipokuwa na matatizo. Lakini ni vyema tungefahamu au tungejiuliza kwa nini Halmashauri zetu ambazo zimekuwepo toka muda mrefu, maana kwa mara nyingine zilianzishwa mwaka 1984, sasa kufikia leo ukiangalia ni miaka mingi kabisa, hazina maendeleo. Kama ni uzoefu basi ni imani yangu kwamba na zenyewe zimekwishapata uzoefu wa kutosha, lakini matatizo makubwa ya hizi Serikali zetu za Mitaa, kwanza, hazina wataalamu wa kutosha na suala hili Serikali inalifahamu vizuri. Vilevile hazina madaraka ya kutosha, maana kila kodi inayokusanywa na Halmashauri zetu, ni kodi ya majadiliano. Ukiitwa kule *TRA* kwamba unadaiwa kodi, usipoangalia, kwanza unapelekwa mahakamani, lakini wanapokusanya kodi zile wanakusanya wakiwa na Polisi.

Sasa leo zile Manispaa au zile Halmashauri zikienda kukusanya kodi zake, zinaenda kwa kubembeleza licha ya kutokuwa na wataalamu wa kutosha. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba kama tunataka tuzisaidie Serikali za Mitaa, hebu tuzijengee uwezo ambao ni pamoja na kuwa na mahakama zake zenyewe, vilevile na kuwa na Askari Polisi wake zenyewe. Maana suala la kodi si suala la lelemama, hakuna mtu ambaye anataka kutoa kodi au anayetoa kodi kiurahisi rahisi, lazima abanwe kidogo na ndio maana leo tunaipongeza *TRA* kwa sababu baada ya kuwa inao uwezo huo na ndio maana kodi zake zinakusanywa kiurahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa utaratibu ambao tunaunda, lazima tukubali kwamba tutafika mahala maana halisi ya Serikali za Mitaa tutaiondoa. Kwamba tunafika mahala tunaendelea kuzinyang'anya madaraka yake tofauti na sheria ile iliyotungwa au iliyoanzisha Serikali za Mitaa. Mimi ni imani yangu kwamba kodi ya majengo katika kuikusanya kazi kubwa ambayo inatakiwa kwanza ni kufanya uthamini. Ni kufanya uthamini wa yale majengo yaliyopo. Na kwenye zoezi hili si kazi ya *TRA*, maana leo tunayo majengo mengi ambayo yamejengwa na yaliyoanzishwa, lakini majengo hayo hayajafanyiwa uthamini. Kwa hiyo, ni vizuri tungeangalia vile vyombo vinavyofanya uthamini ambayo ni Mamlaka ya Ardhi katika kile kitengo cha *Valuation*, tukawa na *Valuers* wa kutosha na wakafanya kazi hiyo kama zoezi maalumu, waweze kufanya Mkoa kwa Mkoa, majengo yote yatambulike na thamani za majengo yale zifahamike.

Bada ya hapo sasa itakuwa ni rahisi zaidi kujua kwamba kila mmoja anapaswa atozwe kiasi gani. Kwa hiyo, kutokana na utaratibu huo, hilo ndilo zoezi ambalo kazi ya uthamini ikifanyika vizuri, basi itakuwa rahisi zaidi katika kila Mkoa na katika kila Manispaa au *Council* kufahamika wale wote wanaopaswa kutozwa kodi na Serikali itasimamia katika utozaji wa kodi. Pamoja na kwamba tulivyosema *TRA* itaanzia Dar es salaam, iwarahisishie hata wale watu walioko katika Mikoa mingine nao kuanza kutoza baada ya ule uthamini kuwa wote umekwishafanyika. Kwa hiyo, nadhani pamoja na mambo mengine, hilo ni la msingi sana ili liweze kufanikisha zoezi hili la ukusanyaji wa kodi ya majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda kusema, mbali ya kodi za majengo, zipo kodi zingine ambazo ni nyingi na fedha hizo zinapotea, na ndio maana nasema tungejikita zaidi katika kuangalia ni kwa kiasi gani tutazisaidia Halmashauri zetu ziweze kukusanya zenyewe. Mfano, kuna kodi kama ya *Hotel levy* ambayo ni asilimia 20 ya gharama alizotumia yule mlalaji. Ni kweli kwamba fedha hizi zinazotokana na *Hotel levy*, fedha nyingi sana hazikusanywi. Hazikusanywi kwa sababu *Council* hazina *power*. Lakini kuna ile kodi inayoitwa *Service levy*, kama ninavyokumbuka ni asilimia 3 ya mapato *especially* ya viwanda ambapo kodi ile ni rahisi sana kukusanywa. Leo ni rahisi kukusanywa kwa sababu kila kampuni inapokuwa inafanya biashara zake, inapofika mwisho wa mwezi inaenda ku-*submit* kule *TRA* kiasi cha mauzo kulipa zile fedha za *VAT*.

Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba kila mamlaka ya mapato inayo hesabu ya kila mfanyabiashara, mwenye viwanda na makampuni makubwa, juma la mauzo yake ya mwezi ambayo ile asilimia 3 ndiyo inayotakiwa kama *service levy*. Kwa hiyo basi, kodi kama hii ingekuwa ni rahisi zaidi nayo ikakusanywa kule *TRA* kwa sababu yale makusanyo yanawasilishwa pale kwa maana ya ile hesabu yake inakuwa ni rahisi sana kufahamika.

Lakini cha ajabu hata hiyo kodi ya *service levy* bado haikusanywi vizuri kwa sababu hata Mamlaka ya Mapato nayo haitoi ushirikiano kwa hizi *Council* kuonyesha kwamba ni kiasi gani cha *turnover* ambacho kimewasilishwa kule ili huyo mtu anayehusika aweze kutozwa kiasi hicho cha asilimia 3 kama *service levy* ambayo nayo ni makusanyo makubwa katika *Council*. Lakini yapo mengine ya mabango na hali kadhalika hayo yote ni mapato ambayo yanapaswa kukusanywa kutokana na vyanzo vya Manispaa au vya *Council* ambavyo vitasaidia katika kuinua mapato ya Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na hilo kuna hili suala la misamaha mbali mbali; kuna misamaha kama ya makanisa, shule, hospitali, lakini mbali na hiyo, iko misamaha ambayo ilikwishazungumzwa ile ya wastaafu kwa maana kwamba walikuwa ni watumishi, sasa wamestaafu na hawana uwezo wa *income* kwa sababu ndio hako *kajumba* alikojenga, ama kwa mkopo, ndiko anakoishi. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ingeangalia na hao, ingeliangalia vizuri na iliseme hilo vizuri ili kama wanapata msamaha huo basi waweze kutambulika na waweze kufaidika na msamaha kama ilivyokuwa imeamuliwa hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, mimi nizungmzie kwa ufupi sana suala la waendesha baiskeli pamoja na pikipiki. Suala hili limezungumzwa sana na wakati mwingine tunashindwa kufahamu kwamba hivi ni sheria inakuwepo kwa ajili ya binadamu au binadamu ndiye anakuwepo kwa ajili ya sheria? Ni imani yangu kwamba mahitaji ya binadamu ndiyo yanaelekeza utungaji wa sheria ili iweze kumlinda yule binadamu. Katika jengo hili hili, huu sasa ni mwaka wa pili tumezungumza suala la waendesha baiskeli pamoja na waendesha pikipiki. Na tulipolizungumza mimi nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyekuwepo alilisema hili kwamba katika kikao kijacho sheria italetwa.

Lakini na mzee wangu Mwapachu wakati akiwa Waziri wa Usalama wa Raia, aliahidi kabisa kwamba katika Mkutano ambao ungefuata sheria ingeletwa na hatimaye kuanza kutumika mara moja. Lakini cha ajabu kila leo inakuwa ni hadithi, kila leo inakuwa ni hadithi! Lakini mimi napenda niseme kwamba zipo faida nyingi sana kwa sababu kwanza, baadhi ya maeneo yetu tunayotoka, usafiri wa gari haufiki. Sasa usafiri pekee unaoweza kutusaidia ni usafiri wa baiskeli na pikipiki na leo nimesikia tena Mzee wangu, kakangu Shellukindo anazungumzia baiskeli za miguu mitatu. Jamani tulichozungumza wakati ule ilikuwa ni baiskeli za miguu miwili na pikipiki za miguu miwili. Sasa ni vizuri na hilo nalo likaangaliwa kwa haraka zaidi maana inaonekana katika Mkutano huu wa Bunge sasa inaonekana ni hadithi.

Kusema kweli baada ya kuwa sisi tumeahidiwa na Serikali, tulienda kule tukawapa wananchi matumaini kwamba hebu wake wajiandae vizuri, wasubiri Serikali inakuja na mpango mzuri baada ya kuangalia kwamba katika nchi zingine wanafanyaje. Na hata tukiangalia leo katika nchi zinazoendelea, ukienda India, yeyote ambaye amekwenda kule, kuna usafiri mpaka wa punda wanaruhusu kama usafiri ambao binadamu anaweza kutumia. Sasa sisi leo tunachoomba hapa tu usafiri wa pikipiki na baiskeli ambapo mimi ninapoangalia katika Mji wangu wa Musoma, safari fupi unayoweza kutumia teksi ni shilingi 3000/=. Lakini safari hiyo hiyo, unaweza kwenda kwa pikipiki kwa shilingi 500/=. Kwa maeneno mengine, ukienda kwa teksi mara moja, kwa pikipiki ni karibu mara 6. Lakini ukienda kwa baiskeli ni shilingi 300/=, maana yake ni kwamba ukienda mara moja kwa gari, kwa baiskeli ni safari 10. Sasa kwa watu wenye kipato kidogo kama wale wananchi wa eneo lile, huu ni usafiri ambao unawarahisishia kufika maeneo wanayotaka kwenda. Vilevile inasaidia sana kuongeza ajira kwa wale vijana kuliko sasa wanavyokaa pasipokuwa na ajira na hiyo ndiyo inayosababisha hata wakati mwingine ujambazi unazidi kwa sababu vijana wanakuwa hawana kazi!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa basi Waziri atoe kabisa tamko kuhusiana na hili kuelezea sheria inaletwa lini ili tuweze kuifanyia marekebisho na hatimaye iweze kufanya kazi. Baada ya kusema hayo, nashukuru sana. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii iliyo mbele yetu. Awali ya yote naomba kutoa rambirambi kwa niaba ya wananchi wa Bukene kwa ndugu na jamaa wote waliopata maafa kule Mererani. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze mahali pema peponi roho za

marehemu hao, Amina! Pili, naomba kutoa pole kwa wale wote waliopata maafa katika mafuriko kule Kyela.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niingine katika hoja yenyewe tunayoizungumzia. Mimi naafiki kabisa kuwapa *TRA* kazi ya kukusanya kodi kwa niaba ya Halmashauri kwa sababu najua wenyewe *TRA* wameonyesha kwamba wanaweza kukusanya kodi katika hali ya kirafiki *(friendly environment).* Najua vilevile Manispaa na Halmashauri zetu hazijawa tayari tayari katika utaalamu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano hai naweza kuutoa ule wa kwangu mwenyewe hapa. Huwa nina nyumba na huwa naletewa ile barua ya kukusanya kodi ya majengo, lakini barua yenyewe inatoka Manispaa ya Dodoma, ukienda kulipa kule Manispaa ya Dodoma vilevile watu hawaelewi wapi unalipia mpaka unamfuata yule aliyeandika kabisa uonyeshwe, lakini kila mtu pale katika ofisi inaonekana kwamba hajui hicho kitu.

Anapokuonyesha mara nyingine unakwenda kulipa kwenye kiofisi kidogo, unakuta wakati mwingine kimefungwa kule *Area D* na wakati mwingine nimekwishalipa kule kwenye ofisi moja pale *NSSF Building* na mwaka jana nilipeleka nikalipa pale katikati kwenye maduka karibu ya *One Way*. Sasa haieleweki wapi unalipa. Na unapopeleka vile vile, hujui kwamba hizi pesa unazolipa kweli za majengo zinafika kwa wale wanaohitaji kupokea hiyo kodi ambao ni Manispaa ya Dodoma!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama Makao Makuu hapa Dodoma ndiyo hali halisi ilivyo, kwa hiyo, kule kwingine ni wazi hatuna uwezo au hatuna *experience* ya ukusanyaji wa kodi. Kwa misingi hiyo, nakubalina kabisa kwamba *TRA* wafanye kazi ya kukusanya kodi zetu.

Vilevile nataka kuongeza kwamba wanapokusanya kodi, maana yake tumeona kwamba watakaa kama kwa miaka mitano au Halmashauri ikiwa tayari, siyo lazima tufike miaka mitano, wanaweza kuomba wakakusanya wenyewe. Kwa hiyo, nafikiri kwamba wakiwa wanakusanya wale *TRA*, basi kuwe na *staff* wa Halmashauri angalau mmoja au wawili wakaende nao, wakiona jinsi wanavyokusanya ili iwe kama *on job training* ili wakishapata ujuzi huo, siyo lazima waendelee kutukusanyia kodi ya majengo kwa miaka mitano, hata miwili au hata mitatu kama kipengele kinavyosema, basi uwezo huo urudi kwa Halmashauri ili Halmashauri wakusanye wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba iongezwe ile kwamba wawepo wale wafanyakazi wa Halmashauri au Manispaa wafanye kazi pamoja na *TRA* ili wajue ujuzi huo jinsi ya kukusanya kodi na baadaye wawe tayari kuchukua jukumu hilo ili Halmashauri zijitegemee zenyewe, zisionekane kwamba zinanyang'anywa madaraka yake ya ukusanyaji wa kodi na hali tunataka madaraka yarudi vijijini, yarudi kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala ambalo hasa nimesimama kuzungumzia kuomba ni lile la baiskeli. Ukiangalia hapa zinazungumziwa baiskeli kwa muda mrefu kama msemaji aliyetangulia na tuliambiwa kwamba *by November* mwaka

juzi, uamuzi ungepita, na sisi tunaotoka katika sehemu ambazo usafiri maana yake baiskeli, kwa kuwa tunazungumzia *majority* ya watu wanasafiri kwa baiskeli, na baiskeli hapa ni yenye miguu miwili na wala siyo yenye miguu mitatu, kwa sababu baiskeli ya miguu mitatu ipo Dar es Salaam.

Lakini huko kwetu kwa mfano, kwenye jimbo langu na Wilaya ya Nzega na jirani zangu wa Shinyanga, Mwanza, Tabora ni baiskeli ninayoizungumzia ya magurudumu mawili, matairi mawili. Kwa hiyo, pale unapoangalia kama wenzangu walivyotangulia kuzungumza ni kwamba mtu anaweza kuchukua teksi kutoka Bukene kuja Nzega kwa ajili ya magonjwa. Kwa mfano, mama mjamzito au magonjwa mengine tu ya kawaida au usafiri wowote ule, analipa shilingi 25,000/= kwa gari. Lakini akichukua baiskeli, analipa shilingi 1,500/=. Sasa angalia kima cha chini cha wananchi walioko kule kwetu. 1,500/= zinamfikisha kumwokoa mama mjamzito kufika hospitali, shilingi 25,000/= hawezi, maana yake unataka kufanya wajawazito washindwe kufika kliniki mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya wajawazito unayafahamu, akichelewa kufika kliniki ni tatizo, akichelewa kupata mambo mengine ya kuhudumiwa haraka, ni matatizo, hata wengine wanajifungulia nyumbani. Akishamaliza kujifungua nyumbani, wanampakia kwa baiskeli kwenda hospitali ambayo ni shilingi 1,500/=. Hawawezi kujikusanya kwa shilingi 25,000/= au 30,000/= kama wale wa mbali zaidi wanaotoka kwa mfano, Semembela, Maambali, mpaka afike Nzega itakuwa labda shilingi 50,000/=. Sasa hii pesa haipo! Kwa hiyo, ni lazima tujitahidi kuleta sheria hii mapema kama tulivyokuwa tumeahidiwa na ndivyo tulivyopeleka ujumbe kule ili tuweze kuhakikisha tunawasaidia wananchi wetu kwa hali halisi ilivyo. Ukizungumzia shilingi 25,000/= kwa ajili ya usafiri wa kuja hospitali kwa wagonjwa wetu ni fedha nyingi sana kwa mwananchi ambaye anajikakamua kwa shilingi 1,500/=, nayo anachanga kwenye ukoo ili aweze kumpeleka mama mjamzito au mgonjwa hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tunapozungumza hapa tusifikirie tu kwamba sisi wote tunatoka kwenye barabara za lami ambazo tunaweza kupitisha hiyo gari ndogo yenye matairi matatu ambayo inaitwa *bajaj* au baiskeli ya matairi matatu inayoweza kupita. Kuna njia za vichochoroni ambako baiskeli za namna hiyo haziwezi kule maporini!

Tunahitaji baiskeli ya miguu miwili ili kuhakikisha kwamba tunawasaidia wananchi na kwa kweli kama alivyosema msemaji aliyetangulia, sheria tunatunga kufuatana na mazingira na hali halisi ya watu wanavyoishi. Kwa hiyo, *majority* tunaozungumzia baiskeli, tunazungumzia baiskeli ya miguu miwili na wala siyo ya miguu mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, chonde chonde, ili kusaidia wananchi, ili kuhakikisha tunapata kupunguza vifo vya akina mama na watoto wao ambao ni watoto wetu sisi wote akina baba na wakina mama, ni lazima tufikirie hali halisi ya kumsafirisha mgonjwa kutoka kijijini, maporini, kumleta kwenye zahanati au katika hospitali zinazohusika katika Wilaya ili aweze kupata huduma anayostahili kwa kukoa maisha yake na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisema baiskeli za miguu mitatu kama nilivyosema, haziwezi kupita katika sehemu zingine maana yake ni mapori na hatuna barabara. Na kama tuna barabara, basi tuna barabara ambazo zina mchanga mwingi, kwa hiyo, matairi matatu hayawezi kupita kwenye barabara za namna hiyo.

Kwa hali halisi, naomba kusisitizia hii sheria ije upesi ili tuweze kuhakiksha kwamba wananchi wetu wanapata huduma na vilevile kupata ajira kwa vijana maana kuna vijana wengi kwa mfano, kwenye Jimbo langu, mpaka wamejiandikisha kitu kama *SACCO*, wale wanangoja ikitokea sheria tu wataanza na kupata ajira na wanaweza kutunza familia zao kutokana na baiskeli kwa sababu watu wote wanategemea baiskeli kusafiri na siyo gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia, lakini naomba hii sheria ije upesi ili tuwasaidie wananchi na kupunguza vifo vya mama na mtoto. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana1 Wale waliokuwa wameomba kuchangia, wote wamechangia na kutokana na hoja mbalimbali, lakini pia kutokana na jedwali lililogawiwa inabidi likaangaliwe tena. Kwa hiyo, napenda Wizara iweze kufanya kazi hiyo wakati wa mchana. Halafu tumegawiwa *Supplimentary Order Paper*, nyongeza ya *Order Paper* ambapo jioni pamoja na kukamilisha Muswada huu, tutakuwa na maazimio ambayo yapo hapa. Na nafikiri pia ina makosa kidogo, mchana mtagawiwa *Supplementary Order Paper* iliyo sahihi zaidi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00.

*(Saa 6.30 Mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali za Ukusanyaji wa Mapato wa Mwaka 2008 *(The Financial Laws (Miscellaneous Amendments) Bill,* 2008)

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli za Serikali mchana orodha yangu ya wachangiaji ilikuwa imekwisha, kwa hiyo tulitaka Mheshimiwa Waziri aendelee kuangalia hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Sasa nitamwita mchangiaji wa kwanza kutoka kundi la Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Sumari.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Muswada ambao uliwasilishwa hapa Bungeni asubuhi leo kuhusu Marekebisho Mbalimbali ya Fedha wa Mwaka 2008 ambao lengo lake ni kuiwezesha mamlaka ya mapato kukusanya kodi ya majengo kwa niaba ya Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuwashukuru sana Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, kwa jinsi walivyosimamia Muswada huu kwanza tulipowasilisha kwao waliusoma, waliuelewa na kuutafakari na baadaye wakaridhika kwamba sasa uko tayari kuletwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa kuwataja nikianza na Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatma Fereji, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mbunge wa Kyerwa, Mheshimiwa Devota Likokola, Mbunge wa Viti Maalum,Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mbunge wa Mikumi, Mheshimiwa Anna Maulida Komu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mbunge wa Makete.

Wengine ni Mheshimiwa Monica Mbega, Mbunge wa Iringa Mjini, Mheshimiwa Felix Mrema, Mbunge wa Arusha Mjini, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mbunge wa Ilemela, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa Mbunge wa Mfenesini, Mheshimiwa Damas Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka Mbunge wa Morogoro Mjini na Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mbunge wa Mvomero, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Mzee Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ambao walizungumza hapa Bungeni na wengine walichangia kwa maandishi pia ni kuhusu umuhimu wa Serikali kupitia mamlaka ya mapato kuzijengea Halmashauri uwezo wa kukusanya kodi ambao muswada huu una lengo la kuipa kwanza *TRA* hapa mwanzo mamlaka ya kukusanya kodi za majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika hoja hii ni Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Anna Maulida Komu, Mheshimiwa Nuru Bafadhil, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Emmanuel Luhahula.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka ya Mapato ya Tanzania *(TRA)* imekwishaanza kutekeleza agizo la kuzisaidia Serikali za Mitaa kwa kuanza na mikakati ya kujenga uwezo wa wafanyakazi wa Halmashauri zote. Kwa mwaka huu wa fedha 2007/2008 mamlaka ya Mapato ilitenga fedha za kutosha katika bajeti yake ili kutekeleza lengo hili na azma hii kwa kushirikiana na Serikali zenyewe.

Mamlaka ya Mapato ilianza kwa kufanya tathmini ya mafunzo yanayohitajika katika Halmashauri yote ili kubaini mahitaji yao ya kujijengea uwezo na baada ya kufanya hivyo ikatengeneza mitaala ya kufundishia kwa kutoa mafunzo ya majuma sita, na tangu mwezi Februari, m 2008 imekwishaanza kutoa mafunzo haya kwenye Chuo cha Mamlaka hii Dar es Salaam na tayari wanafunzi 29 mwezi huu watamaliza mafunzo yao, lakini maandalizi vilevile yamefanywa ili kuanzia mwezi wa saba mwaka huu wajiunge na Chuo mwezi ambao tunatarajia kwamba kama muswada huu ukiwa sheria basi mamlaka ya mapato itaanza kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo zaidi yataendelea kutolewa kwa watumishi ili hatimaye Halmashauri zote ziwe na uwezo wa kukusanya mapato haya, tunajua kwamba muswada huu unatoa miaka mitano ya kufanya hivyo lakini vilevile endapo Halmashauri yoyote itadhihirika kwamba imejijengea uwezo wa kukusanya mapato yenyewe bila msaada wa *TRA* basi Waziri mhusika ataweka *notice* kwenye gazeti la Serikali na *TRA* itaondoka na Halmashauri ile itaanza kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii Waheshimiwa Wabunge vilevile walisema kwamba hii haitoshi, wakati *TRA* wanapofanya kazi hii ya makusanyo ya kodi hii maafisa kutoka Halmashauri hizi wafanye kazi pamoja ili wapate uzoefu ambao ni wa kazi yenyewe na hilo litazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ya Wabunge ilikuwa kuhusu umuhimu wa kuwapatia wananchi elimu juu ya ulipaji kodi hii ya majengo na manufaa ambayo yatatokana na kodi hii. Naomba niseme kwamba mamlaka ya mapato inayo Idara maalumu kwa ajili ya Elimu kwa umma na kwa hiyo kwa kushirikiana na Halmashauri zetu mamlaka ya kodi itatumia Idara hiyo kuwaelimisha walipa kodi wananchi kuhusu dhana ya kulipa kodi hii ya majengo, wajibu wao wa kulipa kodi na manufaa ambayo yatatokana na ulipaji kodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba katika kutoa hii elimu hatutajikita kwenye kodi hii tu maana mojawapo ya changamoto ambazo tunazo Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ni jinsi ya kuongeza mapato ya Serikali, na rai tunayotoa ni Watanzania tulipe kodi, Watanzania ni pamoja na wageni tuliowakaribisha kufanya biashara nchini mwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokuwa tunafanya hivi tutapanua wigo wa ulipaji kodi na maana ya ulipaji na matumizi ya kodi yenyewe, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwenye hoja ya umuhimu wa Elimu ni Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Ame Pande Ame, Mheshimiwa Idd Azzan na Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed.

Hoja nyingine ambayo Waheshimiwa Wabunge wameitoa inahusu umuhimu wa mapato yatakayotokana na kodi hii ya majengo kurudishwa kwa wananchi kwa njia ya kutoa huduma kama za ujenzi wa miundombinu, afya na kadhalika. Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwenye hoja hii ni Mheshimiwa Janeth Masaburi, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Aloyce Kimaro na Mheshimiwa Idd Azzan.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya fedha zitakazokusanywa, kwanza zitapelekwa moja kwa moja Halmashauri kama sheria itakavyosema na itakapokuwa imepelekwa Halmashauri, na Halmashauri ikapanga matumizi yake. Tunaamini kwamba vipaumbele vya matumizi kwenye Halmashauri vitakwenda sambamba na vipaumbele vya Serikali Kuu, kwa sababu miundombinu ni kipaumbele kwa mwaka huu 2007/08 na uwezekano mkubwa ni kwamba kwa kuwa hicho kipaumbele kitaendelea katika miaka ya ijayo, naamini kwamba matumizi ya kodi hii yatakuwa kama yalivyoshauriwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge ni umuhimu wa kusambaza mpango huu wa mamlaka ya mapato kukusanya kodi nchi nzima kwa niaba ya Halmashauri, kwamba isiwe Dar es Salaam tu. Tunaamini kwamba kuanzia Ilala, Temeke na Kinondoni ni jambo jema na pale tutakaporidhika kwamba ama itakapojidhihirisha kwamba sasa tumefaulu katika lengo hili basi lengo ni kwenda nchi nzima. Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia katika hoja hii ni Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Juma Said Omar na Mheshimiwa Shelukindo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Muswada huu na itakapokuwa Sheria, itakapodhihirika kwamba Halmashauri ambayo *TRA* imeshafika, sasa ni wakati muafaka wa kwenda kwenye Halmashauri nyingine, Waziri mwenye dhamana atatangaza kwenye Gazeti la Serikali maeneo mengine ambayo *TRA* itakusanya kodi ya majengo na itakuwa kwa muda ambao hautazidi miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia katika Muswada huu ama kwa kuandika au kwa kuzungumza hapa Bungeni na kusema kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu atamalizia ambayo yamebakia. Naomba kuunga mkono.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante nashukuru, sasa nitamwita mtoa hoja Naibu Waziri, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, kwanza naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe kwa kuongoza kikao vizuri. Pili, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi. Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Vuai Abdallah, Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Savelina Mwijage.

Wengine ni Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika na Mheshimiwa Emmanuel Luhahula.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kuzungumza nikianza na Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Anna Komu, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu na mwisho ni Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Sumari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaenda katika hoja ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa mbalimbali, kwanza nilitaka nieleze jambo moja la ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumejitokeza baadhi ya Wabunge walioona kwamba sheria hii itanyang’anya madaraka ya Halmashauri zetu, nataka niseme mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba sheria hii haitanyang’anya madaraka ya Halmashauri zetu isipokuwa itaziimarisha Halmashauri zetu kitaaluma na kitaalamu katika suala zima la ukusanyaji wa kodi za majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, wale Waheshimiwa wote ambao walikuwa na wasiwasi katika eneo hili nataka niwahakikishie kwamba katika eneo hilo mambo mazuri yanakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya jumla, naomba sasa nielekee katika hoja ambazo Wabunge wengi walikuwa wanataka ufafanuzi.

**NAIBU SPIKA:** Lakini Mheshimiwa Yono Kevela alichangia kwa mdomo naona hukumtaja.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Nimemtaja Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kulikuwa na hoja ambayo Waheshimiwa Wabunge walisisitiza kwamba mapato ya kodi yatakayopatikana yarudishwe moja kwa moja kwenye Halmashauri husika badala ya kupitia Hazina. Nataka niwatambue waliochangia hoja hii ni: Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga na Mheshimiwa Riziki Omar Juma.

Nataka niseme kwamba mapato yote yatakayokusanywa yanayotokana na kodi ya majengo yatafunguliwa akaunti maalumu na akaunti hiyo itakuwa chini ya Kamishna wa kodi za ndani *TRA*, na kila mwezi makusanyo yatakayopatikana yatapelekwa moja kwa moja kwenye Halmashauri husika. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nataka nikuhakikishieni kwamba hakuna hela hata moja itakayokwenda Hazina wakati wa kutekeleza sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nataka nieleze tu kwamba kama tulivyoeleza asubuhi ya leo wakati tunawasilisha, tumesema kwamba mwaka wa kwanza tutakapokuwa tunafanya zoezi hili, au *TRA* itakapokuwa inafanya zoezi hili hakutakuwa na *agency fee* ya aina yoyote ambayo Halmashauri zitatozwa.

Tutakwenda nao mwaka wa kwanza, tutawajengea uwezo wa kukusanya wenzetu wa Halmashauri na kuelewa matatizo yao yaliyopo katika ukusanyaji. Utakapoingia mwaka wa pili ndiyo hapo tutaweza kukaa pamoja viongozi wa Halmashauri husika na *TRA* kuona ni *agency fee* ya kiwango gani iweze kuwekwa kulingana na Halmashauri inayohusika. Kwa hiyo, katika eneo hili mwaka wa kwanza nia ya *TRA* na gharama zote zitakuwa zinatoka katika *TRA*, ni kuwajengea wenzetu uwezo wa kutekeleza suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ni suala zima la utaratibu wa ukusanyaji wa kodi za majengo usiwe na usumbufu. Hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis na Mheshimiwa Idd Azzan.

Nataka niseme tu kwamba katika kukusanya kodi za majengo, kitakachowaongoza *TRA* ni sheria ya kodi ya majengo mijini, Sura Namba 290. *TRA* hawatakuja na mbinu mpya zaidi ya kuangalia sheria ili iweze kuwaongoza, kwa maana hiyo nataka nielezee kwamba hawatakwenda nje ya sheria iliyopo hivi sasa. Hata kama kutakuwa kuna ulazima wa kufanya hivyo, hawatafanya peke yao, watafanya kwa mashirikiano baina yao na watendaji wa Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la usumbufu nataka niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba halitakuwepo katika kutekeleza suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo Waheshimiwa Wabunge walitaka ufafanuzi ni suala la kuwepo kwa utaratibu mzuri wa kutoa misamaha. Wengine walionesha wasiwasi wao kwamba kuna majengo ya ibada, majengo ya jamii kama shule, nyumba za yatima na kadhalika zitahusikaje katika suala zima la utoaji wa misamaha. Napenda niseme kwamba Sheria ya Kodi ya Mamlaka ya Miji, Sura Namba 289, imetoa

orodha ya majengo ambayo yatapata misamaha, majengo ya ibada yamo, nyumba za kulelea watoto zimo lakini vilevile kama kuna majengo ambayo wamiliki wa majengo yale au wale wanaoishi katika majengo yale hawana uwezo wa kulipia hii kodi, Halmashauri husika ndiyo itakayotoa orodha na baadaye watakaa na *TRA* kuangalia hali halisi ya wale watu husika, watakubaliana na kutoa msamaha kwa majengo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba halitakuwa na usumbufu kwa sababu *TRA* hawatakwenda na kitu cha ku-*impose* katika Halmashauri badala yake watafanya kazi kwa karibu zaidi na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilichangiwa na Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Herbert Mntangi na Mheshimiwa Aloyce Kimaro. Hoja nyingine ambayo Waheshimiwa walitaka wapatiwe maelezo ni suala zima la jinsi tutakavyotathmini majengo, hoja hii imeulizwa na Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Savelina Mwijage na Mheshimiwa Herbert Mntangi. Nataka nieleze tu kwamba katika kutathmini majengo kuna njia mbili zinatumika katika dunia yetu ya leo, njia ya kwanza ni suala la *market value* yaani hali halisi kibiashara jengo lile likoje, na njia ya pili ni *replacement* value, nikilivunja jengo hili kulijenga jengo kama hili itanigharimu kiasi gani. Nataka niseme kwamba Halmashauri pamoja na *TRA* kwa kushirikiana watateua wakala wa kutathmini majengo ili baadaye ndiye atuongoze kwa utalaamu alionao wa kutathmini majengo, kwamba jengo hili gharama yake ni kiasi kadhaa na baadaye tufanye mahesabu ili tuweze kuelewa kodi kwa ajili ya jengo lile ni kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine sambamba na hilo ni kwamba baadhi ya Wabunge waliochangia walitaka kuelewa hii tathmini itafanywa kila baada ya kipindi gani, wengine wakauliza kama itafanywa kila baada ya mwaka, miaka miwili, mitatu na kadhalika. Nataka niseme tu kwamba tutaandaa Kanuni ambazo zitatuongoza lakini tathmini aghalabu itafanywa kila baada ya miaka mitano, lakini vilevile Waziri mwenye mamlaka anaweza akasema kwamba tathmini ya mji huu imepitwa na wakati, kwa hiyo, hata kama miaka mitano haijapita miaka minne anaweza kuiomba mamlaka ifanye tathmini ili kuja na vigezo vipya. Lakini Kanuni itatuelekeza tutumie njia gani kama tutatumia baada ya miaka mitano au tutatumia zote kulingana na eneo husika. Kwa hiyo, hiyo ndiyo tathmini ambayo tutakuja kuifanya katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imetolewa na Mheshimiwa Clemence Lyamba na ilikuwa ya mwisho katika suala hili ni suala zima la *TRA* kuziangalia Halmashauri katika maeneo mengine mapya ya kukusanya mapato. Nataka niseme tu kwamba Elimu itakayotolewa na *TRA* kwa watendaji wa Halmashauri itawasaidia sana watendaji wa Halmashauri kuweza kubaini maeneo mengine ambayo yana *weakness* katika ukusanyaji wao wa mapato, na *eventually* wao wenyewe watatazama ni jinsi gani ya kukusanya mapato kwa kutazama uzoefu watakaoupata kwa njia hii ya ukusanyaji wa majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nataka niseme kwamba Serikali Kuu itakuwa tayari wakati wowote, Halmashauri ikisema kwamba wanahitaji elimu ya ziada kuhusu kodi yoyote basi *TRA* au taasisi nyingine yoyote ile tutakuwa tayari kusaidiana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu, Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali na Ukusanyaji wa Mapato wa Mwaka 2008 *(The Financial Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2008)*

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 15

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Sehemu ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali na Ukusanyaji wa Mapato wa Mwaka 2008 *(The Financial Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2008)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, ninaomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima, imepitia Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa mwaka 2008 *(The Financial Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2008)*, kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Kwa hiyo, ninaomba kutoa hoja kwamba, taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

## HOJA ZA SERIKALI

## M A A Z I M I O

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuligawa nyongeza ya Orodha ya Shughli za leo na katika nyongeza hizo ni Hoja za Serikali, kwa maana ya Maazimio. Kwa hiyo, ninaamini wote mmepata na zilikuwa zinagawiwa pale nje. Atawasilisha Maazimio yote kwa pamoja, kwa sababu yana shughuli zinazolingana na Mwenyekiti wa Kamati pia atawasilisha pamoja, Wabunge mtajadili yote kwa pamoja lakini tutakapofika kufanya uamuzi, tutaamua Azimio moja baada ya jingine. Mtoa hoja.

### Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Mkataba kuhusu Masuala Maalum yahusuyo Vifaa vya Ndege Vinavyohamishika
***(The Protocol to the Convention on International Interests in Mobile Equipment on Matters Specific to Aircraft Equipment)***

**MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI (K.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu, ninapenda kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Tamko la Kuridhia Mikataba miwili na Itifaki mbili za Kimataifa inayohusu usafiri wa anga, Marekebisho ya Sheria iliyoanzisha Kamati ya Kudumu ya Kiserikali ya Usafiri wa Baraharini na Mkataba wa Makubaliano wa Kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji wa Uchukuzi wa Mizigo Ukanda wa Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu, ninaomba kutoa maelezo kuhusu Mikataba mitatu ya Kimataifa inayohusu Usafiri wa Anga, Marekebisho ya Sheria inayoanzisha Kamati ya Kudumu ya Kiserikali ya Usafiri wa Baharini na Mkataba wa Makubaliano ya Kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji wa Uchukuzi wa Mizigo Kanda ya Kati, kwenye Bunge lako hili Tukufu kwa madhumuni ya kuridhiwa. Kabla sijatoa maelezo haya, ninaomba kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu. Sina maelezo ya kutosha kuelezea wasifu wake; sote ambao tumefanya naye kazi, tunajua kwamba uteuzi uliofanywa na Mheshimiwa Rais ni miongozo ya Mwenyezi Mungu, kwa sababu anao uwezo mkubwa wa kusimamia, pia kuratibu, kuongoza kwa vitendo na yote yanayokubalika na jumuiya tunayoiongoza. Aidha, ninawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. Uteuzi wenu uwe ni kichocheo cha kutekeleza kwa vitendo, Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia nimpongeze Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto kupitia Chama cha Mapinduzi. Nina imani kubwa kwamba, kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge, si kwa bahati bali ni kwa wananchi kutambua uwezo wake wa kujenga na kutetea hoja ambazo zitaleta maendeleo kwa Wananchi wa Jimbo la Kiteto. Aidha, ninampongeze pia Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na Mheshimiwa Rais. Watanzania tupo zaidi ya milioni 36, siyo kitu cha bahati, itakuwa ni sababu ya uwezo wake wa kujenga na kutetea hoja za msingi, ambazo zina lengo la kuleta maendeleo kwa jamii na Watanzania. Ninampongeza sana kwa sababu ninamfahamu na amefanya kazi nami kwa karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na kutoa pongezi hizo, ninaomba sasa nianze kwa kutoa maelezo kuhusu Mikataba ambayo Bunge hili Tukufu linaombwa kuridhia. Umuhimu wa uchukuzi unatokana na jukumu lake la msingi la kuchochea na kukuza maendeleo ya Sekta nyingine za uzalishaji mali na utoaji huduma za kijamii na kiuchumi katika nchi yoyote duniani. Kwa misingi hii, Jumuiya za Kimataifa zimeona ni vyema kuwepo na juhudi za makusudi za kuhakikisha kwamba, huduma za uchukuzi zinatolewa kwa kiwango cha ufanisi wa hali ya juu, zenye gharama nafuu na zilizo salama. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Jumuiya za Kimataifa zimeanzisha taasisi mbalimbali, zenye lengo la kuhakikisha kwamba, huduma za uchukuzi katika kila nchi, kati ya nchi na nchi, zinatolewa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Kimataifa zinazoratibiwa na taasisi hizi. Hata hivyo, Sheria, Kanuni na Taratibu hizo ni lazima ziridhiwe na nchi wanachama kwa kufuata taratibu za Sheria za nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kwa kutambua hili, imekuwa ikichukua hatua za makusudi kuhakikisha kwamba, Sekta ya Uchukuzi inakuzwa ili iweze kuwa kichocheo cha maendeleo ya nchi yetu. Pamoja na kuwa na Sheria ambazo zinalenga kuwepo na utaratibu unaofaa wa kuhakikisha huduma za uchukuzi zinatolewa kwa viwango vinavyoridhisha; kuwa na vyombo vya udhibiti wa kuhakikisha Sheria hizo zinafuatwa; kuwa na Wakala ambazo zinatoa huduma kwa kuzingatia Sheria za nchi na za Kimataifa; na kuwa na Kanuni ambazo ndizo zinazowezesha Sheria kutekelezwa na kuhakikisha kwamba Sekta Binafsi inawezeshwa kutoa huduma za uchukuzi zilizo bora na salama. Aidha, Serikali imekuwa ikitunga Sera na kupanga Mikakati na Programu za Kutekeleza Sera hizo. Yote haya yamefanywa na yanaendelea kufanywa ili kuwa na Sekta ya Uchukuzi nchini, ambayo inaoana na matakwa ya Kimataifa, ikiwa ni pamoja na kuridhia Mikataba ambayo inaleta manufaa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitoe maelezo kuhusu Mikataba mitatu ya Kimataifa inayohusu Sekta ya Uchukuzi, ambayo ina lengo la kuboresha huduma za Sekta ya Uchukuzi katika nchi wanachama ikiwa ni pamoja na Tanzania. Mikataba hiyo pamoja na maelezo yake ni kama ifuatavyo:-

Mkataba wa kwanza ni wa Shirika la Kimataifa Linalosimamia Usafiri wa Anga *(ICAO)*, unaohusu vifaa vitembeavyo pamoja na Itifaki ya Mambo Maalum yanayohusu

Vifaa vya Ndege wa mwaka 2001 *(The Protocol to the Convention on International Interests in Mobile Equipment on Matters Specific to Aircraft Equipment of 2001).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi Mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Usalama wa Anga Duniani *(International Civil Aviation Organization),* lililoanzishwa kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Usalama wa Anga wa mwaka 1944. Shirika hili ndilo linalosimamia Usalama wa Usafiri wa Anga Duniani kwa kuweka Kanuni, viwango vya usalama na taratibu za usimamizi wa viwango hivyo katika maeneo mbalimbali, kama vile Viwanja vya ndege, mafunzo ya wafanyakazi, pamoja na ndege zenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, mwezi Novemba, 2001, Shirika hili la Kimataifa kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Uunganishwaji wa Sheria Binafsi za Kimataifa *(International Institute for the Unification of Private Internatioanl Law - UNIDROIT),* lilianzisha Mkataba wa Kimataifa wa Vifaa Vinavyohamishika *(Convention on International Interests in Mobile Equipment),* pamoja na Itifaki ya Mkataba huo kuhusu Masuala Maalum yahusuyo Vifaa vya Ndege *(Protocol to the Convention on International Interests on Mobile Equipment on Matters Specific to Aircraft Equipment).* Mkataba huo na Itifaki zilianzishwa kwenye Mkutano wa Kidiplomasia uliofanyika Cape Town, Afrika Kusini na Shirika hilo limekuwa likizitaka nchi wanachama kuridhia Mkataba na Itifaki hiyo. Tanzania ilishiriki kwenye mkutano huo na ilisaini Mkataba na Itifaki hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kuu la Mkataba ni kuimarisha usafiri duniani kwa kuweka misingi ya Kisheria, ambayo inatoa fursa kwa makampuni ya usafiri kununua vyombo vya usafiri kama vile injini za treini na mabehewa, bodi za ndege, injini za ndege, vifaa vya anga za juu na vifaa vingine vinavyohamishika, vya thamani kubwa kwa njia ya mkopo nafuu na bila kulazimika kuwa na dhamana. Itifaki ya Masuala Maalum yanayohusu vifaa vya ndege *(Protocol on Matters Specific to Aircraft Equipment)*, ilianzishwa ili kuweka utaratibu wa kisheria ambao utawezesha makampuni ya ndege duniani, kunufaika kwa kutekelezwa kwa Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo muhimu kwenye Mkataba huu yanatoa maelezo kuhusu kutoa Haki ya Kimataifa kwa baadhi ya vifaa vitembeavyo na vyenye thamani kubwa. Vifaa hivyo kama nilivyoeleza awali ni bodi za ndege, injini za ndege na ndege ndogo aina ya helikopta, mashine za treni zinazotembea kama vile injini na mabehewa na vifaa vitembeavyo nje ya anga *(Space Mobile Asset).* Maeneo mengine muhimu ya Mkataba huu ni yale yanayotoa maelezo kuhusu mazingira yanayohitaji ile haki ya Kimataifa iweze kukaziwa kisheria. Mkataba pia unatoa maelezo kuhusu hatua za kuchukuliwa endapo Mkataba kati ya mkopaji na mkopeshwaji utavunjika. Kimsingi pale ambapo Mkataba utavunjika, haki ya kuchukua chombo, haki ya kuuza chombo kwa mtu mwingine, haki ya kupata pato au faida itokanayo na matumizi ya chombo husika na haki ya kupeleka suala hili kwenye Mahakama ili liamuliwe kisheria zitatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo muhimu ya Itifaki ni yale yanayotoa maelezo kuhusu kutumika kwa Mkataba na Itifaki. Mkataba na Itifaki hii itatumika kwa vifaa vya ndege chini ya masharti ya Itifaki hii. Maeneo mengine muhimu ya Itifaki hii ni yale yanayotoa ufafanuzi kuhusu Mahakama ya nchi moja kushirikiana na Mahakama za nchi nyingine panapokea masuala ya ufilisi, kinga ya Serikali ya kutokushtakiwa au kufuatiliwa kwamba inaondolewa. Ulazima wa Itifaki kuridhiwa na nchi ambazo zimetia saini na kwamba, nchi haiwezi kuwa mwanachama wa Itifaki kama siyo Mwanachama wa Mkataba na maelezo jinsi nchi mwanachama inavyoweza kujitoa kwenye Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya kuridhiwa kwa Mkataba na Itifaki kuhusu Vifaa Vitembeavyo, pamoja na Itifaki ya Mkataba huu kuhusu masuala maalum ihusuyo vifaa vya ndege ya mwaka 2001 ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuwezesha Makampuni ya Ndege ya Tanzania mikopo nafuu ya vifaa vya usafiri wa anga kutoka kwenye Masoko ya Kimataifa.

(b) Kuongeza imani kwa wakopeshaji au wauzaji wa ndege kutokana na kuwepo kwa Sheria ya ndani inayoruhusu wakopeshaji kukamata mali iliyowekwa rehani.

(c) Kutoa fursa kwa Makampuni ya Tanzania kuwa na ndege mpya na zenye teknolojia ya kisasa

(d) Kupunguza au kuondoa utegemezi wa dhamana kutoka Serikalini, yaani *Government Guarantee* kwa makampuni ya umma yanayohitaji kununua au kukodi ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba na Itifaki zilianza kutekelezwa tarehe 1 Machi, 2006 hadi Oktoba 2007. Nchi 28 ikiwemo Tanzania, zilikuwa zimesaini Mkataba na Itifaki hii. Aidha, nchi 18 zilikuwa zimeridhia Mkataba na Itifaki hii. Kati ya nchi 18 zilizoridhia Mkataba na Itifaki hii; nchi sita zinatoka Bara la Afrika. Nchi hizo ni Angola, Ethiopia, Kenya, Nigeria, Senegal na Afrika Kusini.

Kutokana na nchi hizo kuridhia Mkataba na Itifaki hii, baadhi ya Mashirika yameweza kufaidika na mikopo itolewayo na Mashirika au Mabenki ya Kimataifa wakati wa kununua au kukodi ndege. Baadhi ya mashirika ambayo yamefaidika na mikopo nafuu kutokana na nchi zao kuridhia Mkataba na Itifaki hii ni Shirika la Ndege la Kenya *(Kenya Airways),* Shirika la Ndege la Ethiopia *(Ethiopian Airways)* na Shirika la Ndege la Afrika Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili Tukufu ninaliomba likubali kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Vifaa Vinavyohamishika *(Convention on International Interests on Mobile Equipments)* wa mwaka 2001, pamoja na Itifaki ya Mkataba huo kuhusu Masuala Maalum ya Vifaa vya Ndege *(Protocol to the Convention on International Interests on Mobile Equipment on Matters Specific to Aircraft Equipment)* ya mwaka 2001.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nisome Azimio la Kuridhia Mkataba huu na Azimio la Kuridhia Itifaki yake.

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri wa Anga Duniani *(ICAO)* wa mwaka 2001 kuhusu Vifaa Vinavyohamishika *(Convention on International Interest in Mobile Equipment).*

**KWA KUWA** nchi Wanachama wa Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri wa Anga Duniani *(ICAO)* mnamo mwaka 2001 zilipitisha Mkataba wa Shirika la Kimataifa kuhusu Vifaa Vinavyohamishika ambao Serikali ya Muungano wa Tanzania imesaini mwaka 2001;

**NA KWA KUWA** kimsingi Mkataba huu utatumika kwenye nchi wanachama wa *ICAO* baada ya nchi husika kuridhia, pale ambapo Kampuni iliyokopa iko kwenye nchi mwanachama bila kujali kama Taasisi iliyokopwa ipo kwenye nchi ambayo si mwanachama wa *ICAO;*

**NA KWA KUWA** Mkataba huu unatoa maelekezo kuhusu mazingira yanayohitajika ili maslahi ya Kimataifa *(International Interest),* yaweze kuzingatiwa kama vile Mkataba kati ya Mkopaji na Mkopeshaji, kuwa katika maandishi; Taasisi inayotoa mkopo iwe na nguvu ya kisheria ya kuuza au kutoa mkopo wa kununulia vifaa vya usafiri wa anga vinavyohamishika au kuwekwa rehani ambapo masharti kati ya mkopo au rehani yatawekwa wazi bila ya ulazima kutajwa kwa kiasi cha fedha;

**NA KWA KUWA** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuridhia Mkataba huu itawezesha Makampuni ya Tanzania kupata mikopo nafuu ya vifaa vya usafiri wa anga kutoka kwenye Masoko ya Kimataifa bila kulazimika kuwa na dhamana ya mali au dhamana ya benki *(Bank Guarantee),* badala yake makampuni husika yataweza kutumia kifaa hicho kama rehani; mikopo hii itatoa fursa kwa Makampuni ya Tanzania kuwa na ndege mpya na zenye teknolojia ya kisasa na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji na gharama nyingine zitokanazo na ndege chakavu au ndege za zamani na kupunguza au kuondoa utegemezi wa dhamana kutoka Serikalini, kwa makampuni ya umma yanayohitaji kununua au kukodi ndege;

**NA KWA KUWA** katika Kikao chake cha Baraza la Mawaziri cha tarehe 13 Machi, 2008, Baraza la Mawaziri liliazimia kuridhiwa kwa Mkataba wa Kimataifa kuhusu Vifaa vya Ndege Vinavyohamishika *(Convention on International Interest on Mobile Equipments);*

**HIVYO BASI,** kwa kuzingatia umuhimu wa Mkataba huu na manufaa ambayo Tanzania itapata kwa kuridhia; Bunge hili katika Mkutano huu wa Kumi na Moja na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sura ya 2, linaazimia kwamba, Itifaki ya Mkataba wa Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri wa Anga Duniani *(ICAO)* kuhusu Vifaa vya Ndege

Vinavyohamishika *(Convention on International Interests in Mobile Equipment on Matters Specific to Aircraft Equipment)* ya mwaka 2001 uridhiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Mkataba kuhusu Masuala Maalum yahusuyo Vifaa vya Ndege Vinavyohamishika *(The Protocol to the Convention on International Insterest in Mobile Equipment on Matters Specific to Aircraft Equipment).*

**KWA KUWA** nchi Wanachama wa Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri wa Anga Duniani *(ICAO),* mnamo mwaka 2001 zilipitisha Mkataba wa kuhusu Vifaa vya Ndege Vinavyohamishika ambayo Serikali ya Tanzania iliweka saini mwaka 2001;

**NA KWA KUWA** Shirika la Kimataifa Linalosimamia Usafiri wa Anga Duniani *(ICAO)* kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Uunganishwaji wa Sheria Binafsi za Kimataifa *(Institute for the Unification of Private International Law),* katika kikao hicho hicho cha mwaka 2001 kilipitisha Itifaki ya Mkataba Kuhusu Masuala Maalum Yahusuyo Vifaa vya Ndege Vinavyohamishika;

**NA KWA KUWA** Itifaki hii imeanzishwa ili kuweka utaratibu wa Kisheria ambao utawezesha Makampuni ya Ndege Duniani kunufaika kwa kutekelezwa kwa Mkataba;

**NA KWA KUWA** lengo kuu la Itifaki hii ni kutoa maelezo kwamba Mkataba utahusisha pia Helikopta, kutoa ufafanuzi wa kuwa wakati wowote nchi inaweza kuteua Taasisi moja au zaidi nchini mwake kuwa sehemu ya kupitisha Taarifa zinazotakiwa kwa ajili ya usajili kwenye Masjala ya Kimataifa, kuwezesha kuanzishwa Taasisi ya Usimamizi *(Supervisory Authority)* ambayo itaratibu utekelezaji wa Mkataba wa Itifaki hii na maelezo kuhusu uhusiano kati ya Mkataba wa Itifaki hii na Mikataba mingine;

**NA KWA KUWA** katika kikao chake cha Baraza la Mawaziri cha tarehe 13 Machi, 2008 Baraza la Mawaziri liliazimia kuridhiwa kwa Itifaki ya Mkataba kuhusu masuala maalum yahusuyo vifaa vya ndege vinavyohamishika;

**HIVYO BASI,** kwa kuzingatia umuhimu wa Mkataba huu na manufaa ambayo Tanzania itapata kwa kuridhia; Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Moja na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sura ya Pili, linaazimia kwamba Itifaki ya Mkataba kuhusu Masuala Maalum Yahusuyo Vifaa vya Ndege Vinavyohamishika *(Protocol to the Convention on International Interests in Mobile Equipment on Matters Specific to Aircraft Equipment)* uridhiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki nyingine ni Itifaki ya Kurekebisha Sheria iliyoanzisha Kamati ya Kudumu ya Kiserikali ya Usafiri wa Baharini ya mwaka 1987 *(Protocol Amending the Agreement Establishing the Inter-Governmental Standing Committee on Shipping (ISCOS), 2006).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni Mwanachama wa Kamati ya Kiserikali ya Kudumu ya Usafiri wa Baharini (*Inter-Governmental Standing Committee on Shipping),* iliyoundwa mwaka 1967 na nchi nne ambazo ni Kenya, Uganda, Zambia na Tanzania. Mkataba wa *ISCOS* ulianzishwa na kusainiwa mwaka 1987 na Waheshimiwa Mawaziri wanaosimamia usafiri wa majini katika nchi hizi nne. Nchi hizo ziliona kuna haja ya kuwa na chombo kimoja kitakachoratibu shughuli za usafiri baharini, kwa ajili ya kukuza uchumi na biashara ya usafiri wa bahari.

Kwa hiyo, lengo kuu la kuanzisha *ISCOS* ni kuziwakilisha nchi wanachama kwenye majadiliano na wamiliki wa meli *(shipping lines),* kuhusu masuala ya gharama za usafirishaji wa meli, usalama na mengineyo. Aidha, *ISCOS* ina lengo la kuboresha usafiri wa baharini wa nchi wanachama na watumiaji wa bandari za nchi hizo. Makao Makuu ya *ISCOS* yako Mombasa nchini Kenya.

Kutokana na mabadiliko ya Sera mbalimbali za kiuchumi na kibiashara, pamoja na mabadiliko ya kiteknolojia na kisayansi katika Sekta ya Usafiri wa Majini, hususan masuala ya udhibiti wa shughuli za biashara na huduma za meli. Mwezi Aprili, 2006, nchi wanachama wa *ISCOS* ziliamua kuifanyia marekebisho Sheria hii iliyoanzisha *ISCOS* ya mwaka 1987 kwa lengo la kuipa upeo mpana zaidi wa kiutendaji na hivyo kuandaa Itifaki ya Kurekebisha Mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya maeneo muhimu ya Mkataba ni yale yanayotoa maelezo kuhusu madhumuni ya Mkataba ili kuyapanua zaidi majukumu yaliyomo katika Mkataba, kwa kuzingatia hali halisi ya sasa katika usafiri wa baharini na rasilimali zilizomo. Uanachama wa *ISCOS* ambao unapanuliwa zaidi ili kuziwezesha nchi nyingine kujiunga na *ISCOS* hasa nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini, maelezo kuhusu watakaostahili kuwa Wajumbe wa Kamati ya Utendaji kutoka kwa wanachama kamili.

Wakati *ISCOS* ilipoanzishwa, ilikuwa na majukumu ya kuzishauri Serikali za Nchi Wanachama jinsi ya kushughulikia tozo na ada katika Sekta ya Usafiri wa Baharini; kufanya utafiti na kushauri Serikali kuhusu kiwango na muundo wa tozo na gharama za uendeshaji wa bandari; kufanya majadiliano kuhusu namna ya kuboresha usafiri wa baharini; kufanya utafiti wa masuala ya usafiri baharini inapoombwa na nchi wanachama na kufanya kazi nyingine yoyote kama itakavyoelekezwa na Serikali za Nchi Wanachama kuhusu usafiri wa baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya *ISCOS* yaliyoongezwa na Itifaki ya 2006; baada ya kuanzishwa kwa Itifaki mwaka 2006, *ISCOS* imeongezewa majukumu mapya 18. Majukumu hayo yanalenga kuboresha utendaji wa *ISCOS* na nchi wanachama kwa kuboresha taratibu na mikakati ya kuendeleza shughuli za uchukuzi majini, ikiwa ni pamoja na shughuli za bandarini; elimu ya mabaharia; kuimarisha usalama na kulinda mazingira ya viumbe, mito na maziwa. Majukumu mengine ni kuhakikisha kwamba, nchi wanachama wanasaidiana vifaa vya utafutaji na uokoaji pale yanapotokea majanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya kuridhia Itifaki ya *ISCOS* ni pamoja na kuwezesha kushirikiana na nchi wanachama katika kuboresha na kukuza Sekta ya Usafiri wa Majini na kwenda sambamba na mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia, yanayotokea katika Sekta ya Usafiri wa Baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza Bunge hili Tukufu, likubali kuridhia Itifaki ya *ISCOS* ya mwaka 2006, kuhusu Marekebisho ya Mkataba Uliyoanzisha Kamati ya Kudumu ya Kiserikali ya Usafiri wa Baharini ya mwaka 1987.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nisome Azimio la Kuridhia Itifaki hiyo.

**KWA KUWA** Kamati ya Kiserikali ya Kudumu ya Usafiri wa Baharini iliundwa mwaka 1987 kwa Mkataba uliosainiwa na Mawaziri wanaosimamia usafiri wa majini;

**NA KWA KUWA** lengo la Mkataba huo ni kuanzisha chombo kimoja cha kuratibu shughuli za usafiri wa baharini ili kukuza uchumi na biashara ya usafiri wa baharini;

**NA KWA KUWA** chombo hiki ndicho chenye dhamana na mamlaka kwa niaba ya nchi wanachama kujadiliana na wamiliki wa meli juu ya masuala ya gharama za usafirishaji wa meli, usalama na mambo mengine;

**NA KWA KUWA** mabadiliko ya sera mbalimbali za kiuchumi na kibiashara na mabadiliko ya teknolojia na sayansi katika Sekta Usafiri wa Majini, hususan udhibiti wa shughuli za biashara na huduma za meli, yamelazimu nchi wanachama kufanya marekebisho katika Mkataba uliyoanzisha Kamati ya Kiserikali ya Kudumu ya Usafiri wa Bahari wa mwaka 1987;

**NA KWA KUWA** malengo ya marekebisho hayo ni kuipatia Kamati upeo mpana zaidi kiutendaji, kuziwezesha nchi nyingine kujiunga, kuainisha Wajumbe wa Baraza Kuu na wanachama washiriki na vilevile kuwaainisha Wajumbe wa Kamati ya Kiutendaji;

**NA KWA KUWA** Tanzania ni Mwanachama wa *ISCOS* kutokana na kutia saini, kuridhia Mkataba wa *ISCOS* na kushiriki katika majadiliano ya *ISCOS* yaliyowezesha kusainiwa kwa Itifaki ya Marekebiso ya Mkataba;

**HIVYO BASI,** kwa kuzingatia manufaa ambayo Wananchi wa Tanzania watapata kutokana na kujiunga na *ISCOS* na kutokana na manufaa ambayo watapata kutokana na Itifaki ya Marekebisho; Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mkutano huu wa Kumi na Moja na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa linaazimia kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba uliyoanzisha Kamati ya Kiserikali ya Kudumu ya Usafiri wa Baharini wa mwaka 2006 *(Protocol Amending the Agreement Establishing the Inter-Governmental Standing Committee on Shipping, 2006).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba mwingine ni wa Makubaliano ya Kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji wa Uchukuzi wa Mizigo Ukanda wa Kati *(Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency).*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 2 Desemba, 2006, Mawaziri wanaosimamia Sekta ya Uchukuzi wa nchi za Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kongo, Tanzania na Uganda, walitia saini Mjini Dar-es-Salaam, makubaliano ya kuanzishwa Wakala wa Uwezeshaji wa Kiuchumi wa Mizigo Kanda ya Kati kupitia Bandari ya Dar-es-Salaam. Lengo la makubaliano hayo ni kuanzisha taasisi yenye Sekretarieti ya Kudumu itakayoratibu shughuli za uchukuzi na usafirishaji wa mizigo inayopita Bandari ya Dar-es-Salaam ili kuongeza ufanisi wa kiwango cha mizigo, kupunguza muda wa uchukuzi wa mizigo tangu kuingia bandarini hadi kufika mwisho wa safari na kuongeza usalama wa mizigo inayosafirishwa. Hatua hizo, zitapunguza gharama za uchukuzi na hivyo kufanya bei ya bidhaa zinazopita Ukanda wa Kati kuwa nafuu kwa watumiaji. Aidha, kwa mujibu wa ibara ya pili kifungu cha 2.5 cha makubaliano, Makao Makuu ya *TTFA* yatakuwa Dar-es-Salaam, Tanzania na kwamba, Tanzania itaingia Mkataba wa kukubali kuwa mwenyeji wa kuruhusu kuwapo kwa Ofisi za Sekretarieti ya Kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutatua tatizo la ucheleweshaji wa mizigo kwenda katika nchi hizo, Nchi Wanachama wa Ukanda wa Kati walikubaliana kuanzisha Wakala itakayosimamia uratibu wa shughuli za uchukuzi wa mizigo ya nchi hizo. Nchi hizo ziliomba msaada Benki ya Maendeleo ya Afrika ili ziwezeshwe kuanzisha taasisi hiyo. Kimsingi, *ADB* walikubali ombi hilo la ufadhili wa taasisi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu tu ya mwanzo, kwa kutoa msaada wa kuanzisha na kugharamia uendeshaji wa Sekretarieti ya Kudumu, ambapo baada ya kipindi hicho, taasisi hiyo itajiendesha yenyewe kutokana na mapato ya shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo muhimu ya makubaliano ni yale yanayotoa maelezo kuhusu kukubalika miongoni mwa nchi wanachama kwamba, Ukanda wa Kati ndio njia yenye gharama nafuu na rahisi kwa usafiri wa nchi kavu na majini; kuhakikisha kuwa Ukanda wa Kati unapatikana kwa kupitisha mizigo ya nchi wanachama kwa wakati wote kama njia rahisi kuliko zote; kufanya bidii zote kuupatia Ukanda wa Kati biashara zaidi ili kuongeza matumizi yake; kutayarisha takwimu za gharama mbalimbali za uchukuzi na taarifa za biashara; kuzikumbusha nchi wanachama juu ya hali ya miundombinu ili iwe ya kuridhisha; kuchunguza gharama za uchukuzi kwa kulinganisha na Kanda nyingine; kuwakumbusha wadau juu ya kupunguza gharama hizo iwapo zitaonekana kuwa juu zaidi; na kushirikiana na vyombo vingine vya Kimataifa vilivyo na malengo kama ya *TTFA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwakala huu uatakuwa na majukumu kama yaliyoainishwa kwenye ibara ya 23 kifungu 23(2). Majukumu hayo ni pamoja na kuratibu utekelezaji wa maamuzi ya vikao mbalimbali; kubuni na kutayarisha mikakati ya muda mfupi na mrefu; kutunza takwimu; kufanya tafiti mbalimbali za gharama za uchukuzi kupitia Bandari ya Dar-es-Salaam; kujibu hoja; maoni na ufafanuzi kuhusu gharama za uchukuzi; muda wa uchukuzi wa mizigo kwenda sehemu mbalimbali za

masoko; usalama wa mizigo na uwezekano wa kupata huduma, yaani *reliability;* kuitangaza Tanzania nje na kutunza hesabu za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za awali za uendeshaji zitatokana na msaada kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika, ambao watatoa kiasi cha dola milioni 1.5, zitakazotumika katika kipindi cha miaka mitatu ya mwanzo. Hata hivyo, kabla ya kipindi hicho kumalizika, nchi wanachama kupitia Sekretarieti ya Kudumu, zitawasilisha kwa nchi wanachama mapendekezo kuhusu upatikanaji wa fedha za kuendesha Sekretarieti hiyo baada ya kipindi hicho cha ufadhili wa *ADB* kumalizika, kwa mujibu wa ibara ya 24 ya makubaliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kujiunga na Uwakala huu, nchi yetu itapata fursa ya kuongeza kiwango cha mizigo kupitia Bandari ya Dar-es-Salaam; kuongeza mapato ya Tanzania kutokana na ada za kutumia mioundombinu na vyombo vya uchukuzi na usafirishaji; kuvutia wawekezaji mbalimbali kuwekeza hapa Tanzania; kuongeza usalama katika usafirishaji wa mizigo; kupunguza gharama za uchukuzi nchini pamoja na nchi jirani na kupunguza muda wa uchukuzi wa mizigo kutoka Bandari ya Dar-es-Salaam kwenda ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu utagharamiwa kwa msaada wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, kiasi dola milioni 1.5, sawa na kadirio la shilingi bilioni mbili kwa kipindi cha miaka miatatu ya mwanzo. Fedha hizo zitatumika kugharamia uendeshaji wa Sekretarieti ya Kudumu na kuandaa Mpango wa Biashara *(Business Plan)* ya miaka mitano. Mpango huo utaonyesha mchakato kuhusu kupatikana kwa fedha za uendeshaji kutoka kwa nchi wanachama baada ya kipindi cha ufadhili wa *ADB* kumalizika. Tanzania itagharamia Sekretarieti ya muda ya *TTFA*, inayofanya kazi kabla Sekretarieti ya Kudumu haijaanzishwa. Kiasi cha shilingi milioni 108 zitahitajika na zitatokana na michango ya wadau wa shughuli za usafirishaji wa mizigo kwenye Ukanda wa Kati. Serikali ya Tanzania, imepewa jukumu la kuratibu uanzishwaji wa Sekretarieti ya Kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa faida ya kuridhia makubaliano ya kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji wa Uchukuzi wa Mizigo Ukanda ya Kati *(Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency)* ni kubwa, Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaombwa likubali kuridhia makubaliano haya yaliyotiwa saini Mjini Dar-es-Salaam na Mawaziri wanaosimamia masuala ya uchukuzi katika nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ruanda, Tanzania na Uganda, tarehe 02 Septemba, 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba nilisome Azimio lenyewe la kuridhia Mkataba huu.

**KWA KUWA** Nchi Wanachama wa Ukanda wa Kati wa Jamhuri ya Burundi, Jamhuri ya Watu wa Kongo, Jamhuri ya Ruanda, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda, zilikubaliana kupitisha Mkataba wa Kuanzisha Wakala wa

Uwezeshaji wa Uchukuzi wa Mizigo Ukanda wa Kati na Serikali ya Muungano wa Tanzania iliweka saini mwaka huo huo wa 2006;

**NA KWA KUWA** Nchi Wanachama wanakubaliana kwamba Ukanda wa Kati ndio njia pekee yenye gharama nafuu na rahisi kwa usafiri wa nchi kavu na majini na hivyo kwa pamoja wanakubaliana kupeana haki ya kupitisha mizigo kati ya nchi zao. Aidha, wanakubaliana kwamba, kijiografia Ukanda wa Kati ndio unaoweza kuwa na gharama nafuu kati ya nchi wanachama;

**NA KWA KUWA** lengo la kuanzishwa kwa Wakala wa Uwezeshaji wa Uchukuzi wa Mizigo wa Ukanda wa Kati ni kukuza na kuimarisha matumizi ya Ukanda wa Kati kwa kuvutia wafanyabiashara mbalimbali kutumia miundombinu ya reli, barabara na Bandari ya Dar-es-Salaam katika kusafirisha mizigo inayotoka na kwenda Nchi za Maziwa Makuu;

**NA KWA KUWA** pamoja na mambo mengine Wakala wa Uwezeshaji wa Uchukuzi wa Mizigo Ukanda ya Kati utahakikisha kuwa Ukanda wa Kati unapatikana kwa ajili ya kupitisha mizigo na nchi wanachama kwa wakati wote kama njia rahisi kuliko zote, ikiwa ni pamoja na kufanya bidii zote kuupatia Ukanda wa Kati biashara zaidi, kuzikumbusha nchi wanachama juu ya hali ya miundombinu ili irekebishwe au kuendelezwa katika kiwango cha kuridhisha na kushirikiana na vyombo vingine vya Kimataifa vilivyo na malengo kama ya Wakala wa Uwezeshaji wa Ukanda wa Kati

**NA KWA KUWA** Tanzania kwa kujiunga na Wakala huu itafaidika kwa kuongeza viwango vya mizigo kupitia Bandari ya Dar-es-Salaam, kuvutia wafanyabiashara wengi kutumia bandari hiyo na hivyo kuongeza mapato ya Tanzania kutokana na ada za kutumia miundombinu, vyombo vya uchukuzi na usafirishaji na hivyo kuongeza kasi ya ukuaji wa kiuchumi na jamii na hatimaye kuvutia wawekezaji mbalimbali kuwekeza hapa nchini;

**NA KWA KUWA** katika kikao chake cha Baraza la Mawaziri cha tarehe 13 Machi, 2008 Baraza la Mawaziri liliazimia kuridhiwa kwa Mkataba wa Kuanzishwa kwa Wakala wa Uwezeshaji wa Uchukuzi wa Mizigo Ukanda wa Kati *(Agreement for the Establishment of the Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency);*

**HIVYO BASI,** kwa kuzingatia umuhimu wa Mkataba huu na manufaa ambayo Tanzania itapata kwa kuridhia, Bunge hili katika Mkutano huu wa Kumi na Moja na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, linaamua kuwa Mkataba wa Kuanzishwa Wakala wa Uwezeshaji wa Uchukuzi wa Mizigo Ukanda wa Kati *(Agreement for the Establishment of the Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency)* uridhiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Kama nilivyosema, sasa hivi nina wachangiaji watatu na bado maombi yanaletwa. Kwa hiyo, kwanza, nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyohusika na Muswada huu au muwakilishi wake. Mheshimiwa Mwananzila. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu, ninachukua fursa hii kuwasilisha maoni ya Kamati ya Miundombinu, kuhusu Mikataba ambayo ni kwa mujibu wa kifungu cha 63(3)(c) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kinachoainisha kuwa Bunge litajadili na kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano ambayo kwa masharti yake inapaswa kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuteuliwa katika Kamati mbalimbali za Bunge kwa kipindi kilichobaki cha 2008 - 2010, pamoja na wote waliochaguliwa kuwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati hizo. Aidha, ninawapongeza Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Kiteto na Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, kwa kuteuliwa na Rais kuwa Mbunge. Ninawapongeza wote kwa dhati na kuwatakia kila la heri katika kutimiza majukumu yao ya uwakilishi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, ninaomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, ambao kwa mara nyingine wamemchagua Mheshimiwa Mohamed Missanga kuwa Mwenyekiti wao kwa mara ya pili. Aidha, ninawashukuru pia kwa kumchagua Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kuwa Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu na pia kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Imani yangu ni kuwa, tutashirikiana vyema katika Kamati hii na kuleta mafanikio mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Miundombinu ilipata fursa ya kupitia Mikataba na Itifaki baada ya kuwasilishwa na Mheshimiwa Dr. Militon Makongoro Mahanga, ambaye ni Naibu Waziri wa Miundombinu mbele ya Kamati tarehe 11 Aprili, 2008. Kamati ilijadili kwa kina na kuandaa maoni na ushauri utakaosaidia kwa namna moja au nyingine kutekeleza Mikataba na makubaliano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikataba ifuatayo ilijadiliwa na Kamati:-

(i) Mkataba wa Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri wa Anga *(ICAO)* wa Mwaka 2001 kuhusu Vifaa Vinavyohamishika pamoja na Itifaki ya Mambo Maalum yahusuyo Vifaa vya Ndege ya mwaka 2001 *(The Conversion for International Interest in Mobile Equipment on Matters Specific to Aircraft Equipment of 2001).*

(ii) Itifaki ya Kurekebisha Makubaliano yaliyoanzisha Kamti ya Kudumu ya Kiserikali ya Usafiri wa Baharini ya mwaka 1987 *(Protocol Ammending the*

*Ammendment Establishing the Inter-Governmental Standing Committee on Shipping (ISCOS) of 1987.*

(iii) Mkataba wa Makubaliano ya Kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji wa Uchukuzi wa Mizigo Ukanda wa Kati *(The Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency - TTFA* wa Mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imechambua na kujadili Maazimio yaliyowasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge kama ilivyoainishwa katika nyongeza ya nane ya sehemu ya tatu ya kifungu namba 9(1)(b), Toleo la 2007. Pamoja na kwamba, Kamati imepitia na kujadili Mikataba hiyo mitatu mmoja baada ya mwingine, ninaomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Azimio la Kuridhia Mikataba au Itifaki ya Kimataifa, yote mitatu kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya jumla; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuridhia Mikataba yenye manufaa kwa Taifa letu. Kamati inaishauri Serikali kuifanyia kazi mapema Mikataba ya Kimataifa ili iwe ikiwasilishwa na kuridhiwa na Bunge lako Tukufu kwa wakati muafaka. Kuchelewa kuridhiwa kwa Mikataba hiyo, husababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa Maazimio yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, katika kuhakikisha kuwa, Mikataba hii inatekelezwa kwa ufanisi, Serikali inapaswa kuweka mazingira mazuri ikiwa ni pamoja na kupitia Sera na Sheria zilizopo ili zikidhi utekelezaji wa Mikataba hiyo. Iwapo utekelezaji wake utahitaji kuwepo kwa Sheria Mpya, Serikali iandae Miswada na kuileta ili zitungwe sheria zitakazotoa fursa ya utekelezaji wa Mikataba hiyo bila kuwepo migongano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Mikataba hii mitatu ina lengo la kuboresha Sekta ya Uchukuzi kwa nchi zilizoridhia. Ili Tanzania iweze kufaidika; ni muhimu kutumia fursa za kijiografia na rasilimali tulizonazo katika kujenga uchumi wetu. Serikali itenge bajeti ya kutosha na kuboresha miundombinu hasa barabara, reli, bandari na usafiri wa anga, ili kufungua wigo wa Ushirikiano wa Kimataifa katika uchumi na uwekezaji. Tutumie fursa za nchi jirani ambazo hazina bandari kumiliki soko la sekta ya usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Kamati inaishauri Serikali kujiandaa katika kukabiliana na majanga kwa kuhakikisha kuwa, kuna vitendea kazi na wataalam wa kutosha. Aidha, elimu ya kutosha itolewe mara kwa mara kwa wenye vyombo vya anga na majini, ikiwa ni pamoja na watumiaji wake ili kulinda vyombo vya usafiri, watumiaji na viumbe vinavyoishi majini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Kamati inaishauri Serikali kupitia wataalam wake, kuangalia Mikataba yote ya Kimataifa ambayo Tanzania bado haijaridhia, iwapo ina manufaa kwa maendeleo ya nchi hii na watu wake. Mikataba hiyo iwasilishwe Bungeni ili Bunge lako Tukufu liweze kuridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni kuhusu Mkataba wa Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri wa Anga *(ICAO),* unaohusu Vifaa Vitembeavyo, pamoja na Itifaki ya Mambo Maalum yahusuyo Vifaa vya Ndege ya mwaka 2001 *(The Conversion on International Interest in Mobile Equipments on Matters Specific to Aircrafts Equipment of 2001).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa lengo kuu la Mkataba huu ni kuimarisha usafiri duniani, kwa kuweka misingi ya kisheria na kutoa fursa kwa makampuni ya usafiri kununua vyombo vya usafiri kama vile injini za treni, mabehewa, boti, bodi za ndege, injini za ndege, vifaa vya anga za juu na kadhalika, kwa njia ya mkopo nafuu. Kamati inashauri kuwa, mashirika yetu ya usafirishaji nchini, yatumie fursa hiyo ili kuboresha huduma zao ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Usalama wa Anga Tanzania *(TCAA)* na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)*, wana jukumu la kusimamia, kuendeleza, kuboresha, kushauri na kuhakikisha kuwa, miundombinu na vifaa vya usafiri ni salama. Mamlaka hizi zinapaswa pia kuwa na wataalam wa kutosha wa teknolojia ya kisasa ili kuongeza ufanisi na kwenda na wakati. Hii itasaidia nchi kuingia katika soko la ushindani na kuwezesha Mkataba huu kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapaswa kuwahamasisha wadau wote wa usafiri wa anga; kukopa na kununua ndege mpya, zenye teknolojia za kisasa ili kuvutia wateja na kupunguza gharama za matengenezo ya mara kwa mara, kutokana na kuwa na ndege chakavu. Hii pia itasaidia kuondoa utegemezi wa dhamana kutoka Serikalini wa makampuni ya umma kama vile *ATC* na wengineo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni kuhusu Itifaki ya Kurekebisha Makubaliano yaliyoanzisha Kamati ya Kudumu ya kiserikali ya Usafiri Baharini ya Mwaka 1987 *(The Protocol Amending the Agreement Establishing the Inter-Governmental Standing Committee on Shipping (ISCOS) of 1987).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa Mikataba hii katika kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji, kutunza mazingira, kulinda viumbe na vyombo vya majini na watumiaji wake, Kamati inashauri Serikali iweke mikakati ya kuwezesha kutekelezwa kwa Maazimio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali iwe na mipango ya dhati ya kupanua na kuboresha miundombinu ya bandari na kuacha kusuasua ili shughuli za bandari zifanyike kwa ufanisi. , Kamati inaishauri Serikali kuwa, haina budi kuacha tabia ya kuminya maeneo ya bandari. Kwa mfano, suala la *NASACO,* ambapo hivi karibuni limetangazwa kwa zabuni; kulikuwa hakuna haja ya kutafuta mnunuzi au muwekezaji mwingine wakati kilio cha Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania mara zote ni kupanua eneo la kutoa huduma za bandari. Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania, hawana uwezo wa kushindana na matajiri wengine katika ununuzi wa zabuni za eneo la *NASACO.* Kamati inaitaka Serikali kuisaidia Mamlaka hiyo na kuachana na suala la kutangaza eneo la *NASACO* kwa watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusu swala la kodi; *VAT* ya huduma ya kupakia na kupakua mizigo kutoka kwenye meli *(stiff dooring),* ambayo licha ya kuongeza gharama zisizo za lazima, itaifanya Bandari ya Dar-es-Salaam kuwa na gharama kubwa kwa wenye meli. Kamati inaishauri Serikali, kuiangalia upya sheria husika ili ibadilishwe.

Kodi hiyo imekuwa ni kero, kwani hata bandari za nchi za jirani na ambazo baadhi zimeridhia Mikataba ya Itifaki tunayojadili, kwa mfano, Kenya, Uganda, pamoja na Zambia, hazina. Kodi hiyo inaweza kuitangaza Bandari ya Dar-es-Salaam vibaya na tukakosa mapato mengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuisaidia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kujiimarisha na kujiendesha katika ushindani wa kibiashara, kamati inashauri kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania, *TRA*, ambayo hutumia eneo huduma na majengo kama ofisi na ghala za mamlaka ya usimamizi wa Bandari Tanzania bila kulipia gharama zozote, Kamati inashauri uwekwe utaratibu maalum ili kuchangia gharama za uendeshaji wa *TPA* kadiri ya matumizi ya huduma hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni kuhusu Mkataba wa makubaliano ya kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji wa Uchukuzi wa Mizigo Ukanda wa Kati *(The Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency - TTFA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itafute ufumbuzi wa haraka, kuondoa matatizo ya msongamano wa mizigo katika bandari zetu, hususan Bandari ya Dar-es-Salaam. Bandari hii ya Dar-es-Salaam, ambayo ndiyo tegemeo nchini kwa hivi sasa, mizigo imeongezeka maradufu lakini ufanisi wake umeshuka, hali inayosababisha mlundikano wa mizigo na hivyo baadhi ya wafanyabiashara kupitisha mizigo katika Bandari za Mombasa, Durban na kwingineko, jambo linalochangia Serikali kupoteza mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipimo cha ufanisi wa bandari yoyote ni uwezo wa kuondoa mizigo haraka. Bandari hutegemea zaidi reli na barabara katika usafirishaji wa mizigo. Reli ya Kati ipo mahututi na barabara zetu haziridhishi. Uwezo wa reli yetu kwa mwaka 2007 wa kubeba mizigo umeshuka na ulikuwa ni asilimia saba tu ya mizigo yote iliyotolewa bandarini, ukiondoa hata *TAZARA* ambayo nayo iko *ICU.* Kamati inaitahadharisha Serikali kuwa, bila ya kuwepo kwa miundombinu ya uhakika, Maazimio haya yanayoridhiwa leo hayatakuwa na faida maana hayatatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilishawahi kupokea mapendekezo ya namna ya kusaidia kupunguza tatizo la msongamano wa mizigo bandarini. Katika mapendekezo yao yaliyowasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. *TPA* waliomba wasafirishaji wa mizigo washushie mizigo yao katika Bandari za Tanga na Mtwara na meli ndogo ziweze kusafirisha mizigo hiyo sehemu inakopaswa kwenda, lakini *TRA* hawakubaliani na mpango huu, ambapo katika usafirishaji hili ni jambo la kawaida tu. Mapendekezo hayo mbali ya kuongeza matumizi ya Bandari ya Tanga na Mtwara, yangesaidia pia kuongeza ufanisi katika Bandari ya Dar-es-Salaam. Tunaishauri Serikali ikubaliane na mpango huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ucheleweshaji mizigo bandarini, limechangiwa kwa kiasi kikubwa na ukosefu wa miundombinu ya kutosha hasa eneo la kuhifadhia makontena yanayopakuliwa melini. Ufanisi wa *TICS* umeshuka kwa chini ya asilimia 25 kwa mwaka 2007 na baadhi ya wenye meli wamepunguza safari kutoka mbili hadi moja kwa wiki, kuingia katika Bandari ya Dar-es-Salaam. Kamati inaishauri Serikali, kuimarisha miundombinu ili kuisafirisha mizigo kwa uhakika, kuondoa ukiritimba, yaani *exclusivity* ya *TICS* ambayo sasa imeshashuka katika utendaji wake na kutafuta nafasi nyingine kwa ajili ya uhifadhi wa makontena ya mizigo yanayosubiri kuchukuliwa na wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inaitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania, kupiga mnada mizigo yote iliyokaa bandarini kwa zaidi ya siku 21, lakini hili limekuwa halifanyiki kwa kuwa hata wao *TRA*, hawana sehemu ya kuhifadhia mizigo hiyo; jambo ambalo kwa namna moja au nyingine, huchangia mlundikano wa mizigo pale bandarini. Kamati inashauri kuwa, Mamlaka ya Mapato Tanzania isiliachie suala hili *TPA* peke yake, bali nao watafute sehemu ya kuhifadhia mizigo ambayo imekabidhiwa kwao kwa ajili ya kupigwa mnada.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Andrew John Chenge, Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Naibu Waziri wa Miundombinu na Mheshimiwa Maua Abeid Daftari, Naibu Waziri wa Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia, ambaye amewasilisha vizuri sana Maazimio haya, pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Miundombinu. Jambo ambalo limerahisisha sana kazi kwa Kamati ya Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, kwa kazi waliyoifanya ya kupitia na kujadili Maazimio haya na hatimaye kutoa maoni yatakayosaidia katika utekelezaji. Ninaomba niwatambue kwa majina Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mohamed H. Missanga – Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Pascal C. Degera, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Ephraim N. Madeje, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Joyce M. Masunga, Mheshimiwa Herbert J. Mtangi, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa Sigifrid S. Ng'itu, Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman Ramadhan, Mheshimiwa Profesa Philemon M. Sarungi, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi na mimi msoma taarifa - Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Kaimu Katibu wa Bunge, Dr. Thomas Kashililah, pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, ninapenda

kumshukuru Bwana James John Warburg na Bibi Justina Shauri, ambao ni Makatibu wa Kamati hii, kwa kuweza kuihudumia vyema Kamati na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maoni na ushauri huo, ninaomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ya Miundombinu, imejadili Maazimio yote na kwamba, yamezingatia mahitaji ya nchi. Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuridhia Maazimio na Mikataba hiyo kama yalivyowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja hizi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa ninamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Enhe! Mwongozo wa Spika; Kanuni gani?

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Ya 68.

**NAIBU SPIKA:** Inasema nini?

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba mwongozo wako; Kanuni ya 68, Kanuni zetu mpya zinazuia kutoa pongezi baada ya Mheshimiwa Spika au Naibu Spika kutoa pongezi, lakini kwa sasa hivi nimeona Waheshimiwa Wabunge, pamoja na Mawaziri bado wanazidi kutoa pongezi. Ninaomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninafikiri Mheshimiwa Lucy Owenya, yuko *right*, kwa sababu kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 151; salamu za pongezi na pole zimeelezwa kwa kirefu sana kwamba, endapo litatokea jambo lolote ambalo mhusika wake au mwathirika wa jambo anastahili kupewa pongezi au pole na Wabunge, basi Spika atatoa pongezi au pole kwa mhusika au kwa waathirika wa jambo hilo, kwa niaba ya Wabunge wote. Baada ya Spika kutoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo lolote kwa ajili ya kuokoa muda wa majadiliano, Mbunge yeyote hataruhusiwa kutoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo hilo wakati wowote wa majadiliano Bungeni.

Kwa upande wa Serikali, Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, atatoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo lolote kwa niaba ya Serikali. Baada ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kutoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo lolote kwa ajili ya kuokoa muda wa majadiliano; Waziri yeyote hataruhusiwa kutoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo hilo wakati wowote wa majadiliano Bungeni. Kwa hiyo, alichokisema Mheshimiwa Lucy Owenya ni kweli, Wabunge watoa hoja walikuwa wanafanya hivyo, sasa mimi nilinyamaza

kusudi nione nani anaikumbuka Kanuni hiyo. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Lucy Owenya. *(Makofi)*

Tunaendelea sasa ninawaita Kambi ya Upinzani ili watoe maoni yao kuhusu Maazimio haya.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI (K.n.y MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Pendekezo la Kuridhia Mkataba wa Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri wa Anga *(ICAO)*, linalohusu vifaa vinavyohamishika, pamoja na Itifaki ya Mambo Maalum yahusuyo Vifaa vya Ndege ya mwaka 2001 *(The Convention on Internationa Interests in Mobile Equipment and Protocol to the Convention on International Interests in Mobile Equipment on Matters Specific to Aircraft Equipment of 2001).*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa shukrani zangu kwako binafsi, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuhusu kuridhia Azimio la Mkataba wa Kimataifa wa Vifaa vinavyohamishika, pamoja na Itifaki ya Mkataba huo kuhusu Masuala Maalum yahusuyo Vifaa vya Ndege kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 53(6)(c) na kifungu cha 86(6), Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya Mikataba ya Kimataifa ya Vifaa Vinavyohamishika kwa ujumla wake ni nzuri, kwani kama tungeridhia Mkataba huo pale uliposainiwa mwaka 2001, kwa kweli matatizo ambayo tunayo sasa ya kutapeliwa na Kampuni ya *RITES*, ambayo imepewa mamlaka ya kuendesha lililokuwa Shirika letu la Reli yasingetukuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si hilo tu, kwani Mkataba huu bado una manufaa makubwa kwa nchi yetu; ukiangalia lengo kuu la Mkataba huu ninanukuu: “Kuimarisha usafiri duniani kwa kuweka misingi ya kisheria, ambayo inatoa fursa kwa makampuni ya usafiri kununua vyombo vya usafiri kama vile injini za treni na mabehewa, bodi za ndege, injini za ndege, vifaa vya anga za juu na vifaa vingine vinavyohamishika na vina thamani kubwa kwa ajili ya mkopo nafuu na bila kulazimika kuwa na dhamana.”

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na lengo hili, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, pamoja na mambo mengine, kufanya utaratibu wa kuagiza injini za vivuko mbalimbali ambavyo kwa sasa viko katika hali mbaya na muda wowote vinaweza kusababisha balaa kubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Mkataba huo, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ufafanuzi, kwa kuwa Mkataba huu ni kwa ajili ya Serikali kupata unafuu kwa vifaa tajwa au inahusu pia Makampuni ya Uwekezaji ambayo yapo hapa Tanzania nayo yanweza kupata unafuu huo huo pale wanapohitaji kununua vifaa kama hivyo. Kama hivyo ndivyo, Watanzania kwa ujumla wao kupitia kwa Serikali yao watanufaika vipi kwa udhamini ambao wanautoa kwa kampuni hiyo ya kigeni/uwekezaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya sita ya Mkataba huu inasema kuwa, kama itatokea mkanganyiko kati ya Mkataba na Itifaki kwenye ufafanuzi, tafsiri au maelezo, basi maelezo ya Itifaki ndiyo yatakayochukuliwa kuwa sahihi. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri, atueleze kati ya Mkataba na Itifaki ni kitu gani chenye nguvu kuliko kingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ibara ya saba ya Mkataba, inatoa mazingira yanayohitajika ili kufanikisha ukopaji na ukopeshaji kwa kufuata misingi ya kisheria. Kifungu (c) cha ibara hii kinachosomeka kuwa, chombo kilichowekwa rehani, ibara inaeleza masharti ya rehani kuwekwa wazi na si lazima kiasi cha fedha kwa ajili ya rehani kutajwa. Aidha, kifungu hiki kikisomwa sambamba na lengo kuu la Mkataba linalosema kuwa, ninanukuu: "... na vifaa vingine vinavyohamishika na vya thamani kubwa kwa njia ya mkopo nafuu na bila ya kulazimika kuwa na dhamana." Kambi ya Upinzani inataka ufafanuzi kwa hili, kwani maneno rehani na dhamana yana maana moja vinginevyo, ile dhana ya kusaini Mkataba huu tayari ni dhamana ambayo Serikali inatoa kwa Makampuni kuweza kununua vifaa hivyo itakuwa ni batili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya nane ya Mkataba inatoa maelezo kama mkataba kati ya mkopaji na mkopeshaji utavunjika. Utaratibu huu ni sawa na dhana nzima ya karadha ya fedha au ni ukopaji wa kawaida kwenye biashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 48 inatoa maelezo kuhusu Jumuiya ya Kikanda za Kiuchumi ambazo zimeundwa na Nchi Wanachama wa *ICAO*. Kamabi ya Upinzani inataka kuelewa kama moja kati ya nchi hizo za Ushirikiano wa Kiuchumi Kikanda haijaridhika na Mkataba huu, wanaweza kuendelea kupata manufaa yaliyomo kwenye Mkataba huu na Itafaki yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona itakuwa ni vyema kwa mujibu wa Ibara ya 53 ya Mkataba huu, itoe ufafanuzi kuwa ni Mahakama ipi na imejiandaa vipi kuiwezesha Mahakama hiyo ambayo itashughulikia masuala yote yaliyotajwa katika Mkataba huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Itifaki ya Mkataba huu ambayo imejikita katika ndege na vifaa vyake, kwa ujumla wake ni lenye manufaa kwa nchi yetu kwa kutilia maanani kuwa, sasa Shirika letu la Ndege limerudi kuwa chini ya umiliki wa Serikali. Kambi ya Upinzani inaiasa Serikali kutumia fursa iliyopo katika Mkataba na Itifaki hii kuhakikisha mashirika yetu yanarudi katika hali upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba Ulioanzisha Kamati ya Kudumu ya Kiserikali ya Usafiri wa Baharini ya Mwaka 2006 *(Protocol Amending the Agreement Establishing the Inter-Governmental Standing Committee on Shipping (ISCOS), 2006).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa *ISCOS* ni wenye manufaa kwa nchi yetu kulingana na maudhui ya Mkataba wenyewe. Ni kweli uliowazi kuwa, Tanzania kama

tungekuwa na sera zenye vipaumbele, kwa sasa nchi yetu ingekuwa ni nchi ya kuigwa na wenzetu kutokana na fursa tunazozipata na kuzichezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mazuri yaliyomo kwenye Mkabata huo wa *ISCOS* na nyongeza ya majukumu kwenye Itifaki ya 2006, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe ufafanuzi ni kwa jinsi gani Chuo cha Usafiri Majini *(Maritime Institute)*, kinavyotumika kuinufaisha nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaamini kabisa faida ambazo zimeelezwa katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuwa ni faida kusaini Mkataba wa *ISCOS*. Tunadhani sisi kama nchi, kushindwa kuendesha majadiliano na wamiliki wa vyombo vya usafirishaji majini ni kutokana na kutokuwatumia vyema, wataalam wetu walioko kwenye Chuo cha *Maritime*. Aidha, Tanzania tumekuwa tukikosa stahiki yetu ya msingi toka kwa wenye vyombo vya usafiri baharini (meli), kutokana na watendaji kutokuwa na ujuzi wa kutosha katika sekta hii *(Maritime Transaction).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ina mashaka juu ya uwezo wetu kiutendaji katika kuhakikisha kuwa, manufaa yote yaliyoelezwa katika Mkataba na Itifaki yake nchi yetu itayapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, Itifaki hii inaweza kutafsiriwa kuwa ni upungufu kwa upande wa Serikali yetu kukosa chombo ambacho kinatakiwa kuwa kama mkaguzi kati ya Serikali, Wakala wa Meli *(Shipping Agents)* na wanaotuma mizigo *(consignee).* Tanzania tumepata unafuu mkubwa wa kushuka kwa viwango vya ushuru kutokana na matokeo ya kusaini Itifaki ya *ISCOS*. Tunaomba ufafanuzi juu ya viwango vya ushuru kulingana na Sheria za Kimataifa vikoje au Mashirika ya Kimataifa ya Meli yanajipangia viwango vyao kulingana na nchi wanazopeleka meli zao bila ya kufuata viwango vilivyopo Kimataifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa, Tanzania bado iko kwenye upande wa kunufaika zaidi kama itapanua na kuboresha huduma za bandari na usafirishaji kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji wa Uchukuzi wa Mizigo Ukanda wa Kati *(Agreement for Establishment of the Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency (TTFA) of 2006).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo hapo mwanzoni nilidokeza katika Mikataba mingine ya Kimataifa ambayo Tanzania imesaini, lakini imeshindikana kufanya kazi na hii inatokana na matatizo ya kisera zaidi kuliko ya kiufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaishia Serikali kutobweteka na hivyo kujua mazingira halisi ya kiuchumi wa nchi yetu tuliyonayo, mpaka ikafikia nchi nyingine kutuonyesha fursa za uchumi tulizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili halitakuwa na faida kwa nchi yetu kama miundombinu yetu ya reli hatutoiboresha ili iendane kweli na hali halisi iliyopo katika

karne ya sasa.  Nchi waanzilishi wa Wakala hii, tayari wanaonyesha kuwa biashara sio tatizo kwani Nchi kama *DRC* wana uhakika wa kupitisha tani nyingi za shaba na *copper* ambayo inazalishwa kwao, pamoja na kuagiza toka nje ya nchi, bidhaa nyingi za kuendeshea uchumi wao.  Rwanda na Burundi wana uhakika wa kupitisha mazao yao wanayozalisha kwenda nje na pia bidhaa nyingi watakazoagiza toka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona Tanzania kama mwanachama na nguzo kuu katika biashara hii, bado ina tatizo kubwa kuanzia kwenye utendaji wa kupakia na kupakua mizigo bandarini hadi kwenye usafirishaji mizigo hiyo mpaka kumfikia mwenye mizigo.  Hili si tatizo hilo tu la miundombinu ya bandari na reli, bali hata kwenye utendaji wa taasisi zinazotoa vibali kwa ajili ya mizigo husika, kulipiwa ushuru stahiki nazo ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia manufaa ambayo nchi yetu itayapa, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kwanza ifanye maandalizi ya kutosha kukabiliana na biashara kubwa kutoka nchi wanachama, pamoja na kuweka mazingira mazuri pale Mgodi wa Kabanga Nikel uliopo Ngara, utakapoanza uzalishaji wake.  Vinginevyo, Tanzania itajikuta ni nchi ya kulipa fidia kwa hasara ya ucheleweshaji wa mizigo kutoka na kuingia kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya upinzani, hatuna pingamizi na uridhiwaji wa Maazimio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.   *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:**  Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge.  Tunao wachangiaji wafuatao sasa nitamwita wa kwanza Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Juma Njwayo na wengine nitawataja baadaye.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:**  Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii muhimu ili na mimi niweze kuchangia katika kuangalia jinsi tutakavyopitisha kuridhia Maazimio haya manne.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kusema kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu na  hivyo, nimeshiriki pamoja na wenzangu katika kutoa yale ambayo yamewakilishwa hivi sasa na mwakilishi ambaye ninamshukuru sana kwamba, amejitahidi kweli kweli katika kuelezea yale tuliyokubaliana; Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, tunamshukuru sana kwa kutuwakilisha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia kidogo tu Maamzimio mawili kati ya hayo manne; nitazungumzia Azimio la Kuridhia Itifaki ya Mkataba Kuhusu Masuala Maalum yahusuyo Vifaa vya Ndege lakini vilevile nitazungumzia kwa kifupi kidogo, kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa kwa Wakala wa Uwekezaji wa Ushuru wa Mizigo Ukanda wa Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama kwa makini lengo la Itifaki hizi, kwa mfano, hii ya kwanza ambayo ninaanza kuizungumzia, lengo lake kubwa ni kuimarisha usafiri duniani kwa kuweka misingi ya kisheria, ambayo inatoa fursa kwa makampuni ya usafiri kununua vyombo vya usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo peke yake linatufungulia milango nchi kama Tanzania, kuweza kupata fursa nzuri ambazo zitawezesha mashirika yetu ya usafirishaji, kuweza kupata fedha kwa ajili ya kununulia vifaa kwa shughuli za usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kusema kwamba, hii ni fursa nyingine tena; hivi karibuni Bunge lako Tukufu lilijadili Muswada wa *Financial Laws*, ambao vilevile unatoa fursa kuwezesha baadhi ya Watanzania wenye nia ya kutaka kukopa vifaa kwa ajili ya shughuli za biashara au huduma, kuweza kupata fursa ya kukopeshwa vifaa hivyo. Hii ya pili ya Itifaki ni fursa nyingine kubwa zaidi kwanza, inaelekeza uwezekano wa makampuni ya Kitanzania yaliyoko hapa nchini, yaani usafirishaji wa ndege kuweza kupata fedha kwa ajili ya kununua injini za ndege, bodi za ndege na vifaa vingine mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, fursa kama hii zimekuwa zikitolewa duniani kwa nchi ambazo zimeingia Mikataba na kuridhia Itifaki hizi. Kwa hiyo ni nafasi ya pekee kwa nchi kama Tanzania, kutumia fursa hizi ili tuweze kuboresha usafiri wa anga hapa Tanzania. Katika Bara la Afrika, nchi kama Afrika ya Kusini, Ethiopia na Kenya; mashirika yao ya ndege yamenufaika na mpango kama huu na kama mtakavyoona, haya ndiyo mashirika ambayo yanaongoza katika ufanisi wa uendeshaji wa shughuli za anga katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusichelewe basi kutumia fursa hizi ili tuweze kuona kama shirika letu la Ndege *(ATCL)*, nalo linaweza kutumia fursa hizi likaboresha usafiri wa anga hapa nchini. Tukitazama aina za ndege tulizokuwa nazo katika shirika letu la anga wakati tunazungumzia -200, - 300, hayo mashirika niliyoyataja yako mbali sana – 800; ndege za kisasa katika mazingira ya sasa. Kwa hiyo ni vizuri tukazitumia fursa hizo, lakini fursa hii vilevile inatusaidia ipo Mikataba mingine ndani ya Itifaki hiyo ambayo inawezesha vilevile kuwa na mpango wa kuweza kununua sio vya ndege tu, lakini vilevile injini za treni, mabehewa na kadhalika. Kwa hiyo ni vizuri tukaridhia Itifaki hizi na tukaingia katika Mikataba hiyo ili tuweze kusaidia kuboresha shughuli za usafirishaji hapa nchi.

Shirika letu la Reli liko katika matatizo makubwa sana, lakini tukitumia fursa hizi vizuri ni dhahiri kwamba, Shirika lile kwa vile Serikali ina hisa, basi wawekezaji na Serikali kwa pamoja, inawezekana kabisa tukapata nafasi kwa Mikataba inayofanana na hii ndani ya Itifaki zenyewe, tukaweza kupata uwezo wa kuboresha Shirika la Reli la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia kidogo kwenye kuridhia Mkataba wa Kuanzishia Wakala wa Uwezeshaji wa Uchukuzi wa Mizigo Ukanda wa Kati.

Ukitazama Mkataba wenyewe, unazihusu nchi za Ruanda, Burundi, Uganda, DRC Kongo na Tanzania; Kenya haipo katika mpango huu kwa sababu ina bandari yake ya Mombasa. Inawezekana kabisa Kenya vilevile ikawa ina Mikataba mingine inayofanana na hii kwa ajili ya kuzihudumia nchi nilizozitaja. Hii ni fursa kwetu tena ni fursa ambayo kwa kiasi kikubwa, inatiliwa mkazo sana na hizi nchi nyingine nilizozitaja zaidi ya Tanzania, ambayo ndiyo mwenyeji na mwenye bandari. Kama Ruanda wanasema tuwe na wakala, Burundi wanasema tupo tayari kwa wakala, Uganda wanasema wako tayari kwa uwakala huo, DRC Kongo wanasema wako tayari kwa uwakala huo; sisi Tanzania tunangoja nini?

Wenzetu hawa wanasema hivyo kwa sababu wanaamini kwamba, Bandari ya Tanzania na usafiri wa Reli ya Kati na barabara zetu, kwao ndiyo usafiri wa gharama nafuu kuliko kupitisha mizigo mahali pengine au katika bandari nyingine hapa duniani. *(Makofi)*

Kama hivyo ndivyo, Watanzania tunasubiri nini; wenzetu wameanza wanatuambia Watanzania amkeni tuingie Mkataba wa pamoja tuweze kuboresha shughuli hizi za uchukuzi wa mizigo? Nina uhakika kwa kuwa na chombo kimoja kinachosimamiwa na nchi zaidi ya tano, hiyo tena kwa Watanzania ni fursa nyingine kubwa itakayotuwezesha kuwa na sauti kubwa ya kuweza kupata mikopo kwa ajili ya kuboresha barabara zetu, reli na kwa ajili ya kuboresha mfumo mzima wa bandari ili kuwezesha mizigo kupita kwa haraka na kutoa huduma kwa ufanisi mkubwa katika nchi hizi zilizo *land locked countries* ambazo ni Ruanda, Burundi, Uganda na kadhalika.

Vilevile ni fursa ambayo sisi Watanzania kama tutaitumia vizuri, itaweza sana kutusaidia katika mawazo ambayo tulikuwa nayo mwanzo kati ya Tanzania na Uganda ya kufungua au kujenga reli ya kutoka Tanga hadi Musoma. Hii ni fursa ambayo iko wazi; mawazo tumekuwa nayo, Uganda imekuwa iko tayari kuingia katika mpango huo wa ujenzi wa reli inayoonekana kama sisi Watanzania bado fursa hizo tunazifumbia macho, hatujaweza kuzitumia vizuri; Watanzania tuamke sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si Reli hiyo ya Tanga kwenda Musoma tu lakini sasa hivi tuna mpango wa reli ya kutoka Isaka kuelekea huko Ruanda na nchi za Burundi. Hii tena ni fursa itakayokuwa inashirikisha nchi zaidi ya tatu; ni rahisi katika Vyombo vya Kimataifa kuweza kupata mikopo ya kuendeleza ujenzi au kuanza ujenzi wa reli hiyo ya Isaka kuelekea katika nchi hizo za Ruanda na Burundi. Tutumie fursa hiyo Watanzania; ni fursa bora sana itakayotusaidia. Inawezekana vilevile Itifaki hii ikatoa fursa katika vyombo vingine vya majini, maana yake ni kwamba, tutaweza vilevile kushirikiana na nchi kama *DRC* ili kuboresha muunganisho wa usafiri wa maji katika Ziwa Nyasa ili kuhakikisha mizigo ya *DRC* inafika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niongeze haya machache, kwa sababu haingekuwa imewezekana katika ripoti yetu ya muda mfupi, tuweze kusema yote tuliyokuwa tumeyazungumza ndani ya Kamati.

Kwa hiyo, ninaomba niseme kwamba, ninaunga mkono Itifaki zote nne na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tuziridhie ili fursa hizi ziweze kuwa wazi kwa

vyombo vyetu, mashirika yetu na nchi yetu. Tuweze kutumia na kuboresha usafiri wa anga, maji, reli na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia Itifaki iliyo mbele yetu ili tuweze kuridhia. Kwa kiasi kikubwa ninasisitiza tu yale ambayo wasemaji waliotangulia wamekwisha yasema, lakini nitatumia njia nyingine ya kuonyesha umuhimu wa sisi kuridhia Itifaki zilizo mbele yetu jioni hii, hususan ile ya kuanzisha Wakala wa Usafirishaji na Uchukuzi wa Mizigo katika Ukanda wa Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tarakimu tulizonazo, kufikia Desemba mwaka 2007, nchi yetu ili-*export* bidhaa na huduma zenye thamani ya takribani dola bilioni 3.7, lakini tuli-*import* bidhaa zenye thamani ya takribani dola bilioni 6.3. Kwa hiyo, kwa mwaka huo tulikuwa na nakisi katika akaunti yetu ya kawaida *(Current Account)*, iliyofikia kiasi cha dola bilioni mbili. Katika *exports* zetu zile za dola bilioni tatu ndani yake, *service sector* ili-*account for* dola bilioni 1.6 na katika hizo dola bilioni 1.6; sehemu kubwa ilitokana na utalii na sehemu ndogo iliyobakia ilitokana na *transit trade*. Ninachotaka kusema ni kwamba, ukichukulia reli peke yake katika mwaka wa 2007, ilibeba mizigo yenye uzito wa kati ya tani 500,000 na 700,000, lakini mizigo inayokwenda kutoka nchi za jirani ambayo iko tayari kupitia Tanzania kwa kutumia reli zetu na barabara zetu, hususan reli yetu tunazungumzia tani zisizopungua milioni nne.

Tuna mzigo ambao uko tayari kubebwa wa tani milioni nne na zaidi; reli yetu pamoja na bandari zimepitisha mizigo kati ya tani 500,000 na 700,000. Inasikitisha, maana yake hii ni fursa iliyo wazi kabisa kwa nchi kutengeneza pesa za kigeni kwa kutumia nafasi ya kijiografia, haina ubishi. Sasa kwa nini hatuitumii fursa hii? Ni matatizo yetu ya kutokuwa au kuona na kuelekeza matumizi yetu ya fedha chache tulizonazo katika maeneo ambayo yatainua uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naib Spika, nchi hii sasa hivi tunazungumzia kasi ya ukuaji wa *GDP* ya takriban asilimia 7.3, asilimia 7.2, asilimia 6.9. Katika vikao vya nyuma nilikwishazungumza kwamba, hiyo sio *gross rate* ambayo itaondoa umaskini kwenye nchi hii; tunahitaji kasi ya ukuaji wa *GDP* isiyopungua asilimia kumi; je, tutafikaje hapo? Nimekwishaonyesha fursa hii tuwekeze kwenye miundombinu hususan bandari, reli na barabara zetu. *(Makofi)*

Sasa Itifaki iliyo mbele yetu inatuambia hivyo; Mungu ametujalia tuna bandari; kuna nchi zimefungwa hazina njia ya kufika huko isipokuwa wapitie Tanzania. Watanzania wenyewe tumelala usingizi tena fofo; tunatakiwa tuamke.

Tukiamka tukipeleka mizigo hii tani milioni nne, tayari tunaongeza pato la fedha za kigeni na nakisi niliyokuwa ninaisema hapa itapungua sana na matokeo ya kupungua kwa nakisi hii, yatakuwa ni mazuri hata kwenye *exchange rate* yetu, kwa sababu

*exchange rate* yetu tunapata matatizo, kwa sababu *we import more than we export*. *(Makofi)*

Eneo la kuweza ku-*export* haraka ni la *transit trade; geographical location* ya nchi hii tuitumie vizuri halafu hii Itifaki ya ku-*facilitate* kubeba mizigo katika Ukanda wa Kati. Kwa maana hiyo na kwa tarakimu hizi nilizozisema hapa, mimi binafsi ninaunga mkono Itifaki hii, tuiridhie haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Sasa suala lingine ambalo ninajiuliza ni kwamba, Itifaki hizi zilitiwa saini toka tarehe 22 Septemba, 2006; leo tarehe 17 Aprili, 2008; zilikuwa wapi siku zote hizi? Kwa hiyo, ninasikitika kwamba, tumecheleweshа sana kuzileta mbele ya Bunge hili ili tuweze kuziridhia kwa sababu ni Itifaki muhimu sana kwa uchumi wetu.

Umuhimu wa *transit trade* na Reli yetu ya Kati na jinsi ambavyo hatuko tayari kuitumia kwa manufaa ya nchi hii, ulionyeshwa hivi karibuni miezi miwili au mitatu ya nyuma wakati wenzetu wa Kenya walipokuwa na matatizo ya Kisiasa, Bandari ya Mombasa ikawa haipitiki, ndugu zetu katika *land locked countries* wakawa wamekwama vibaya sana. *The alternative route* ilikuwa ni Tanzania; je, tulichukua *advantage* hiyo?

Jawabu ni kwamba, hatukuchukua; hatukuitumia hiyo faida, hatukuitumia hiyo fursa ya kwamba mizigo Kenya haipiti na *alternative route* ni Tanzania, hatuna mabehewa na reli yetu ni mbovu, hatuna *engine*, Barabara zetu hazipitiki ili mradi matatizo juu ya matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya kusema hayo na kwa dhati kabisa, ninajaribu kuionyesha Serikali, tunaweza tukaongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wetu, tunaweza tukaongeza mapato ya fedha za kigeni ya nchi yetu, kwa kutumia *service sector* na hususan *transit trade* kwa maana ya kutia saini Itifaki hii ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia na ninaunga mkono hoja iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii ili niweze kuchangia kutokana na Maazimio yaliyo mbele yetu.

Kwanza kabisa, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwasilisha vizuri Maazimio ya Mikataba, lakini pia ninapenda kuipongeza Kamati ya Miundombinu kwa kutoa taarifa nzuri, inayoitaka Serikali kuandaa mazingira bora ya miundombinu ya bandari nchini, ikiwa ni pamoja na ufumbuzi wa haraka wa misongamano iliyoko katika Bandari yetu ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Awali ya yote, niseme ninaunga mkono Maazimio yote manne. Sina tatizo na hilo na ninajua hii Mikataba imekuja hapa kwa ajili ya kuhakikisha nchi yetu inajenga uchumi imara na wa kisasa, kwa hiyo, ninaunga mkono hoja kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia nita-*concentrate* sehemu moja tu ile inayohusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji wa

Uchukuzi wa Mizigo Ukanda wa Kati. Ninachangia nikiwa na wasiwasi kwa sababu nikiangalia aya ya tatu na ya tano ya Azimio hilo, kunaonekana kutajwatajwa zaidi Bandari ya Dar es Salaam. Sasa ninakuwa na wasiwasi kwamba, tunaweza tukawaangusha wenzetu wale tunaoingia nao Mikataba hii. Huu ni ukweli ulio wazi kwamba, sasa Bandari ya Dar es Salaam imezidiwa; kuzidiwa huko kunaweza kukazaa mambo mengi sana na tukaonekana Watanzania kuwa wababaishaji. Katika hali hiyo basi ni ombi langu kwamba, tuamue kuangalia Bandari nyingine zilizoko hapa nchini na hasa Bandari ya Mtwara. *(Makofi)*

Mzee wangu, Mzee Mwinyi aliwahi kutamka mahali fulani kwamba, bandari zetu ni sawasawa na migodi ya dhahabu. Je, kama migodi ya dhahabu tunayo kwa nini tusiitumie? Bandari ile ni nzuri na kutoka Durban mpaka Djibouti, ndiyo bandari bora yenye kina kikubwa na bandari iliyo maridhawa lakini tunaiacha tu, inashangaza! Hivi tatizo ni nini au kwa sababu ziko Mtwara? Kwenye mambo ya *public interest*, iwe mahali popote; Tanga, Zanzibar na hata Mtwara ni kwa manufaa ya umma. Ninafikiri tuiangalie bandari hii, tunaicha bandari iliyo nzuri na ya kisasa na tunai-*under utilize* bila sababu za msingi. *(Makofi)*

Ninaiomba Serikali na kama nilivyotangulia kusema, tunaweza tukawaangusha wenzetu wale kwa sababu tu ya mikakati yetu isiyo imara. Wakati sasa umefika, twende Mtwara na lazima tukubali ukweli kwamba, Bandari ya Dar es Salaam imejaa na hatuna namna ya kuendelea kuipanua bandari ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 8 Aprili, 2008, wakati tunaanza Bunge hapa, nilikuwa na swali linalohusu Bandari hiyo hiyo ya Mtwara. Nilipouliza maswali ya nyongeza mawili juu ya kuwepo kwa Kampuni ya *Hemerets Shipping Line*, ambayo ipo tayari kufanya *transhipment* kwenda maeneo ya nchi; niliambiwa na Naibu Waziri aliyejibu swali leo, alikuwa kinara sana hapa Bungeni kwamba, hapana unafanywa utafiti. Ninashangaa ni utafiti gani mnaoutaka; kama mtu tayari yupo ana-*facilities* zote za kwenda ku-*invest* pale unasema unafanya utafiti; utafiti gani?

*TPA* na *TRA* mkae muangalia tena hilo, kama *TRA* ipo maana ninasikia minong'ono hapa kwamba, tukipeleka kule mapato hayapatikana ya kutosha; kwa nini yasipatikane? Kwa sababu kama Bandari ipo, vifaa vipo na watu wanaotaka kupitisha mizigo pale wapo; kwa nini *TRA* isiongeze ukubwa au idadi ya wafanyakazi; kuna jambo gani? Hii inatufanya wananchi wetu pale wafikiri mara mbilimbili, inaleta maswali mengi sana. Ninafikiri kwa Serikali, wakati umefika tuzitumie bandari zetu za Mtwara, Tanga, Lindi, Zanzibar na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na ndugu zangu, jambo lingine ni kwamba, tulifanya makosa huko nyuma, tuliondoa mataruma ya reli inayotoka Mtwara hadi Nachingwea. Yale yalikuwa ni makosa makubwa, lakini yaliyopita si ndwele tugange yajayo. Tuta lile bado lipo, kilichoondoka pale ni mataruma, kwa hiyo, tununue mataruma tuyaweke pale tuyafikishe mpaka Makambako tuungane na maeneo mengine tuongeze uchumi wetu. Bandari ipo inakaa tu, tukiongeza mataruma hayo hakuna tatizo, tutasogeza uchumi.

Nia yetu ni nzuri, ninasema kama mwakilishi wa wana-Mtwara na kama mwakilishi wa Tandahimba. Ninajua namna gani bandari ile itakavyoleta uchumi si wa Mtwara tu bali ni wa Taifa lote. Kwa hiyo, turudishe ile reli, tukitengeneza mazingira mazuri jambo hili ni la miezi miwili au mitatu mambo yatarudi pale pale.

Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ifanye jitihada za kutosha ili mataruma yale yarudi pale, tujenge uchumi wetu imara na wa kisasa kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza pia uwezekano wa kutengeneza mazingira ya kutosha kuanzia Mtwara hadi Mbambabay pia. Kwa sababu mazingira yale ninayosema ya kuboresha bandari hiyo yakitengenezwa vizuri yakafika Mbambabay, basi tuta-*attract* wenzetu wa Malawi, Zambia na hata Zimbabwe kutuunga mkono na kushirikiana nao. Kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali tulifikirie hii na lisiwe la kuchukua muda mrefu, bali liwe la dharura, bandari kwa Tanzania ndiyo namna moja iliyo nzuri ya kutusaidia kujenga uchumi wetu na ulio imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia kwenye hili suala la *Central Corridor Transit Transport*, tuangalie namna tunavyoweza ku-*accommodate* mpango mwingine kama huu utakaoitwa *Mtwara Corridor Transit Transport Facilitation Agency*, ukate nchi za Malawi, Msumbiji na ikiwezekana Zimbabwe na Zambia. *(Makofi)*

Kama Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga alivyosema, vifaa na bidhaa zinazosafirishwa kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda kwa wenzetu kule, baadhi ya maeneo ya Maziwa Makuu kwa sababu zina faida na zinachangia uchumiwa nchi yetu, tukitengeneza mazingira kama hayo, yakaitwa *Mtwara Corridor Transport* yatasaidia sana. Tutakuwa tumetengeneza mazingira ya watu kutoangalia maeneo mengine; ni suala la kujenga tu mazingira imara na bora. Jambo hili litasaidia kama ilivyo *Central Corridor*, walete na *Mtwara Corridor* ijenge uchumi wetu kwa urahisi na kwa wepesi.

Makampuni yapo kama nilivyosema *Hemerets Shipping Line* na yapo mengine, tukifungua tu mazingira yatakuja, wala hakuna sababu ya kuwa na wasiwasi lakini kwa kucheleachelea, jamani tunachelewa pasipo sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo jioni hii na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wewe hodari hata zilipozima taa uliendelea tu kusema. Tunaendelea na msemaji mwingine, ninadhani tunaweza kumfikia Mheshimiwa Godfrey W. Zambi na Mheshimiwa Mohamed Said Sinani.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kupata nafasi ili niweze kuchangia kuhusu Mikataba na Itifaki ambayo imewasilishwa mbele ya Bunge lako jioni ya leo.

Nninaomba pia niseme kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu na kwa hakika nilishiriki sana katika kuchangia yale ambayo yamesomwa na Mwakilishi wa Kamati, Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila. Ninachofanya ni kujaribu kuongezea machache au kuweka tu msisitizo kwenye yale mengine ambayo yamekwisha kuzungumzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokutana sisi kama Kamati, tulimwambia Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, tumechelewa sana kuletewa Mikataba hii. Amezungumza Mheshimiwa Kaboyonga kwamba, kuna takriban miaka miwili tangu ilipotiwa saini, lakini leo ndiyo tunaletewa kwenye Kamati na sisi pia tulizungumza kwamba, imechukua muda mrefu sana ukilinganisha na umuhimu wa Mikataba au Itifaki zenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninaomba nichangie ule Mkataba wa *ISCOS.* Mkataba kwa sehemu kubwa, unazungumzia masuala ya usalama baharini. Ninaomba niishauri Serikali, kwa sababu tunaridhia Mkataba huu, nina hakika Bunge lako Tukufu litaridhia kwa sababu ya umuhimu wake. Tunataka tusisitize usalama wa meli baharini, yaani vyombo vinavyokwenda baharini, tumekuwa tunapata mabalaa mengi sana kwenye vyombo vinavyokwenda baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme kwamba, tukipe nguvu chombo ambacho kwetu sisi tumekiunda kusimamia usafiri wa majini, pamoja na ule wa nchi kavu *(SUMATRA).* Tuwape nguvu zaidi ili waweze kuwa na vifaa vya kutosha kwa ajili ya kufuatilia vyombo hasa vinavyokwenda majini, kwa nchi kavu pengine siyo matatizo. Kwa vyombo ambavyo vinakwenda majini wanaweza kutusaidia sana pengine kuvishika hata vyombo ambavyo vitakuwa vinakiuka taratibu zile ambazo zinapaswa zifuatwe, pamoja na kuhakikiaha kwamba, meli hizo zina vifaa vinavyostahili lakini pia na usalama au uimara wa vyombo vyenyewe ili viweze kwenda vizuri na kwa usalama zaidi baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie kwa kifupi sana Mkataba mwingine wa *TTFA.* Mkataba huu pengine ndiyo unaoonekana wa muhimu sana, kwa sababu unahusu usafirishaji katika huu Ukanda wa Kati. Wenzangu wameshazungumza na mimi ninaomba hili nilisisitize sana kwamba, nilihoji hata kwenye Kamati, pamoja na kwamba, Mheshimiwa Waziri alitoa ufafanuzi kwamba; pamoja na kupitisha Mkataba huu, lakini kama hatuwezi kuiimarisha Bandari yetu ya Dar es Salaam, tutakuwa hatujafanya kitu chochote. Kama hatuwezi kuhakikisha kwamba, hatuwezi kutumia Bandari ya Mtwara kama msemaji wa mwisho alivyosema, tutakuwa hatujafanya kitu chochote. Kama hatuwezi kuhakikisha kwamba hatuwezi kutumia Bandari ya Tanga na bandari nyingine, tutakuwa hatujafanya kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyosema wenzangu, ilishazungumzwa kwamba, eti mizigo ikienda Mtwara kule itaibiwa na watu watakwepa kodi. Sisi tukashanga sana kwamba, hivi *TRA* wanachagua wapi kwa kufanya kazi? Wanajua kabisa tatizo lililopo Dar es Salaam; watachaguaje mahali pa kufanya kazi na vinginevyo tujiulize hivi tulijenga bandari za nini kule Tanga na Mtwara na maeneo mengine?

Ninaomba niishauri Wizara na Serikali kwamba, tuanze kuitumia Bandari ya Mtwara mara moja, tuanze kutumia Bandari ikiwezekana ya Lindi kama inafaa mara moja, tuanze kutumia Bandari ya Tanga mara moja na kwa umakini zaidi. Pia pale Bagamoyo panafaa zaidi na zaidi kuanza kupatumia haraka iwezekanavyo, kwa sababu ni jirani zaidi na Dar es Salaam, kwa hiyo, mizigo inaweza ikawa inatoka mara moja na kwenda kwa watumiaji au kwenda nchi nyingine bila kupoteza muda mwingi. Kwa hiyo, ninaomba hili lisiwe la kuchelewa na ninadhani kama Bunge, tuiagize Serikali kwa kweli kwa mujibu wa Katiba, inze mara moja kutumia bandari hizi hasa za Mtwara na Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, Bandari ya Dar es Salaam haifai sasa hivi imejaa. Watu sasa hivi wanasita kuanza kuitumia Bandari ya Dar es Salaam na Kampuni ya *TICS* tumekutana nayo juzi imekiri kwamba, jamani ikifika mwezi wa sita tunaweza kabisa tukashindwa kuendelea pale kutoa mizigo kwa wateja; wamekiri kabisa mbele ya Kamati. Kwa hiyo, wanahitaji na wao *intervention* ya Serikali. Sasa ukija hapa Bandari wanalia, Serikali inalia na *TICS* wanalia; hivi twende wapi? Ukienda Serikalini; Serikali inalia, Bandari wanalia na *TICS* wanalia; sasa tufanye nini sisi Wabunge?

Ninadhani kama Wabunge, tunaishauri Serikali kwa nguvu kabisa ihakikishe kwamba, haya matatizo yanatoka mara moja na tusiendelee kupoteza pato ambalo sasa hivi tunalipoteza kwa sehemu kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie kidogo suala la ununuzi wa vifaa vya ndege, pamoja na vifaa kama injini za treni na kadhalika. Wenzangu wamezungumza lakini mimi ninasema tutumie nafasi hiyo kwa ukamilifu sana. Reli zetu kama walivyosema wenzangu, ziko taabani. Tumepata fursa ya kwamba, sasa mashirika haya yanaweza yakakopa kwa urahisi zaidi bila kulazimika kuwa na dhamana, lakini pia wakapata mikopo hii kwa riba nafuu zaidi. Kwa hiyo, ninaomba tutumie nafasi hiyo, tulifufue shirika letu la ndege; tuwe na shirika ambalo tunaweza tukaliita shirika la ndege la nchi siyo mfano wa shirika la ndege. Maana yake ninadhani tuna mfano wa shirika la ndege, lakini siyo shirika la ndege ambalo lina hadhi kuitangaza nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuhakikishe tunatumia hiyo nafasi ili tuweze kukopa vifaa hivyo na kwa maana hiyo, mashirika yetu yaweze kufanya kazi bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumze jambo lingine kwa ufupi sana; tumeanzisha huu Uwakala, yaani *TTFA*, ninaomba tu nirudi nyuma pale, tumeanzisha *TTFA* na makao yake yanakuwa Dar es Salaam, ninaomba nipongeze kwamba Wakala huu utakuwa na Makao Makuu katika nchi yetu.

Makao Makuu kuwa Tanzania, maana yake tutakuwa tunapata pia faida kubwa sana; kuna ajira ambazo siyo lazima waajiriwa watoke nchi nyingine, unaweza kuwa na wahudumu, madereva na kadhalika, hawa wanatoka kwetu kwa hiyo ni faida kubwa sana kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nilisikitika kidogo na kadri Naibu Waziri leo alivyokuwa anasoma kwamba, pesa ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuanzishia *agency* hii ni dola milioni 1.5 na pesa hizi tumezipata kama mkopo kutoka Benki ya Afrika *(ADB).* Sasa hapa najiuliza; iko wapi dhamira halisi ya Serikali na *seriousness* ya Serikali; kwa sababu tunaanzisha Wakala kwa mkopo kutoka Benki ya Afrika, sisi hatuna pesa zetu wenyewe?

Ninaziomba Serikali zote ambazo ni wanachama na ambao wanaridhia Mkataba huu, tuhakikishe kwamba, tunajipanga sawasawa, maana yake tunaweza tukafika hii benki ikasema kwamba, pengine hatuwezi kutoa pesa hizi kwa utaratibu huo.

Wengi ni mashahidi, humu ndani tumekuwa tukisubiri pesa wakati mwingine tunapangia miradi yetu pesa ambazo hatujazipata na tumeona miradi mingi imeathirika kwa sababu tulitegemea zaidi mikopo na wale ambao walitegemea watupe baadaye wanasema hatutatoa, kwa sababu pengine ya matatizo haya au kwa sababu mmeshindwa kutimiza vigezo vya aina fulani.

Kwa hiyo, ninafikiri ili kuepukana na hayo, basi hizi nchi zionyeshe *commitment* ili tuhakikishe kwamba, hatukwami katika kuendesha Wakala wenyewe, maana yake inaweza ikawa aibu, tumeanzisha chombo kizuri lakini kinakwama kwa sababu nchi zenyewe hazikujiandaa zilitegemea misaada kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tena ninashukuru kwamba, umenipa nafasi na mengi ambayo nilikuwa nizungumze wenzangu wameshazungumza, lakini pia nilipata nafasi ya kuchangia kwenye Kamati.

Niseme tu kwamba, kwa sababu ya umuhimu wa Mikataba hii, basi ninaomba Bunge liliridhie mara moja lakini na Serikali ianze utekelezaji wake mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED S. SINANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nami nafasi ya kuchangia Itifaki na Mikataba iliyopo mbele yetu. Kabla sijasahau, ninaomba kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi ninataka kutilia mkazo zaidi katika Bandari ya Mtwara. Ninapenda kuanza kwa kutoa wasifu wa Bandari hii na niielezee kijiografia kwa faida ya Bunge lako Tukufu. Bandari ya Mtwara ni Bandari ya Asili *(Natural Harbour)*, haikuchimbwa, ina kina cha mita kumi wakati wa maji mafu au *low tide* na ina kina cha mita 14 wakati wa *high tide*. Ina eneo la kuweka makontena 1,000 ambalo limeshafanyiwa *heavy duty pave* linaweza likaweka makontena 1,000.

Bandari hii inaweza ikafunga gati meli mbili kubwa na moja ndogo na ndani ya huba zinakaa meli sita za Kimataifa. Ina mashedi ya kuweza kuhifadhi bidhaa kuanzia tani 15,000 mpaka 20,000; hiyo ndiyo bandari ya Mtwara. *(Makofi)*

Bandari hii iko kilomita 600 kutoka Ruvuma na iko kilomita 1,000 na zaidi kutoka Ruvuma kwenda Dar es Salaam. Bandari hii ya Mtwara ni kilomita 948 kufika Mkata Bay kwa kupitia Tunduru, Songea mpaka Mbambabay na kwenda Malawi. Kutoka Bandari ya Dar es Salaam mpaka Malawi ni kilomita 1648. Sasa kijiografia mizigo ya Malawi ingepaswa kutumia Bandari ya Mtwara. Bidhaa za Ruvuma zingepaswa kwenda Bandari ya Mtwara badala ya ile ya Dar es Salaam na hivi sasa Daraja la Umoja ambalo litakamilika mapema mwakani, litaunganisha Tanzania na Msumbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kijiografia na sifa zote hizi, bado bandari ile iko tupu, haitumiki kabisa inatumika wakati wa korosho tu; hii ni ajabu kubwa sana kwa sababu eti mizigo inapotea, yaani mizigo ikipitia Mtwara itapotea, huko bandari nyingine mizigo haipotei? Sasa isiachwe kutumika Bandari hii eti kwa sababu mizigo itapotea. Tatizo lingine ni kwamba, watakosa kodi, ninaona kwamba, wataongeza wingi wa kodi. Kwa kutumia bandari hii ni kichocheo muhimu sana kwa wawekezaji kuja kuwekeza Mtwara, kwa sababu tutakuwa na umeme wa kutosha kama Mwenyezi Mungu akipenda ukipita huu Muswada ambao utaletwa hapa kesho au keshokutwa, ndiyo kusema tutakuwa na umeme wa kutosha, gesi ya kutosha, tuna uwanja mzuri na bado sisi tuko nyuma kimaendeleo katika nchi hii! Mtuonee huruma, mtutazame kwa jicho la huruma Mtwara, Lindi na Ruvuma, bado tuko nyuma kimaendeleo. Hivi vichocheo ambavyo sisi vinaweza kutupeleka mbele mkiviwekea vikwazo, bado tunabaki palepale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba sana wahusika kama ni *TRA*, Miundombinu au Wizara yoyote, mtusaidie kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna faida kubwa sana kuitumia Bandari ya Mtwara; kwanza, nimeshaeleza kwamba ni kichocheo kikubwa sana cha kuwachochea wawekezaji wa ndani na nje ya nchi hii kuja kuwekeza Mtwara.

La pili, ni kwamba, itapunguza *congestion* ya Bandari ya Dar es Salaam, ambayo haitarajiwi kupungua bali inatarajiwa kuongezeka siku hadi siku. Matatizo ya Dar es Salaam hayatapungua, yataongezeka kwa sababu nchi bado inaendelea na viwanda vinajengwa zaidi. Nchi za jirani kuna amani sasa, kutakuwa na ujenzi mwingi vilevile wa bidhaa za viwanda, kilimo na kadhalika, kwa hiyo, watahitaji Bandari ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, itaongeza zaidi; kuacha kuzitumia Bandari za Mtwara na Tanga na bandari nyingine ni kujitia katika matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaona hakuna sababu ya msingi ya kuacha kutumia Bandari ya Mtwara. Bandari hii kama nilivyokwishasema, nimetoa sifa zake na wenzangu wameshaongea sana juu ya suala hili na juu ya Itifaki hii na Mikataba hii, nisingependa kuongea zaidi; ya kwangu yalikuwa ni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, ambaye ni msemaji wa mwisho kwa jioni hii.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Sitachukua muda mrefu, kwa sababu Mheshimiwa Siraju Kaboyonga na Mheshimiwa Godfrey Zambi wamesema mambo mengi ambayo ningeweza kuyazungumzia. Kwa hiyo, ninataka tufikirie nchi yetu katika uhai wa karne na karne, kwa sababu mambo haya tunapofanya kana kwamba tunafanya kwa leo tunakosea, lazima tufikirie kufanya mambo kwa ajili ya kesho. Labda nifafanue kidogo maelezo aliyoyatoa Mbunge wa Tabora kwamba, Bandari zinazoshindana kwa kanda hii ya kwetu ni Dar es Salaama na Mombasa, lakini sisi tuna bahati kuliko Mombasa, kwa sababu tuna nchi nyingi zaidi ambazo hazina bandari tungeweza kuzihudumia kuliko Kenya.

Sisi ndiyo tunaopakana na Malawi, Zambia, Burundi, Rwanda na hata Kongo na Uganda. Labda niwaambie jambo la Uganda ambalo hamtalifurahia sana na ni aibu kwetu kuwa, tulipokuwa hapa Dodoma wakati ilipokuwa imekaribia *reshuffle* ya Serikali; Waziri wa Mawasiliano wa Uganda na wenzake walikwenda Dar es Salaam, wakawa wameomba Mawaziri wetu wakutane nao kuzungumza. Wao walisema wanasafirisha kupitia Mombasa kwa mwaka mmoja zaidi ya tani milioni tatu, sasa wao wameamua kwao kwamba, nusu ya hiyo ipitie Bandari ya Dar es Salaam na walipokuja kukutana na Mawaziri wetu, hawakuwa na nafasi. Hivi ninavyozungumza, hakuna kiongozi yeyote wa Tanzania, ambaye amekwenda Uganda kufuatilia jambo hili. Kwa hiyo, sisi hatupendi biashara; hatufanyi biashara, hata hii tunayopitisha leo itawanufaisha watu wengine wala siyo sisi. *(Makofi)*

Tumesema hivi duniani kote, ninataka nirudie tena nilisema jambo hili Dar es Salaam; mfanyabiashara mkubwa huwa ni Serikali, wale watu binafsi ni watekelezaji tu.

*Mohamed Enterprises* akinunua dengu kupeleka nje si yeye, inatakiwa Serikali imsaidie kutengeneza mazingira ili afanye kazi nzuri zaidi, hiyo ndiyo kazi na sisi hatuifanyi hapa. Halafu vilevile hii habari ukiizungumza hadharani na wenzetu kama wa Dubai, kwa mfano, wakusikie unazungumza habari ya Bandari kujaa na mizigo haiwezi kutoka ni fedheha kwa sababu mizigo inayopita pale Dubai ni mingi kuliko Bandari ya Dar es salaam, lakini *management* ni *very poor* pale, halafu tuna vyombo vingi sana pale bandarini vinavyofanya kazi moja ukipanga watu wanaotakiwa kufanya maamuzi ili mizigo itoke Dar es Salaam wako wengi kupita kiasi. Kumbe tungepunguza na kuweka utaratibu unaorahisisha mizigo kutoka, hili ndiyo tatizo na kama alivyosema Mheshimiwa Godfrey Zambi na mimi ninasema hivyo hivyo kwamba, hivi tunaponung’unika kwa mfano, kama Waziri Mkuu akienda akasema ninasikita bandari imejaa, *TICS* nao pia kila mtu aseme hivi; sasa nani atafanya kazi kama wote tunalia? Sasa hii nayo pia ni aibu. Sisi tuna bandari tatu, Kenya hawana bandari tatu ; sisi tuna Mtwara ingesaidia kanda yote ile, tuna Dar es Salaam ingesaidia Kanda yote hii na Tanga pia.

Tumekuwa tukizungumza habari ya kujenga reli kutoka Tanga kwenda mpaka Mara kwa ajili ya kuunganisha na wenzetu wa Uganda, imekuwa ni simulizi. Ninashauri kwamba, ingefaa wakati mwingine tukae tuichore nchi yetu, tuseme kutoka sasa *priority number one* iwe ni reli kwa sababu ndiyo inayoweza kusafirisha mizigo mingi. Wenzetu India wana Wizara ya Reli tu, nchi kubwa kama Tanzania hamuwezi kuendesha uchumi wa barabara, uchumi mkubwa wa kusafirisha mizigo ni kwa reli na watu wa kawaida wasafiri waende kwa ndugu zao kwa reli. Siku hizi ukienda Japan au nchi nyingine, treni zinakwenda *speed* kuliko gari, watu wanaweza kuishi Iringa wakafanya kazi Dar es Salaam, kwa teknolojia ya leo sisi bado tunahangaika. Ninasikia kuna jambo la kichekesho eti *Management* Mpya ya Reli tuliyoingia nayo mkataba, wanataka kung'oa reli, yaani wanataka kuzuia na kufunga reli ya Mpanda na Manyoni kwenda Singida; ninashangaa Serikali mnaweza kukubali mambo ya kijinga kama hayo; watu wanafikiria kujenga reli mnakwenda kusimamisha zilizokwisha kujengwa! Inawezekanaje, kama si utani, yaani kwanza ni matusi kwa Serikali; huyo anayependekeza hivi anaitukana Serikali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninataka niseme hiyo ninavyoona na ninavyofikiri, itabidi Wabunge tufikirie kama inawezekana baadaye tuweke Kamati ya Wataalam na Wabunge, tuchunguze kwa nini bandari yetu siyo kama bandari nyingine, kwa sababu haiwezekani tukaachia hivi hivi ni lazima tuisaidie Serikali yetu.

Kwa mfano, *really exporting*, watu mliokwenda Dubai mtashangaa; vitu vyote vinavyouzwa Dubai si vyao na Watanzania tunakwenda nao huko huko, sisi ndiyo tungedhibiti biashara hapa; watu wa Kongo, Zambia, Burundi na Rwanda wasiende Dubai; Dubai yao ni Dar es Salaam. Nimekutana nao wengi Nairobi tulisafiri pamoja wanashangaa, kwa sababu wakija hapa wanapata usumbufu wa ajabu; *bureaucracy*, unyanyasaji, wanasema kwa nini tusiende mahali pengine? Kama mtu atakwenda Dubai, atatumia muda mfupi kuishi pale na kuchukua biashara; kwa nini aje Dar es Salaam kusumbuka bure?

Kwa hiyo, ninaomba kumalizia kwa kusema kwamba, wakati wa sisi Viongozi wa Tanzania kunung'unika umekwisha tuache. Juzi kuna utani mmoja nimepewa pale, wanasema Bwana Mzindakaya tunawapongezeni maana Tanzania tunaona kwa kanda hiyo yenu ndiyo mnaongoza kwa *critics*, yaani sisi tulichosomea ni *criticism*; kila atakayesimama ni *criticism* hakuna the *way forward*! Sasa mimi ninaomba tubadilishe *concept*, Serikali msinung'unike na Wabunge msinung'unike, sasa raia wananung'unika na Wabunge tukija Bungeni tunanung'unika; nani ataiondoa nchi katika matatizo? Sasa hilo ni tatizo. Kule Dar es Salaam Wabunge mtakumbuka nilisema hivi; kule kwetu kuna maji yale yasiyotembea, kuna kama mdudu hivi kwa jina anaitwa *Intengaruzi*, ana mbio kupita kiasi. Kwa hiyo, ukimkuta anakimbia kwa *speed* kubwa sana ndani ya maji, lakini haendi mbele anazunguka hapohapo, yaani humohumo ndani ya maji! Sasa haiwezekani nchi kubwa kama hii, tukawa kama *Intengaruzi* tunazunguka hapohapo; *we have to go forward;* kwa nini tunachelewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. *Actually*, kesho asubuhi tutaanza kupitisha yale Maazimio, kwa sababu walioomba kuzungumza wote wamepata nafasi. Sasa Waheshimiwa Wabunge, mimi ninasema Kanuni mnazo, madaraka ndani ya Katiba mnayo, ninadhani mkiyatumia vizuri, haya mnayoyasema yanaweza kuwa ya vitendo kuliko kuendelea kwa maneno. *(Makofi)*

Baada ya kusema hivyo, ninapenda kuahirisha Bunge leo mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 07.36 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 18 Aprili, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*